TUPO KARIBU SANA!

PASIPO MANENO YA KUJITETEA, NI MADHUMUNI YA KITABU HIKI KUONYA WATU WENGI INAVYOWEZEKANA JUU YA USHAHIDI MWINGI WA KIBIBLIA KWAMBA MWISHO WA ULIMWENGU UMEKARIBIA SANA. MWISHO WA ULIMWENGU NI ULE WAKATI WENYE KUTISHA NA KUOGOFYA WAKATI YESU KRISTO, MTAWALA WA MWANADAMU MWENYE MAMLAKA, ATAKAPOKAMILISHA UTARATIBU WA HUKUMU ILIYOANZA KATIKA BUSTANI YA EDENI WAKATI ADAMU NA HAWA WALIPOSHINDWA KUMTII MUNGU.

HAROLD CAMPING / FAMILY RADIO

Tupo Karibu Sana! (We Are Almost There – Kiswahili)
Na Harold Camping

Maandiko yanatoka katika toleo
la Biblia ya Mfalme Yakobo

Family Stations, Inc.
Oakland, California 94621

Mtandao: www.familyradio.com

Toleo la Kwanza July 2008

Tupo Karibu Sana!

Fahirisi

Utangulizi…….....

Sura ya 1. Neno Tukufu la Mungu……...

Sheria ya Mungu Iliyoandikwa……

Kipindi cha Tatu cha Ufunuo……

Tafsiri ya Biblia……..

Mwishowe, Ufunuo Kamili wa Mpango wa Wokovu wa Mungu……..

Sura ya 2. Biblia Inatoa Ratiba ya Matukio ya Historia…….

Kufunuliwa kwa Mpango wa Wokovu wa Mungu ni Ratiba ya Matukio ya Historia……

Israeli na Miaka kutoka 1447 K.K. mpaka 33 B.K……

Mwanzo wa Nyakati za Kanisa……

Biblia Inatabiri Kanisa lenye Upungufu…….

Tatizo la Shetani ndani ya Makanisa……

Je Biblia Nzima ni Neno la Mungu lisilo na Makosa?.....

Kungekuwapo Mwisho wa Nyakati za Kanisa……

Sura ya 3. Mpango wa Mungu Katika Kukawiza Ufahamu wa Mwisho…….

Sasa Tupo katika Wakati wa Kufahamu……

Umuhimu wa Mahusiano ya Wakati Umeungamanishwa katika Sikukuu za Utaratibu wa Ibada……...

Usahihi wa Matukio Muhimu ya Wokovu……..

Mungu Alitumia Hekalu Kueleza Ukweli wa Kiroho kwa Mifano…….

Habari ya Kuwekwa Wakfu kwa Hekalu Inatoa Habari Muhimu ya Wakati……

Siku ya Nane, Oktoba 21, 2011……

Mtazamo Mwingine katika Sikukuu ya Mahema……

Sura ya 4. Tunaanza Uchunguzi Wetu kwa Ajili ya Ratiba ya Mwisho……

Tarehe ya Mwisho wa Nyakati za Kanisa……

Sura ya 5. Je Ufahamu Wetu Juu ya Ratiba ya Matukio ya Historia Uko Sahihi?……

Maadhimisho ya Miaka 13,000 ya Ulimwengu……

Siku Moja ni Miaka Elfu……

Miezi Mitano ya Mwisho……

Habari ya Kushangaza Zaidi……..

Upatanisho Mpaka Unyakuo: Siku 722,500……

Mathibitisho Zaidi……

Utaratibu wa Hukumu ya Mungu Unaendelea Wakati Mkutano Mkubwa wa Watu Unaokolewa……

Sura ya 6. Je kuna Tumaini kwa ajili Yangu?.....

Wale Ambao Kamwe Hawajawahi Kusikia……

Wale Ambao Wamesikia Neno lakini Ni Watu wa Dhihaka……

Wale Ambao kwa Unyenyekevu Wanaamini Biblia Inatakiwa Kufuatwa……

Mwenye Masikio na Asikie ……..

Utangulizi

PASIPO MANENO YA KUJITETEA, NI MADHUMUNI YA KITABU HIKI KUONYA WATU WENGI INAVYOWEZEKANA JUU YA USHAHIDI MWINGI WA KIBIBLIA KWAMBA MWISHO WA ULIMWENGU UMEKARIBIA SANA. MWISHO WA ULIMWENGU NI ULE WAKATI WENYE KUTISHA NA KUOGOFYA WAKATI YESU KRISTO, MTAWALA MWENYE MAMLAKA JUU YA MWANADAMU ATAKAPOKAMILISHA UTARATIBU WA HUKUMU ILIYOANZA KATIKA BUSTANI YA EDENI WAKATI ADAMU NA HAWA WALIPOSHINDWA KUMTII MUNGU.

Kila mtu ambaye hajaokoka atapitia ghadhabu kamili ya Mungu. Kama Kristo hajalipa adhabu kwa ajili ya dhambi zako, utapitia ghadhabu kamili ya Mungu.

Hakuna mtu anayependa kuongea juu ya habari ya namna hii. Hakuna kitu kinachoweza kuvunja moyo zaidi. Ni rahisi sana kuishi katika kukataa kabisa, kwa siri ukitumaini kwamba haya mazungumzo yote juu ya siku ya hukumu ni mazungumzo tu na hayatakiwi kuchukuliwa kwa uzito kabisa.

Lakini, wakati tunapofahamu kwamba Biblia kwa hakika ni ya kweli na yenye mamlaka, tunaamriwa kuuambia ulimwengu yale yote ambayo Biblia inafundisha juu ya tukio hilo lenye kutisha. Waamini wa kweli katika Kristo hawana chaguo. Lazima wauonye ulimwengu juu ya hukumu inayokuja. Nabii Yona, kwa mfano, aliamriwa na Mungu kwenda Ninawi kuuonya huo mji uliokuwa na ovu kwamba katika siku 40, Mungu angeuangamiza. Yoha hakuwa na furaha hata kidogo kuchukua hiyo habari yenye kutisha kuipeleka Ninawi, lakini, mwishowe alitii. Kwa mshangao, watu wa Ninawi walitubu na kwa unyenyekevu walimsihi Mungu, wakitumaini kwamba Mungu angewahurumia. Na Mungu aliwahurumia, na Mungu hakuangamiza mji wao.

Hali ni ile ile siku hizi, isipokuwa ulimwengu wote upo katika picha. Muda ni chini ya miaka minne, badala ya siku 40. Licha ya kuwa mji wote wa Ninawi ulitubu, ulimwengu wote wa siku hizi hautatubu. Lakini, habari njema ni kwamba Biblia inatangaza kwamba mkutano mkubwa sana wa watu ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, kwa unyenyekevu utamsihi Mungu kwa ajili ya rehema, na mavuno makubwa ya watu, ambao Mungu amechagua kuwaokoa, watapewa uzima wa milele, na wataepuka hukumu ya Mungu, ambayo wanaistahili kwa sababu ya dhambi zao.

Dai la kawaida sana limefanywa, hasa na wale ambao ni wanachama wa makanisa kwamba Kristo atakuja kama mwivi wakati wa usiku. Kwa hiyo, wanashikilia kauli kwamba hakuna mtu atakayevutiwa katika kujaribu kujifunza kutoka kwenye Biblia juu ya kile ambacho Mungu anakisema juu ya wakati wa mwisho wa ulimwengu.

Watu hawa wapendwa wako sahihi. Biblia inafundisha kwamba kwa watu wengi, Kristo atakuja kama mwivi wakati wa usiku. Tunasoma katika 1 Wathesalonike 5:2-3:

Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula, kama vile utungu umjiavyo mwenye mimba, wala hakika hawataokolewa.

Lakini kisha Biblia inasema katika mstari wa 4-6:

Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza. Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe, na kuwa na kiasi.

Mistari hii inafundisha kwamba kuna watu wa aina mbili ulimwenguni ambao wanatambua kwamba huu ulimwengu utakuja kufikia mwisho, wakati ambao Mungu atawatenganisha watu waliookoka na wasiookoka. Makundi yote yanafahamu kwamba watu wasiookolewa watapitia ghadhabu kamili ya Mungu, na kwamba wale ambao wameokolewa watakuwa pamoja na Kristo milele katika furaha na utukufu mwingi.

Kundi moja linajumuisha watu wengi ambao wanaamini wameokolewa, lakini kwa hakika, hawajaokolewa. Hawafahamu kwamba siku hizi Mungu amefunua habari nyingi sana ndani ya Biblia ambazo zinahusiana na ratiba ya matukio ya historia, moja kwa moja mpaka kufika mwisho wa ulimwengu, na hawajali kujaribu kujifunza yale yote ambayo Biblia inayafundisha. Wana uhakika kwamba wameokolewa, na kwa hiyo, kwa hakika hakuna tofauti yo yote kwao ni wakati gani Kristo atakuja. Kwao, Kristo atakuja kama mwivi wakati wa usiku. Lakini kwa huzuni, hii mistari inafundisha kwamba wakati Kristo anapokuja, "**uharibifu wa ghafla"** utakuja juu yao. Lakini ukosefu wao wa moyo wa kutaka kufahamu zaidi inavyowezekana juu ya kile kinachofundishwa na Biblia, wanaonyesha kwamba hawajaokolewa, na bado wanaelekea katika ghadhabu ya Mungu yenye kutisha.

Lakini pia kuna watu wengi sana ambao kwa sababu ya upendo wao na kuiheshimu Biblia, wamejifunza kwamba Biblia inatoa habari nyingi juu ya ratiba ya matukio ya historia. Kwa hiyo, wamejifunza habari nyingi sana juu ya matukio ya nyakati za mwisho, pamoja na ratiba ya haya matukio. Biblia inawazungumzia kama "**walinzi"** (Ezekieli 33:2-9), kwa sababu wanaweza kuonya watu wa ulimwengu wasiookolewa juu ya mwisho wa ulimwengu ambao unakuja na ambao umekaribia sana.

Kitabu hiki kiliandikwa kwa matarajio kwamba, nawe pia utatambua umuhimu kamili wa hatari ambayo ulimwengu upo ndani yake. Hakuna njia ya kubadilisha mpango wa Mungu kwa ajili ya mwisho wa ulimwengu. Lakini, inawezekana kwamba wewe pia unaweza kuwa mmoja wa wale ambao wataepuka ghadhabu ya Mungu kupitia neema ya mpango wake mzuri wa wokovu.

Katika kitabu hiki tutatazama kwa ufupi matendo ya Mungu katika kipindi chote cha historia ya ulimwengu, wakati Mungu anapofunua mpango Wake wa wokovu katika ulimwengu.

Hasa tutaweka mkazo katika kipindi cha mwisho wa historia ya dunia, wakati ambapo matukio mawili makubwa yanatokea kwa pamoja. Haya matukio ni utimilifu wa utaratibu wa hukumu ya Mungu, na wokovu wa mkutano mkubwa sana wa watu, ambao hapana mtu anayeweza kuuhesabu.

Katika kitabu hiki, tarehe za matukio mbalimbali ya kihistoria, pamoja na matukio yajayo zimetolewa. Kwa wale ambao wanataka kuangalia ushahidi zaidi wa Kibiblia kwa ajili ya tarehe hizi, na kujifunza habari za undani juu ya matukio yanayohusiana na tarehe hizi, wanakaribishwa kupiga simu au kuiandikia Redio ya Familia kwa ajili ya vitabu vya bure ambavyo vinaonyesha kwamba habari yote imetoka kwenye Biblia, na haitokani na mawazo au kazi ya kubahatisha ya aina yo yote. Vitabu vinajumuhisha vichwa vifuatavyo:

Wakati Una Mwisho

Mwisho wa Nyakati za Kanisa na Baada

Ngano na Magugu

Mafundisho ya Kwanza ya Masomo ya Biblia

Natumaini Mungu Ataniokoa

Adamu Lini?

Upatanifu Sahihi wa Namba za Wafalme wa Kiebrania

Sura ya 1.

Neno Tukufu la Mungu

Kufahamu wazo lenye kuogofya kwamba ulimwengu upo karibu sana na mwisho wa wakati kunahitaji ufahamu wazi wa asili na mamlaka ya Neno la Mungu, Biblia. Biblia inaweka kanuni za msingi ambazo lazima zifuatwe iwapo tunataka kupokea ukweli kutoka kwa Mungu. Hizi kanuni lazima ziwekwe kabisa ndani ya mawazo ya kila mtu anayetaka kufahamu hili wazo linalotisha.

Biblia ni Neno la Mungu. Katika lugha za asili za Biblia, hasa Kiebrania na Kigiriki, kila neno, na kila herufi ya kila neno, linatoka katika kinywa cha Mungu. Kwa hiyo, wazo kwamba mwanadamu yo yote, au taasisi yo yote ya kanisa, ina mamlaka yo yote juu ya neno lo lote au kifungu cho chote katika lugha asili za Biblia, kamwe halitakiwi kuvumiliwa. Mungu amelinda nakala nyingi sana za kale za lugha asili ya maandiko ya Kiebrania na Kigiriki, ili kwamba tuweze kuwa na uhakika kwamba tunalo Neno asili la Mungu, moja kwa moja kutoka kinywani mwake. Maandiko yaliyotumiwa katika tafsiri ya Kiingereza ya Biblia ya Mfalme Yakobo, pamoja na tafsiri nyingine za wakati huo, ni maandiko ambayo Mungu ameyahifadhi. Kweli, mwalimu makini wa Biblia, wakati anapochunguza fundisho lo lote la Biblia, siku zote lazima aangalie kazi ya mtafsiri na kufanya masahihisho yo yote muhimu, kama kuna masahihisho yo yote yanayohitajika.

Biblia katika ujumla wake ni kitabu cha Mungu chenye mamlaka kubwa kabisa, na kinatakiwa kufuatwa kwa uangalifu sana na kila mwanadamu. Kama kitabu cha sheria ya Mungu, Biblia inaamuru kwamba adhabu ya laana ya kutengwa na Mungu inatakiwa kutolewa kwa kila mtu ambaye amevunja sheria ya Mungu katika njia yo yote (Warumi 6:23; Yakobo 2:10).

Biblia ni ujumbe wa Mungu wa wokovu. Hiyo ni kusema kwamba, kilichojumuishwa katika sheria ya Mungu ni habari ya ajabu kwamba Mungu Mwenyewe, katika nafsi ya Bwana Yesu Kristo, alisimama kwa niaba, au alikuwa mbadala, ambaye alibeba adhabu ya ghadhabu ya Mungu kwa niaba ya wale wote ambao Mungu alikuwa amewachagua ili wapate kuokoka kutoka kwenye adhabu ya dhambi, ambayo ni laana ya kutengwa na Mungu milele.

Biblia ni kamusi yake yenyewe na tafsiri yake yenyewe. Kila neno, sentensi, wazo, n.k., linatakiwa kueleweka kwa kuchunguza matumizi ya neno hilo hilo au wazo hilo hilo kama linavyopatikana mahali pengine ndani ya Biblia. Hakuna hitimisho lo lote kuhusu fundisho lo lote la Biblia litakalo kubalika mpaka liwe limeangaliwa kwa makini kupitia Biblia nzima ili kuhakikisha kwamba kwa pamoja linakubaliana na kila ukweli mwingine wa Biblia. Mungu anaamuru katika I Wakorintho 2:13:

> **Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya binadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.**

Sheria ya Mungu Iliyoandikwa

Kwa rehema za Mungu, Mungu ametoa nakala iliyoandikwa ya sheria ya Mungu. Sheria iliyoandikwa ni Biblia, Neno la Mungu. Sheria pia ni agano la Mungu na mwanadamu, na inarejewa kama Injili na kama Agano la Kale na Agano Jipya. Kwa hiyo, iwe Biblia inatumia maneno "sheria," au "amri," au "Injili," au "agano," au "Neno," bado inaendelea kuzungumzia Biblia peke yake. Haya maneno yote yana maana sawa.

Biblia ilitolewa kwa mwanadamu katika sehemu mbili tofauti, lakini Mungu aliiandika Biblia katika njia ambayo kweli za Biblia zimefunuliwa kwa mwanadamu katika sehemu tatu.

Sehemu ya kwanza ya Neno iliyoandikwa ambayo Mungu aliitoa ilikuwa Agano la Kale. Uandishi wa Agano la Kale ulianza katika mwaka 1447 K.K., wakati Mungu alipowapa Israeli amri kumi pamoja na sheria nyingine nyingi. Wakati huo huo, ndani ya hili agano au kitabu cha sheria, Mungu aliandika kweli nyingi juu ya uumbaji, kuingia kwa dhambi ulimwenguni, na gharika la siku za Nuhu, pamoja na amri nyingi ambazo zilisisitiza hitaji la mwanadamu kwa ajili ya Mwokozi. Mungu aliendelea kuandika Agano la Kale mpaka mwaka 391 K.K.

Lakini Mungu aliandika Agano la Kale katika njia ambayo kiasi kikubwa cha ukweli na habari iliyojumuishwa katika kuandika Agano la Kale kilikuwa hakijafunuliwa wazi kwa mwanadamu. Zaidi, kwa sababu kiwanda cha uchapishaji kilikuwa hakijagunduliwa mpaka karne kadhaa baada ya Agano la Kale kuwa limeandikwa, nakala halisi za sehemu ya kwanza ya Biblia karibu zilikuwa hazipo kabisa. Mwanzoni kabisa, nakala chache sana za sehemu ya kwanza ya Biblia zilikuwa zinapatikana.

Sehemu ya pili ya agano, ambayo inaitwa Agano Jipya, ilianza kuandikwa na Mungu karibu mwaka 33 B.K. Ilikamilika yapata mwaka 95 B.K. Ilitoa kiasi kikubwa cha ukweli ambao ulisaidia kufanya Agano la Kale liweze kueleweka kidogo zaidi. Kimsingi hii ni kwa sababu Agano Jipya lilitoa habari nyingi juu ya Mwokozi Yesu Kristo, wakati alipopitia ghadhabu halisi ya Mungu kwa niaba ya wale wote aliokuwa amepanga kuwaokoa. Pamoja na hayo, Agano Jipya, kama Agano la Kale, liliandikwa na Mungu katika njia ambayo kweli nyingi zilizoelezewa ndani yake zilibakia kuwa zimefichwa kwa waamini wa kipindi cha nyakati za kanisa.[1]

Kwa hiyo, hata kama Biblia imekuwa agano kamili lililoandikwa au kitabu cha sheria kwa takribani miaka 2,000, kweli nyingi muhimu sana ambazo zimeenea katika Biblia nzima kamwe zilikuwa hazijafunuliwa hata kwa wanatheolojia waliokuwa wamejitoa kumcha Mungu ambao walikuwa wana wa Mungu. Hizi siri au mafundisho yaliyofichika hasa yanahusiana na ufahamu sahihi wa mpangilio na asili ya mpango wa wokovu wa Mungu, pamoja na matukio muhimu ambayo yangetokea katika kipindi cha miaka 23 ya mwisho wa historia ya ulimwengu.

---

[1] Tumetumia kifungu cha maneno "nyakati za kanisa" kuonyesha kipindi ambapo Mungu aliyatumia makanisa kuleta Injili.

Kipindi cha Tatu cha Ufunuo

Kwa hali yo yote, siku hizi, wakati ambapo tupo karibu sana na mwisho wa wakati, Mungu kwa mara ya tatu, anafunua ukweli mwingi wa ziada ambao siku zote umekuwa ndani ya Biblia, lakini ulikuwa umebaki kuwa siri katika nyakati zote. Kwa hiyo, karibu ni kana kwamba Mungu ametupa nyongeza katika Agano la Kale na Aganno Jipya, lakini kwa hakika, Biblia haijapata kuongezwa. Kwa hakika hakuna maneno mapya ambayo yameongezwa ndani yake. Biblia tunayoitumia leo, katika lugha ambazo kwa asili Biblia ilikuwa imeandikwa, ni Biblia ile ile ambayo ilikamilika yapata miaka 1,900 iliyopita. Ni kwamba tu sasa hivi, utukufu kamili wa Injili unaweza kuonekana kwa sababu Mungu, siku hizi amefungua ufahamu wetu karibu katika kweli zote ambazo huko nyuma zilikuwa zimefichwa. Katika Waebrania 8:8, Biblia inatangaza:

> **Maana, awalaumupo, asema Angalia, siku zinakuja, asema Bwana, Nami nitawatimizia nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda agano jipya;**

Katika mstari huu, maneno, "**Nami nitawatimizia … agano jipya"** yangekuwa yametafsiriwa "**Nami nitawakamilishia … agano jipya."** Agano jipya ni Agano Jipya la Biblia, lakini ni katika mwisho wa wakati, siku hizi, ambapo Mungu anakamilisha ufahamu wetu wa hilo agano kwa kufungua macho yetu katika kweli nyingi mpya. Siku zote zimekuwa ndani ya Biblia, lakini siku hizi, zinadhihirishwa kwetu, hivyo tunaweza kuzielewa. Ni kana kwamba Mungu anakamilisha uandishi wa agano, ambao ni Biblia. Hii ipo katika kukubaliana kabisa na mstari kama Danieli 12:9:

> **Akasema, Enenda zako, Danieli; maana maneno haya yamefungwa na kutiwa muhuri, hata wakati wa mwisho**.

Tafsiri ya Biblia

Ni jambo la kusikitisha sana kwamba karibu kila kanisa katika ulimwengu wote haliwezi kufahamu kweli nyingi za Biblia. Hii iko hivyo kwa sababu hawaitii miongozo ya Biblia juu ya tafsiri ya Biblia. Aidha, kuna uwezekano mkubwa kwamba waalimu wengi wa Biblia hawafahamu kwamba kila neno katika lugha asili za Biblia linatoka katika kinywa cha Mungu, na kwa hiyo, ni neno lenye umuhimu kupita kiasi na pia lenye usahihi wa hali ya juu.

Njia ya kutafsiri Biblia iliyotengenezwa na mwanadamu ambayo karibu inashikiliwa na kila kanisa, dhehebu, seminari n.k., inatakiwa kukataliwa kabisa. Njia sahihi ya Ki-Biblia juu ya tafsiri ya Biblia imelenga katika ukweli kwamba Biblia inafundisha kuwa Biblia ni kitabu cha kiroho kilichoandikwa katika hali ya dunia hii. Kwa sababu imeandikwa na Mungu, kila tukio la kihistoria, na kila mazungumzo, na kila tukio lililoandikwa ndani ya Biblia kwa hakika ni la kweli na lenye kuaminiwa. Lakini, kwa sababu hizi kauli halisi za kihistoria pia lazima zieleweke kiroho, ujumbe mkuu wa kweli ambao Mungu anautoa kwa mwanadamu ndani ya Biblia hautaeleweka mpaka mafundisho ya kiroho yaliyochunguzwa juu ya mstari huu yawe yamepatikana.

Yesu alizungumzia kanuni ya tafsiri hii katika Marko 4:33-34, ambapo tunasoma:

> **Kwa mifano mingi ya namna hii alikuwa akisema nao neno lake, kwa kadiri walivyoweza kulisikia; wala pasipo mfano hakusema nao; lakini akawaeleza wanafunzi wake mwenyewe mambo yote kwa faragha.**

Yesu ndiye nafsi halisi ya Neno la Mungu. Tunasoma katika Yohana 1:14 kwamba Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu. Kwa hiyo, kanuni ya kutafuta maana ya kiroho ya kila neno na kila kifungu kilichoandikwa ndani ya Biblia inatumika katika Biblia nzima kadiri Kristo anavyohusika na Biblia nzima. Biblia ni Neno la Mungu. Kristo ni Neno la Mungu. Na kwa sababu Biblia ni kitabu cha Mungu, mwanafunzi wa Biblia lazima atafute msaada kutoka kwa Roho Mtakatifu, Mungu Mwenyewe. Mungu peke yake ndiye anayeweza kuleta ukweli katika mioyo yetu (Yohana 16:13). Hitimisho lo lote la kiroho lazima lijaribiwe kwa makini na mwanafunzi wa Biblia ili kuhakikisha kwamba linakubaliana kabisa na ukweli mwingine wo wote unaofundishwa na Biblia.

Kanuni iliyotangulia kwamba Kristo alisema kwa_mifano, na pasipo mfano hakusema, inaonekana kuwa njia kuu ambayo kwayo Kristo anawasaidia waamini wa kweli katika ufahamu zaidi wa Biblia. Lakini pia inaoneka kuwa njia kuu ambayo kwayo Mungu anawapofusha wale wanaoijia Biblia wakiwa na mawazo yao waliyotangulia kuyawaza. Hii kanuni inaelezewa katika Marko 4:11-12 ambapo Mungu anasema:

> **Akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje, yote hufanywa kwa mifano, ili wakitazama watazame, wasione; Na wakisikia wasikie, wasielewe; wasije wakaongoka, na kusamehewa.**

Kwa mfano, mtu ye yote anayefuata tafsiri ya mwanadamu, ambayo inatumika katika makanisa yote ulimwenguni, hatoweza kufahamu kwa usahihi kweli nyingi muhimu za Biblia. Hii inajumuhisha mafundisho ya Biblia juu ya mwisho wa nyakati za kanisa, na ukweli kwamba waamini wa kweli wanaweza kufahamu mambo mengi kuhusu ratiba na habari zote za mwisho wa ulimwengu.

Mwishowe, Ufunuo Kamili wa Mpango wa Wokovu wa Mungu

Kuna maeneo makuu matatu muhimu ya ukweli ambayo yapo katika picha kwa sababu Mungu, siku hizi, anafungua macho yetu katika ukweli mpya mwingi ambao katika kipindi chote cha nyakati za kanisa ulikuwa haueleweki vizuri. Haya maeneo ni kama yafuatayo. (1) Asili na mpangilio wa wokovu wa Mungu. (2) Habari zote za wakati wa mwisho, ambazo zinajumuisha ratiba ya matukio ya historia. (3) Asili na unyofu wa mpango wa hukumu ya Mungu.

Katika uchunguzi huu, tutaweka mkazo kwa hatua kidogo juu ya asili ya mpango wa wokovu wa Mungu. Baadaye, kwa makini tutalenga zaidi katika habari za wakati wa mwisho. Asili na unyofu wa mpango wa hukumu ya Mungu vitatolewa katika kitabu kinachofuata.

Katika Waebrania 8:10-11, Mungu anatuamuru:

> **Maana hili ndilo agano nitakaloagana na nyumba ya Isareli baada ya siku zile, asema Bwana; Nitawapa sheria zangu katika nia zao, na katika mioyo yao nitaziandika; Nani nitakuwa Mungu kwao; nao watakuwa watu wangu. Nao hawatafundishana kila mtu na jirani yake, na kila mtu na ndugu yake, akisema, Mjue Bwana; kwa maana wote watanijua, tangu mdogo wao hata mkubwa wao.**

Mistari hii hasa imelenga juu ya mpango wa wokovu wa Mungu. Katika kipindi chote cha nyakati za kanisa, fundisho lililotawala kwa makanisa mengi ya Biblia lilikuwa kuwaambia ndugu wa mikusanyiko ya waumini, wanaume kwa wanawake <u>jinsi</u> wanavyoweza kuhakikisha wameokolewa au <u>jinsi</u> wanavyoweza kuokolewa. Uchambuzi makini wa mafundisho ya haya madhehebu siku zote huonyesha kwamba wanajumuisha masharti kwamba mchango fulani ufanywe na mtu anayetafuta wokovu. Michango hii inaweza kujumuisha ubatizo wa maji, kukiri wazi hadharani imani yako, tendo la kumkubali Kristo, kushiriki Ekaristi au ushirika mtakatifu, au kuomba maombi ya aina fulani. Karibu katika kila jambo, kulikuwa na ukiukaji wazi wa sheria ya Mungu, ambayo kwa uwazi inatamka kwamba kazi yote ya kumwokoa mtu ilifanywa na Kristo, zamani sana kabla mtu huyo hajazaliwa.[2]

---

[2] Unakaribishwa kuagiza kitabu kidogo bila malipo *Natumaini Mungu Ataniokoa* kwa habari zaidi juu ya hili somo lenye kustaajabisha.

Katika Waebrania 8:10-11, iliyonukuliwa juu, Mungu anasisitiza kwamba mara tu ufunuo kamili wa Biblia unapotokea, mafundisho ya wokovu ulimwenguni kwa pamoja yatakuwa ya Ki-Biblia. Wanadamu hawatafundishwa jinsi wanavyoweza kuokolewa, ila badala yake watafundishwa kwamba wokovu kwa ujumla ni kazi ya Mungu. (Waefeso 2:8-9). Mungu atakuwa akiokoa mkutano mkubwa wa watu ambao kwa hakika wanaweza kuwa na ufahamu kidogo sana wa Biblia.

Tutajaribu kuelezea muhtasari kidogo wa mafundisho ya Biblia juu ya wokovu wa mkutano mkubwa sana ya watu ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, ambao wanaokolewa siku hizi.

1. Biblia inawaamuru waamini wa kweli kupeleka Injili ulimwenguni kote. Mungu ameongoza maendeleo ya mawasiliano duniani kote, kama vile redio na mtandao (intaneti), ili kufanya uwezekano wa kusikia Injili kwa kila mtu ulimwenguni.

2. Katika uongozi wa Mungu usioelezeka, watu wengi wanaofahamu kidogo au wasiofahamu kitu kuhusu ukweli wa Biblia wataanza kutambua yafuatayo:

a. Wao ni watenda dhambi ambao wapo katika njia yao kuelekea katika wakati unaokuja wenye kutisha ambapo watahukumiwa kwa ajili ya dhambi zao.
b. Biblia wanayosikia habari zake, na ambayo wameanza kuisikiliza, lazima itoke kwa Mungu, na kwa hiyo, wanaanza kujaribu kutii maagizo yake.
c. Wanajifunza kwamba siku ya hukumu imekaribia sana, lakini Mungu anaokoa watu wengi sana.
d. Wanaanza kutambua kwamba wanaweza na lazima wamlilie Mungu kwa ajili ya msamaha, wakitumaini kwamba labda Mungu atawaokoa.

Hii ndiyo hali ya sasa hivi ulimwenguni, wakati watu wengi zaidi wanaokolewa kila mahali ulimwenguni, kwa ujumla wanaokolewa kupitia kazi ya Mungu. Wakati Mungu anapomwokoa mtu, anampatia mtu huyo roho mpya iliyofufuliwa milele. Kwa hiyo, wana shauku kubwa inayoendelea kuwa watii kwa Biblia. Ongezeko la ajabu katika idadi ya watu wanaopata kuokolewa, kama Biblia inavyosisitiza (Ufunuo 7:9-14), kwa hakika linahusiana na ukweli kwamba sasa hivi Mungu anafunua kweli nyingi sana za Biblia, ambazo vizazi vilivyopita havikufahamu.

Sura ya 2.

Biblia Inatoa Ratiba ya Matukio ya Historia

Kwa kuchunguza Biblia nzima kwa makini, tumejifunza kwamba Biblia siyo tu kitabu cha sheria kinachoelezea sheria zote ambazo kwazo Mungu anatawala wanadamu wote, bali pia ni kitabu ambacho kimetolewa kwa wanadamu ili kwamba waweze kujua ratiba ya Mungu ya matukio ya historia. Tunasoma katika Mhubiri 8:5-7:

> **Ashikaye amri hatajua neno baya; na moyo wa mwenye hekima hujua wakati na hukumu. Kwa maana kwa kila shauri kuna wakati na hukumu; kwa sababu mashaka ya mwanadamu yaliyo juu yake ni makubwa; kwa kuwa hajui yatakayokuwako; kwa maana ni nani awezaye kumweleza jinsi yatakavyokuwa?**

Katika mistari hii, neno “hukumu” ni neno lenye maana sawa na neno “sheria.” Kwa hiyo, inafundisha kwamba kwa kusoma Biblia, mwamini wa kweli siyo tu anajifunza sheria ya Mungu, hasa wakati inapohusisha utaratibu wa hukumu ya Mungu, bali pia, anajifunza mambo mengi kuhusu ratiba ya Mungu kwa ajili ya dunia.

Kwa sababu hiyo, mwamini wa kweli anaweza kufahamu mambo mengi kuhusu utaratibu wa matukio ya historia, ikiwa ni pamoja na kweli nyingi juu ya wakati wa mwisho wa ulimwengu. Kwa wale ambao hawafuati njia ya Ki-Biblia ya kutafsiri Biblia, Kristo atawajia kama mwivi wakati wa usiku. Mara moja, mateso yao yataongezeka sana wakati wanapotambua, wamechelewa mno, kwamba mwisho wa ulimwengu umekuja. Hakutakuwapo tena na huruma au neema, au wokovu kwa watu ambao hawajaokolewa. Hivyo, tunasoma katika 1 Wathesalonike 5:2-6:

> **Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula, kama vile utungu umjiavyo mwenye mimba, wala hakika hawataokolewa. Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza. Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe, na kuwa na kiasi.**

Na tunasoma katika Ufunuo 3:3:

Basi kumbuka jinsi ulivyopokea, na jinsi ulivyosikia; yashike hayo na kutubu. Walakini usipokesha, nitakuja kwako kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako.

Katika mistari hii, Mungu anatufundisha kwamba wale wanaosoma Biblia wamegawanyika katika watu wa aina mbili. Kuna wale ambao wameridhika na ufahamu wao wa sasa hivi wa uhusiano wao na Mungu. Wanafahamu kwamba siku moja ulimwengu utafika mwisho, lakini ufahamu wao ni kwamba ratiba ya siku ya mwisho inajulikana tu kwa Mungu peke yake. Kwa hiyo, wanafikiri kwamba wanadamu hawahitaji kuwa na hofu juu yake. Kwao, kwa hakika Kristo atakuja kama mwivi wakati wa usiku. Lakini, ujio wake kwa watu hawa, ni kwa ajili ya kuwaangamiza. Inatisha sana!

Kwa upande mwingine, kuna wale ambao wamekuja kutambua kwamba Mungu ametupa habari nyingi katika Biblia kuhusu ratiba ya matukio ya historia. Kwa hiyo, wamejifunza mambo mengi sana kutoka kwenye Biblia kuhusu ratiba ya uumbaji wa ulimwengu pamoja na matukio mengine mengi muhimu yaliyoandikwa kwenye Biblia. Pia wamejifunza mambo mengi sana kuhusu ratiba halisi ya mwisho wa ulimwengu. Kwao, wakati wa mwisho wa ulimwengu hautakuwa wa ghafla.

Kufunuliwa kwa Mpango wa Wokovu wa Mungu ni Ratiba ya Matukio ya Historia

Biblia inafundisha jinsi Mungu alivyotoa ujumbe wa Injili kwa wanadamu katika kipindi chote cha ratiba ya matukio ya historia. Injili inajumuisha Biblia nzima. Kwa hiyo, kwa kuchunguza Biblia kwa makini, tunajifunza kwamba kufunuliwa kwa mpango wa wokovu wa Mungu ni ratiba ya matukio ya historia.

Kwa miaka 9,500 ya kwanza ya historia ya ulimwengu, Mungu hakutumia mfumo wo wote wa kidunia ili kuwakilisha ufalme wa Mungu katika ulimwengu huu. Katika kipindi hicho, Mungu siku zote alifanya kazi kupitia waamini binafsi ambao walikuwa wawakilishi wa ufalme wake. Habili, Enoko, ambaye alichukuliwa mbinguni, Nuhu na familia yake. Ibrahimu, Isaka, Yakobo, na Yusufu ni majina ambayo Mungu ameyaandika ndani ya Biblia kama wawakilishi wa ufalme wa Mungu.

Wakati tunapochunguza Biblia kwa makini, tunatambua kwamba ulimwengu uliumbwa karibu miaka 13,000 iliyopita.[3] Biblia iko sahihi kabisa, kwa hiyo tunapolinganisha kalenda ya Biblia na kalenda yetu ya siku hizi, tunafahamu kwamba mwaka wa uumbaji ulikuwa 11,013 K.K.

---

[3] Unakaribishwa kuagiza kutoka Redio ya Familia kitabu kinachotolewa bure *Adamu Lini* ambacho kinaonyesha jinsi Biblia inavyotoa habari hii.

Katika uwezekano wote, katika kipindi cha kwanza cha miaka 9,500 ya historia ya dunia, watu wachache sana walipata kuokolewa. Kwa mfano, katika siku za Nuhu, katika ulimwengu wote uliokuwapo katika mwaka 4,990 K.K., wakati Mungu alipoiangamiza dunia kwa gharika, kulikuwa na watu wanane tu waliookolewa.

Israeli na Miaka kutoka 1447 K.K. mpaka 33 B.K

Walakini, katika mwaka 1447 K.K., Mungu alifanya badiliko kubwa katika mfumo wake wa kuufanya ufalme wa Mungu kuwakilishwa juu ya dunia hii. Katika huo mwaka, Mungu alianza kutumia taifa la Israeli katika kuwakilisha ufalme wa Mungu. Ilikuwa katika mwaka 1447 K.K., ambapo Israeli, wakiwa chini ya uongozi wa Musa, walitoka katika utumwa wao kwa Wamisri. Taifa la Israeli lilijumuisha vizazi vya Ibrahimu, ambaye alikuwa amezaliwa miaka 700 kabla. Ibrahimu alizaliwa mnano mwaka 2167 K.K., kama raia wa Uri wa Wakaldayo au Babeli. Katika mwaka 2092 K.K., yeye na mke wake, Sara, katika kutii agizo la Mungu, walikwenda katika nchi ya Kanaani. Wakawa waanzilishi wa taifa la Israeli, na nchi ya Kanaani ilitumiwa na Mungu kama kiwakilishi cha duniani cha ufalme wa Mungu.

Taifa la Israeli, pamoja na nchi ya Kanaani, vikawa kiini cha kufunuliwa kwa mpango wa wokovu wa Mungu katika kipindi cha miaka 2,100 iliyotangulia kuzaliwa kwa Kristo. Ukweli ni kwamba Yesu, Mwana wa Mungu alipokea asili yake ya ubinadamu kama uzao wa moja kwa moja wa Ibrahimu.

Kufikia mwaka 1447 K.K., vizazi vya Ibrahimu, walioitwa Israeli, waliongezeka kuwa taifa lenye uwezo wa takribani watu milioni mbili. Ilikuwa ni katika huo mwaka ambapo walitoka katika utumwa wa Misri. Na kwa miaka 1,480 iliyofuata, Israeli iliitwa watu wa Mungu. Walikuwa wamepewa sheria za Mungu nyingi sana. Walikuwa wawakilishi wa nje wa ufalme wa Mungu duniani.

Mungu alilipa taifa la Israli nchi, nchi ya Kanaani, ambayo pia inaitwa nchi ya Israeli, kama mahali pa kuishi, na hekalu, na masinagogi ya kuabudia. Aliwapa sheria, ambazo kiteolojia, tunaziita sheria za utaratibu wa ibada, ambazo zilitakiwa kuadhimishwa kwa sababu hizi sheria ziliwaekeleza Waisraeli kwa Masiha anayekuja, Yesu Kristo. Utaratibu wa sheria za ibada ulijumuhisha mambo kama vile kuadhimisha siku za sikukuu, miezi mipya, sabato za siku ya saba, sadaka za kuteketezwa, sadaka za damu, n.k.

Mungu alitumia vitu vya kidunia kama vile Kanaani, Israeli, Yuda, Yerusalemu, Sayuni, hekalu, Uyahudi, n.k., ili kuonyesha ufalme wa Mungu kwa nje. Kwa hiyo, maneno haya haya yametumika mara kwa mara ndani ya Biblia katika kuwakilisha ufalme wa Mungu kiroho. Kwa mfano, katika kipindi cha nyakati za kanisa, makanisa yalikuwa yakiwakilisha ufalme wa Mungu kwa nje. Kwa hiyo, kila mara Biblia inatumia maneno kama Israeli, Yuda, hekalu, n.k., katika kuzungumzia makanisa katika nyakati za kanisa.

Sehemu muhimu ya taifa la Israeli ilikuwa jumla ya sheria ambazo Mungu alizitoa kuhusu uteuzi wa makuhani, Walawi, manabii, na wafalme ili kutawala juu ya taifa zima. Lilikuwa chombo kitakatifu kilichoanzishwa na Mungu Mwenyewe ili kuwakilisha kwa nje ufalme wa Mungu hapa duniani. Kila Myahudi ambaye alikuwa uzao wa Ibrahimu moja kwa moja alikuwa mwanadamu wa huu mkusanyiko mkubwa. Ili kudhihirisha huu uanachama, kila mwanaume alitahiriwa, ambapo ilikuwa sheria nyingine ya utaratibu wa ibada iliyoelezewa na sheria ya Mungu.

Mungu anatupa habari nyingi kuhusu miaka ambayo moja kwa moja ilitangulia mwanzo wa taifa la Israeli pamoja na miaka yake elfu moja ya kwanza ya historia. Biblia inatoa habari zote kuhusu Israeli, kama taifa, wakati Mungu alipowakomboa kutoka utumwani na kuwatoa Misri, wakati kwa muujiza walipovuka Bahari ya Shamu katika nchi kavu, na kutembea miaka 40 jangwani, na kisha kuvuka mto Yordani katika nchi kavu. Kisha Biblia inatoa habari muhimu juu ya miaka 360 ya historia yao iliyofuata, wakati Mungu alipotawala juu yao, akitumia watu walioitwa waamuzi, katika nchi ya Kanaani.

Kisha tunapewa habari zote juu ya miaka 116 iliyofuata, wakati Israeli ilipokuja katika sifa yake kuu ya kidunia, wakati walipotawaliwa na Mfalme Sauli, ambaye alifuatiwa na Mfalme Daudi, na mwishowe Mfalme Sulemani.

Habari muhimu pia inatolewa ndani ya Biblia kuhusu mgawanyiko wa taifa moja lililokuwa limeunganika, lililojumuisha mataifa 12 ya Israeli, kuwa mataifa mawili. Mara baada ya kifo cha Mfalme Sulemani, makabila kumi yalikuwa ufalme unaojitegemea ulioitwa Israeli, na hatimaye mji wake mkuu ulikuwa katika Samaria, na makabila mawili yaliyobaki yakawa taifa la Yuda, na mji wake mkuu ulikuwa Yerusalemu. Biblia inatupa habari nyingi juu ya falme hizi na wafalme waliowatawala.

Pia Biblia inatupa habari muhimu juu ya mwisho wa mataifa haya. Mataifa kumi ya taifa la Israeli yalipigwa na Waashuri katika mwaka 709 K.K., Kisha katika mwaka 587 K.K., taifa la Yuda lilipigwa na Wababeli, wakati ambapo mji wa Yerusalemu na hekalu zuri lililojengwa na Mfalme Sulemani viliharibiwa.

Lakini, baada ya kuharibiwa kwa Yerusalemu katika mwaka 587 K.K., habari za mapito ya makabila 12 zilikuwa kidogo sana. Tunajifunza kwamba katika mwaka 539 K.K., karibu watu 40,000 walionusurika katika mji wa Yuda uliokuwa umeharibia na Wababeli, walirudi Yerusalemu. Tunajifunza habari chache kuhusu kujengwa upya kwa hekalu, jitihada zilizokamilika mwaka 515 K.K. Tunajifunza juu ya mapito machache ya Wayahudi waliorudi katika nchi ya Israeli, hasa kutoka katika vitabu ndani ya Biblia, vinavyoitwa Ezra, Nehemia, na Esta.

Lakini baada ya hapo kwa karibu miaka 400 ya historia, kutoka mwaka 391 K.K., mpaka mwaka wa 8 K.K., Biblia iko kimya kabisa kuhusu nchi ya Israeli, wakazi wake, na kwa jambo hilo, kila taifa lo lote lingine ulimwenguni.

Kwa huzuni, katika kipindi chote cha kuwepo kwa Israeli, kwa hakika ni watu wachache sana waliopata kuokolewa. Biblia imejawa na kauli zinazohusu dhambi, ukanaji wa imani, na uasi wa taifa la Israeli dhidi ya sheria za Mungu. Hata wakati Kristo alipokuja kama Mwokozi,

ambaye katika asili yake ya uanadamu alikuwa uzao wa Ibrahimu, waliasi, na hawakumtazama kama Masiha wao. Kwa hakika, mwishowe walimwua (Matendo 2:22-23).

Biblia inatuhakikishia kwamba Kristo ambaye ni tunda la ajabu alizaliwa na taifa la Israeli. Ni kupitia taifa la Israeli ambapo Mungu alichukua asili ya mwanadamu, akazaliwa na bikira Mariamu, ambaye alikuwa wa kabila la Yuda.

Katika mwaka wa 8 K.K., kwa mara nyingine Biblia ilianza kutupatia habari nyingi juu ya taifa la Yuda. Katika mwaka huo, kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji kulitangazwa, na alikuwa Yohana ambaye alitakiwa kuutangazia ulimwengu kwamba Masiha, Bwana Yesu Kristo, Mwana-kondoo wa Mungu, alikuwa amekuja kuchukua dhambi za ulimwengu. Kwa hakika, Yesu Kristo, ndiye njia pekee ambayo kwayo mtu ye yote ulimwenguni anaweza kupata kulipiwa adhabu ya dhambi zake, na hivyo kupatanishwa na Mungu milele.

Kutoka wakati wa kuzaliwa kwa Yesu katika mwaka wa 7 K.K., mpaka karibu mwaka 65 B.K., Biblia inatoa habari nyingi kuhusu taifa la Israeli. Ni katika kipindi hiki cha wakati ambapo matukio mengi ya kustaajabisha katika historia ya ulimwengu yalitokea. Mungu, Bwana Yesu Kristo, alichukua asili ya mwanadamu kwa kuzaliwa na bikira Mariamu. Katika kipindi hiki cha wakati, Yesu alihubiri karibia miaka mitatu na nusu. Yesu Kristo alisulubiwa katika mwaka wa 33 B.K. Alifufuka kutoka kwa wafu na akapaa tena mbinguni. Huo mwaka, 33 B.K., ulitia alama mwisho wa kipindi cha miaka 1,480 kipindi ambacho taifa lote la Israeli lilikuwa kusanyiko ambalo kwa nje liliwakilisha ufalme wa Mungu.[4]

Mwanzo wa Nyakati za Kanisa

Siku chache baada ya kupaa kwa Kristo mbinguni, jumuiya kubwa takatifu ambayo ilikuwa iwakilishe ufalme wa Mungu kwa miaka 1,955 iliyofuata, ilipata mwanzo wake.

Katika siku ya Pentekoste katika mwaka wa 33 B.K., karibu watu 3,000 waliokolewa. (Matendo 2). Wale waliokolewa siku hiyo walitoka katika mataifa mengi mbalimbali. Hili tukio kubwa liliweka alama ya mwanzo wa nyakati za kanisa. Ilikuwa ni katika sehemu hii ya kwanza ya nyakati za kanisa ambapo habari zaidi zimetolewa juu ya wamisionari kutumwa katika nchi ambazo sasa hivi tunazifahamu kama Uturuki, Ugiriki na Italia. Nyakati za kanisa zilielezewa na Mungu kama mpango mtakatifu ambapo kwa huo Mungu angepeleka Injili ulimwenguni kote. Masinagogi ya Kiyahudi, mji wa Yerusalemu, taifa la Israeli, au hekalu katika mji wa Yerusalemu visingeweza tena kuwa kiwakilishi cha nje cha ufalme wa Mungu. Makanisa na mikusanyiko yake ambayo ingeundwa katika ulimwengu wote ingewakilisha ufalme wa Mungu kwa nje. Kwa hiyo, kiroho, kila mara Biblia inayaita makanisa na mikusanyiko yake, “Yerusalemu,” “hekalu,” “Sayuni,” Yuda,” “Uyahudi,” n.k.

---

[4] Unakaribishwa kuagiza vitabu vinavyotolewa bure *Mwisho wa Nyakati za Kanisa… na Baada* na *Ngano na Magugu* kwa ajili ya taarifa zaidi kuhusu mwisho wa nyakati za kanisa

Hii jumuiya takatifu, ambayo mwishowe ilijumuisha makanisa yaliyopatikana kila mahali ulimwenguni, ilikuwa imepangwa kwa makini na Mungu. Na Mungu aliweka masharti makali katika kitabu chake cha sheria, ambayo yalitawala uchaguzi wa viongozi na mashemasi (1 Timotheo 3). Wanawake hawakutakiwa kufundisha au kuwa na mamlaka katika mikusanyiko. Sheria za utaratibu wa ibada za Agano la Kale, ambazo zilitakiwa kuadhimishwa na taifa la Israeli, hazikutakiwa kuadhimishwa tena. Badala yake, sheria mbili mpya za utaratibu wa ibada zilitangazwa ili kusaidia katika kufundisha asili ya Injili. Kulikuwapo na ubatizo wa maji pamoja na Chakula cha Bwana. Sheria kuhusu kutengwa kutoka kwenye uanachama wa kanisa ilitangazwa (1 Wakorintho 5). Jumapili iliteuliwa na Mungu kama siku ya Jumapili ya Sabato, ambayo ilitakiwa kutumiwa kwa ajili ya shughuli zote za kiroho. Kila kanisa ambalo lingeanzishwa kila mahali ulimwenguni lilitakiwa kuongozwa na sheria zilizotangazwa katika Biblia.

Jukumu kubwa lililotolewa katika haya makanisa ambayo yalikuwa yameamriwa na Mungu lilikuwa kupeleka Injili katika ulimwengu wote. Kwa hiyo, tayari, kama ambavyo tumeona, kabla hata Biblia haijakamilika, wamisionari tayari walikuwa wakitumwa katika mataifa jirani (Matendo 13).

Mnamo mwaka 95 B.K., Mungu alikamilisha uandishi wa Biblia, na hakuna habari zaidi iliyotoka kwa Mungu ikielezea maendeleo halisi ya kanisa ulimwenguni kama habari ya kihistoria. Lakini, zamani sana kabla ya nyakati za kanisa kuanza, Mungu alitabiri jinsi ambavyo nyakati za kanisa zingeendelea kiroho.

Mtu angeweza kutegemea kwamba pamoja na mwanzo wenye heri wa nyakati za kanisa katika Pentekoste mwaka 33 B.K., ambapo karibu watu 3,000 waliokolewa katika siku moja (Matendo 2), maendeleo ya nyakati za kanisa yangekuwa historia ya kutambulika yenye mafanikio. Lakini, Biblia inatabiri kwamba huu haukuwa mpango wa Mungu. Kwa huzuni tunajifunza kutoka kwenye Biblia kwamba hata kabla Mungu hajamaliza kuandika Biblia (karibu mwaka 95), tayari kulikuwapo na ushahidi uliokuwa unaongezeka kwamba nyakati za kanisa hazitakuwa historia yenye mafanikio makubwa.

Biblia Inatabiri Kanisa lenye Upungufu

Katika Ufunuo 2 na Ufunuo 3, Mungu anatwambia juu ya hali ya kiroho ya makanisa saba yanayofanana sana kwa asili. Hizi hali zilikuwapo karibia miaka 30 baada ya haya makanisa kuundwa. Kwa mfano, kanisa la Efeso lilikuwa limepoteza upendo wake wa kwanza (Ufunuo 2:4-5). Kumbuka, kumpenda Mungu ni kushika amri zake (Yohana 14:21-23). Kwa hiyo, Mungu alitoa onyo kuondoa kinara chao, ambacho kinawakilisha nuru ya Injili, kwa sababu walikuwa hawashiki tena sheria za Mungu. Hili kanisa lisingetumiwa tena na Mungu katika kepeleka Injili ulimwenguni.

Katika Wagalatia 1:2-9, Biblia inatoa taarifa kwamba tayari, kabla ya Biblia kumalizika, makanisa ya Galatia yalikuwa yameanza kufuata injili ambayo haikuwa Injili ya Biblia. Katika

Ufunuo 2:13, Biblia inatoa taarifa kwamba kanisa la Pergamo tayari lilikuwa kanisa ambalo Shetani alikuwa anatawala ndani yake kwa kiasi fulani. Hii mistari inatoa rejeo kwa “kiti” cha Shetani. Katika Biblia, neno “kiti” katika mazingira ya namna hii, linamaanisha utawala au kumiliki. Na katika Ufunuo 3:1-4, Biblia inatoa taarifa kwamba kanisa la Sardi tayari lilikuwa kanisa lililokuwa limekufa, licha ya kuwa lilikuwa na waamini wachache waliokuwa wamebaki ndani yake.

Katika Mathayo 13:24-30, Biblia inaandika mfano wa ngano na magugu. Ngano iliwakilisha waamini wa kweli katika makanisa. Magugu yaliwakilisha watu wasioamini ambao walitoa kila ushahidi wa kuwa waamini wa kweli, kiasi kwamba ni katika mwisho wa nyakati za kanisa peke yake ambapo Mungu angetoa njia ambayo kwayo ngano ingetenganishwa kutoka kwenye magugu. Hii inamaanisha kwamba katika kipindi chote cha nyakati zakanisa, kungekuwapo na magugu, wale ambao bado walikuwa watumwa wa Shetani, ambao walinuia kufanya kazi sana makanisani. Kwa hiyo, kupitia kwao, Shetani angeweza kutawala ndani ya makanisa licha ya kuwa kimadaraka rasmi, Kristo alikuwa mtawala wa makanisa.

Tayari katika Isaya 9:1-4, Mungu alitabiri kwamba kipindi cha kanisa kisingepata historia yenye mafanikio makubwa. Hapo tunasoma:

> **Lakini yeye aliyekuwa katika dhiki hatakosa chamgamko. Hapo kwanza aliiingiza nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali katika hali ya kudharauliwa, lakini zamani za mwisho ameifanya kuwa tukufu, karibu na njia ya bahari; ng’ambo ya Yordani, Galilaya ya mataifa. Watu wale waliokwenda katika giza, wameona nuru kuu; wale waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti, nuru imewaangaza. Umeliongeza taifa, umezidisha furaha yao; wanafurahi mbele zako, kama furaha ya wakati wa mavuno, kama watu wafurahivyo wagawanyapo nyara. Kwa maana umeivunja nira ya mzigo wake, na gongo la bega lake, na fimbo yake yeye aliyemwonea, kama katika siku za Midiani.**

Katika mistari hii, Mungu anaongea juu ya nuru kuangaza ng’ambo ya Yordani kama “Galilaya ya mataifa” (pia angalia Mathayo 4:15-16). Hiyo ni kusema kwamba, mataifa yote ya ulimwengu yalitakiwa kuwa chini ya nuru ya Injili. Hiyo nuru, kwa hakika, ni Bwana Yesu, ambaye ndiye nuru ya ulimwengu (Yohana 1:7-10).

Kwa sababu nuru ya Injili ilikuwa iangaze katika ulimwengu wote, badiliko kubwa katika mpango wa Injili ya Mungu lingetokea kwa sababu giza la kiroho la ulimwengu lingechomwa na nuru hii (Isaya 9:2). Ingekuwa nuru ambayo ingekuja kuwa hai katika ulimwengu wote, kundi kubwa la watu ambao kwa nje wangeonekana kuwa waamini wa kweli katika Kristo, kama Isaya 9:3 unavyotangaza, “**Umeliongeza taifa**.” Kwa maneno mengine, ukubwa wa nje wa ufalme wa Mungu ambao ungeendelezwa kila mahali ulimwenguni ungekuwa mkubwa.

Lakini, katika mstari huo huo, Mungu alitabiri kwamba hajaongeza furaha ya mavuno. Furaha ya mavuno ni furaha ambayo huja wakati mtu anapokuwa amepewa uzima wa milele, kwa namna hiyo amekuwa mwamini wa kweli (Luka 15:10). Kama furaha ya mavuno haipo, inaweza tu kumaanisha kwamba mavuno ya waamini wa kweli ni machache sana. Ukweli ni

kwamba, kama tunavyoona, hili tumaini la ukosefu wa mavuno makubwa ya watu kupata kuokolewa na kuja katika ufalme wa Mungu limetabiriwa katika maeneo mengi ndani ya Biblia.

Zaidi katika marejeo yote ya Biblia ambazo tayari tayari tumeisha yaona, tunasoma katika Isaya 5 kwamba Mungu anasimulia nyakati za kanisa kama shamba la mizabibu ambalo limepandwa kwa makini na kwa uzuri sana na Mungu Mwenyewe. Lakini hili shamba la mizabibu halikuzaa matunda mazuri. Lilizaa zabibu-mwitu. Kiroho, zabibu-mwitu zinahusiana na wale watu ambao wamebuni injili yao wenyewe badala ya kufuata kwa makini Injili ya Biblia. Baadaye katika uchunguzi huu, tutaona kwamba ulikuwa ni mpango wa Mungu ambapo kwa sababu ya huu uovu, Mungu mwishowe ataliangamiza shamba la mizabibu.

Itakumbukwa kwamba katika sura nyingi za vitabu vya Isaya, Yeremia, na Ezekieli, n.k, Mungu anaonyesha hasira yake kubwa dhidi ya mataifa ya Israeli na Yuda kwa sababu ya kuendelea kwa maovu yao. Kwa hakika, mwishowe, waliteketezwa. Israeli iliteketezwa na Waashuri katika mwaka 709 K.K., na Yuda katika mwaka 587 K.K., iliteketezwa na Wababeli.

Mungu aliwatumia Israeli na Yuda, ambao katika kipindi chao walikuwa wawakilishi wa nje wa ufalme wa Mungu, kama mfano wa makanisa yote ambayo kwa nje yamewakilisha ufalme wa Mungu katika wakati wote wa nyakati za kanisa. Wakati tunapochunguza hivi vitabu vya Biblia vya Agano la Kale, kwa hakika tunasoma kile alichokiazimia Mungu kwa nyakati za kanisa, na hasa zaidi kwa ajili ya mwisho wa nyakati za kanisa.

Kwa hiyo, Mungu anafundisha kwamba makanisa yalitakiwa kuanzishwa kila mahali ulimwenguni katika kipindi chote cha nyakati za kanisa, akitoa mwelekeo kwamba nyakati za kanisa zilikuwa zimefanikiwa sana. Lakini kwa hakika, mabaki peke yao, sehemu ndogo ya watu wote katika makanisa, ndio kwa hakika waliopata kuokolewa, yaani, kwa hakika kuwa waamini wa kweli

Wazo hili hili linaelezewa katika Warumi 9:27, ambapo Mungu ananukuu kutoka Isaya 10:22-23.

> **Warumi 9:27: Isaya naye atoa sauti yake juu ya Israeli, kusema, hesabu ya wana wa Israeli, ijapokuwa ni kama mchanga wa bahari, ni mabaki yao tu watakaookolewa.**

> **Isaya 10:22-23: Maana watu wako, Ee Israeli, wajapokuwa wengi kama mchanga wa pwani, ni mabaki tu watakaorudi; kuangamiza kumekusudiwa, kunakofurika kwa haki. Kwa maana Bwana, BWANA wa majeshi, atayatimiza maangamizo yaliyokusudiwa katika nchi yote**.

Tatizo la Shetani ndani ya Makanisa

Sababu moja kubwa kwa ukosefu wa mafanikio ya kiroho katika nyakati za kanisa ilikuwa tatizo la Shetani. Wakati wa msalaba, Shetani alipewa pigo la kifo. Alifukuzwa kutoka mbinguni (Ufunuo 12:7-11), na alifungwa ili asiweze kuwadanganya mataifa katika kipindi chote cha nyakati za kanisa, ambacho kiishara kilielezewa kama kipindi cha miaka 1,000 (Ufunuo 20:1-3). Miaka 1,000 lazima ieleweke kama ishara au namba ya kiroho inayomaanisha "ukamilifu." Kipindi halisi alichofungwa kilikuwa miaka 1,955 (kutoka mwaka 33 B.K., mpaka mwaka 1988).

Kufungwa kwa Shetani kulimaanisha kwamba katika njia yo yote asingeweza kuzuia mpango wa Mungu katika kuokoa wale ambao mwanzoni kabisa mwa wakati Mungu alikuwa amewachangua kwa wokovu. Lakini ukweli kwamba Shetani alikuwa amefungwa haikumzuia kuzunguka zunguka kama simba angurumaye, akitafuta mtu anayeweza kummeza (1 Petro 5:8). Hiyo ni kusema kwamba, wakati wa kipindi cha kanisa, kwa ujumla mpango wa Mungu ambapo kupitia huo Injili ilitakiwa kuufikia ulimwengu wote, ungekuwa umezuiwa sana na Shetani katika mafanikio yake ya kiroho. Angeweza kuzuia mafanikio ya makanisa kwa kupanda magugu au majani katikati yao (Mathayo 13:24-30). Hiyo ni kusema kwamba, Shetani akifanya kazi kama **"malaika wa nuru"** angeweza kuleta "**watumishi wake wa haki**" katika kila kanisa (2 Wakorintho 11:13-15).

Katika Ufunuo 6:4, anaonyeshwa kama mpanda farasi juu ya farasi mwekundu akibeba upanga mkubwa, ambao ni Upanga wa Roho, Biblia, ambapo kwa huo angeondoa amani kutoka duniani. Kwa maneno mengine, angetumia maneno kutoka kwenye Biblia ili kujaribu kutoa mamlaka katika mafundisho yake ya uongo.

Wakati tunapopatanisha kwa makini hizi kumbukumbu zote za Biblia, tunajifunza kwamba, kwa hakika, kutoka katika mtazamo wa nje, wakati wa kanisa ulifanikiwa sana, kwa sababu kanisa baada ya kanisa lilitoa taarifa kwamba idadi kubwa ya watu iliokolewa. Lakini, kwa hakika, mabaki tu ya wale waliopata kuwa wanachama walioungama katika ushirika kamili ndani ya kanisa, ndio hakika waliopata kuwa waamini wa kweli.

Baraka kubwa sana ulimwenguni katika kipindi cha nyakati za kanisa yumkini ilikuwa uchapishaji na usambazaji wa mamia ya mamilioni ya Biblia katika ulimwengu wote. Biblia, nuru ya Injili, ilipelekwa kila mahali ulimwenguni, licha ya kuwa idadi ya wale waliopata kuwa waamini wa kweli katika nyakati za kanisa ilikuwa ndogo.

Kwa hiyo, unabii unaotisha wa Mathayo 7:21-23 utakuja katika ukweli ulio wazi katika siku Mungu anapoleta ghadhabu yake juu ya watu wa ulimwengu ambao hawajaokolewa. Na kwa huzuni, hiyo inajumuisha wale wote ambao bado wapo katika kanisa lo lote mahali po pote ulimwenguni wakati unyakuo unapotokea, yaani, wakati waamini wa kweli wanaponyanyuliwa juu ili kumlaki Bwana hewani. Katika mistari hii Mungu anatangaza:

> **Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa**

pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo, nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.

Kutoka katika mtazamo wetu mkubwa wa kuweza kutazama nyuma katika kipindi chote cha kanisa, tunaweza kuona ukweli wa kauli ya unabii wa Mungu juu ya ukosefu wa mafanikio ya nyakati za kanisa. Kweli, kilianza na mafanikio makubwa katika mwaka 33 B.K., katika siku ya Pentekoste ambapo karibu watu 3,000 waliokolewa. Lakini kama ambavyo tayari tumekwishaona, ndani ya makanisa yaliyokuwa yameanzishwa hata kabla Biblia ilipokuwa haijamalizika, uasi ulikuwa tayari unaonekana wazi. Kadhalika, Shetani alikuwa tayari anatawala katika makanisa mengi kwa kuyapandikiza magugu ndani ya makanisa hayo. Makanisa katika Ufunuo 2 na 3 yalikuwa mfano wa makanisa yote ambayo yangekuja kuwapo katika kipindi chote cha nyakati za kanisa la Agano Jipya.

Zaidi, wakati tunapochunguza historia ya kanisa, kamwe hatujifunzi juu ya wakati wa uaminifu mkubwa katika Biblia. Historia ya kanisa imejawa na taarifa za kutokuwa waaminifu katika Biblia. Alama kubwa ya kuonyesha kutokuwa na uaminifu kwa Biblia yumkini ilikuwa katika wakati wa Mgawanyiko wa Kanisa, ambao ulitokea Ulaya karibu miaka mia nne mpaka miaka mia tano iliyopita. Kwa wakati huo katika historia, kanisa lililokuwa na nguvu lilikuwa kanisa Katoliki. Hali ilikuwa mbaya sana katika uvunjaji wake wa sheria za Biblia kiasi kwamba wanaume Wakatoliki kama Martin Luther, na John Calvin walililiacha kanisa Katoliki na wakawa waanzilishi wa makanisa ya Kiprotestanti. Mengi ya makanisa haya ya Kiprotestanti kwa bidii walijaribu kuwa waaminifu ilivyowezekana katika mafundisho ya Biblia.

Lakini, haikuchukua muda mrefu makanisa mengi ya Kiprotestanti yakawa yanafundisha mpango wa wokovu uliobuniwa na mwandamu ambapo mtu ye yote anaweza kumpokea Kristo kama Bwana na Mwokozi wake na kwamba hili tendo lilizaa wokovu. Mtazamo katika uamsho mkubwa wa zamani unadhihirisha kwamba msingi wa wengi wao ulikuwa injili ya namna hiyo. Kwa huzuni, haikuwa Injili ya Biblia. Licha ya hili, Mungu aliokoa watu wachache katika kipindi cha nyakati za kanisa.

Je Biblia Nzima ni Neno la Mungu Lisilo na Makosa?

Ukweli kabisa kwamba miongoni mwa madhehebu mengi ya Kiprotestanti yaliyokuwa yamejitokeza huko, ni kutokukubaliana kwingi juu ya sehemu nyingi za mafundisho ya Biblia ikionyesha kwamba kila dhehebu lilichagua mistari kutoka kwenye Biblia ambayo hasa waliipenda, na kisha walikuza imani zao na maungamo yao kutoka katika mistari hii. Kila dhehebu lilisisitiza kwamba mistari waliyokuwa wameichagua ilikuwa yenye uhakika na haikuwa na makosa. Kwa hiyo, ilionekana kwamba mahitimisho ya kiteolojia ambayo yaligeuka kanuni za imani ya kanisa lao, na ambayo yalitokana na kulinganisha ufahamu wao wa hii mistari waliyokuwa wameichagua, yote kwa pamoja yalikuwa kweli na yenye kuaminiwa.

Lakini kile kilichoonekana kuwa kweli na kuaminiwa siku zote hakikuwa kweli na chenye kuaminiwa. Kwa bahati mbaya, mara nyingi sana, hii mistari waliyokuwa wameichagua kama msingi kwa ajili ya maungamo yao, ilieleweka vibaya kwa sababu Biblia nzima haikuangaliwa na hawa wanateolojia wa kanisa. Hawakuchunguza Biblia nzima kwa makini, kwa kulinganisha Maandiko kwa Maandiko, ili kuhakikisha kwamba matihimisho yao yalikuwa sahihi. Ilionekana kwamba waliamini kuwa Biblia nzima ilikuwa haina makosa, lakini kwa hakika, waliweka tumaini lao tu katika hiyo mistari waliyokuwa wameichagua ili kuthibitisha mafundisho yao. Kwa hiyo, kwa hakika, walikataa mamlaka ya kila mstari katika Biblia nzima.

Matokeo ya huku kuamini Biblia kwenye makosa, yalikuwa ni kutoa injili ya wokovu ambayo kutoka siku hadi siku ilikuwa mbali na ukweli. Hiyo ndiyo maana katika kipindi chote cha nyakati za kanisa kumekuwapo na ufahamu tofauti mwingi wa mafundisho ya Biblia kupitia madhehebu mbalimbali. Kwa mfano, Wabaptisti hawakubaliani na Walutheri, Walutheri hawakubaliani na Wapresibiteri, Wapresibiteri hawakubaliani na Wabaptisti, n.k., juu ya mafundisho mengi ya Biblia.

Tunafahamu Biblia ni kweli na yenye kuaminiwa kuhusiana na kila fundisho la Biblia, na kwa hiyo, kunaweza kuwepo tu na jibu moja. Kwa hiyo, kama mitazamo kadhaa kuhusiana na fundisho fulani ilikuwa imeshikiliwa na madhehebu mbalimbali, si zaidi ya dhehebu moja la haya madhehebu lililokuwa linaongea ukweli, na mengine yote yalikuwa yakihubiri uongo.

Kwa upande mwingine, kama haya madhehebu yaliamini kwamba Biblia nzima ni Neno la Mungu lisilo na makosa, na kanuni za imani yao lazima ziwe chini ya mamlaka ya Biblia peke yake na katika mapana yake, baada ya hapo kimsingi mtu angeweza kutegemea kwamba mwishowe madhehebu yote yangeweza kufundisha kila fundisho katika njia ile ile ambayo kila kanisa lingine lilifundisha fundisho hilo.

Pia, kumekuwapo na mgawanyiko mkubwa wa makanisa, kama vile Wakatoliki Wamormoni, Wasabato, na makanisa ya miujiza ya siku hizi ambao kwa uwazi wanatangaza kwamba mafundisho ya kanisa lao ni zao la Biblia na mafunuo yanayokuja kutoka kwa Mungu, ujumbe ambao ulitolewa baada ya Biblia kukamilika. Kwa hiyo, kwa tamko lao hilo, wana mamlaka ambayo inajenga na kubainisha ufahamu wao wa Biblia ambao ni tofauti na mamlaka ya Mungu, ambayo ni Biblia peke yake na katika ujumla wake (Ufunuo 22:18-19). Kwa hakika lazima tutambue kwamba kamwe kusingekuwapo na nyongeza yo yote katika Biblia mara tu ilipokuwa imekamilika yapata miaka 1,900 iliyopita.

Kama tulivyoonyesha mapema, Mungu aliazimia na kutabiri kwamba kwa ajili ya sababu zote hapo juu, unabii ungekuja kutimia kama Mungu alivyotangaza, “**Wanafurahi…kama furaha ya wakati wa mavuno”** (Isaya 9:3). Ingawa Israeli, yaani, makanisa ulimwenguni kote, yangekuwa kama mchanga wa bahari, mabaki tu ndio ambao wangeokolewa (Warumi 9:27).

Kungekuwapo Mwisho wa Nyakati za Kanisa

Mungu alitabiri kwamba mwishowe, kungekuwapo na mwisho wa nyakati za kanisa, na baada ya hapo Mungu angekamilisha mavuno ya wateule wake, wale waliokuwa wamechaguliwa na Mungu ili wapate kuokolewa (Waefeso1:3-6), kwa kuleta Injili kwa watu waliokuwa nje ya mamlaka ya kanisa.

Wakati tunapoichunguza Biblia, tunaona kwamba Biblia inafundisha kuwa kutakuwapo na dhiki ya mwisho, ambayo katika Mathayo 24:21 inaitwa “dhiki kubwa.” Hapo tunasoma:

Kwa kuwa wakati huo kutakuwepo dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe.

Zaidi sana, tunaishi katika kipindi kwenye historia ambapo tunaweza kuangalia nyuma karibu miaka 2,000 iliyopita ya historia iliyokuja baada ya Biblia ilipokuwa imekamilika. Kama tulivyojifunza mapema katika uchunguzi huu, habari ya kihistoria iliyopo kutoka katika vyanzo visivyo vya Ki-Biblia kuhusu historia ya makanisa, inatuonyesha kwamba nyakati za kanisa hazikuwa na mafanikio kama vile Biblia ilivyokuwa imetabiri.

Lakini hilo linatuleta katika swali kubwa. Siku zote imeeleweka kwa wanafunzi wa Biblia kwamba mwishowe, kungekuwapo na mwisho wa ulimwengu huu, kipindi ambacho watu wasiookolewa wangepokea adhabu kamili ya ghadhabu ya Mungu, na watu waliookolewa milele wangekuwa salama na Kristo katika mbingu mpya na dunia mpya. Zaidi, kwa kawaida imekuwa ikiaminika kwamba mwisho wa ulimwengu ungekuja wakati ambapo Kristo angekuja kama mwivi wakati wa usiku. Yaani, ilieleweka kwamba, kwa usahihi wo wote, hatuwezi kufahamu wakati wa mwisho. Hii ilikuwa hivyo licha ya kuwa katika nyakati mbalimbali kwenye historia, ambapo mateso mengi ya Wakristo zaidi yalikuwa yanaonekana wazi katika baadhi ya maeneo ya ulimwengu, kuna wale ambao walithubutu kubahatisha kwamba walijua mwaka wa kurudi kwa Kristo. Kwa hakika, kwa kila namna, walithibitika kutokuwa sahihi. Hii ilikuwa hivyo kwa sababu hawakujenga hitimisho lao juu ya uchambuzi makini wa kila kitu kinachosemwa na Biblia juu ya kurudi kwa Kristo.

Kwa hakika, katika kipindi chote cha nyakati za kanisa imeonekana kwamba ufahamu wa kawaida wa makanisa ulikuwa kwamba makanisa yangeendelea mpaka mwisho kabisa wa wakati, na kwa ghafla, huu ulimwengu ungekuja kufikia mwisho wake kwa kuwa Kristo angekuja kama mwivi wakati wa usiku.

Badiliko kubwa la wazo hili lilikuwa maarufu sana katika karne iliyopita wakati mafundisho yaliyoitwa kabla ya millennia yalipofundishwa, hasa katika makanisa ya Kibaptisti. Hiyo imani ilitangaza kwamba Kristo angekuja kama mwivi wakati wa usiku na kulinyakua kanisa, yaani, kuchukua watu wote ndani ya makanisa kuwapeleka mbinguni. Wakati huo huo au muda mfupi baada ya hapo, kungekuwapo na kipindi cha miaka saba ya dhiki kubwa. Mara tu kufuatia hiki kipindi cha miaka saba, Kristo angerudi kimwili katika dunia ya sasa hivi ili kutawala miaka 1,000 katika mji halisi wa sasa hivi wa Yerusalemu. Baada ya kipindi hiki cha miaka 1,000, mwisho wa ulimwengu ungekuja. Fundisho la namna hii, ambalo kwa ujumla lina makosa, linawezekana kwa sababu kuna sura nyingi sana, hasa katika Kitabu cha Ufunuo, ambacho kwa hakika kinaongea juu ya mwisho wa ulimwengu lakini ni sura ambazo ni ngumu

sana kueleweka. Ni katika siku hizi tu ambapo tunaweza kuanza kuelewa kwa uwazi haya marejeo ya Ki-Biblia katika siku za mwisho wa nyakati.

Sura ya 3.

Mpango wa Mungu Katika Kukawiza Ufahamu wa Mwisho

Kwa hakika Biblia inatufundisha kwamba isingekuwa rahisi kufahamu habari yo yote ndani ya Biblia ambayo inatoa habari zote za mwisho wa ulimwengu mpaka ambapo kwa hakika ulimwengu ungekuwa karibu sana na mwisho wake. Kwa mfano, mistari mingi sana katika Kitabu cha Danieli inazungumzia mwisho wa ulimwengu, lakini Mungu anapasha habari katika Danieli 12:9:

> **Akasema, Enenda zako, Danieli; maana maneno haya yamefungwa na kutiwa muhuri, hata wakati wa mwisho.**

Kwa maneno mengine, siyo mpaka tulipokuja katika wakati ambapo tulikuwa karibu sana na mwisho wa ulimwengu ambapo waamini wa kweli wangefahamu habari kubwa kuhusu habari za Injili ya nyakati za mwisho ulimwenguni. Lilikuwa kusudi la Mungu kwamba mara tu kabla ya ulimwengu kuja katika mwisho wake, ndipo habari ya aina hiyo ingeweza kupatikana kwa waamini wa kweli ambao mwishowe wangeifanya ipatikane ulimwenguni.

Njia moja ambayo Mungu ameitumia kufanya habari za nyakati za mwisho zisifahamike ni kuruhusu karibu makanisa yote kukubali tafsiri iliyotengenezwa na mwanadamu, yaani, njia ya kutafsiri Biblia iliyotengenezwa na mwanadamu, ambayo inafanya kiasi kikubwa cha habari za Biblia kuwa ngumu kueleweka katika mawazo ya wanateolojia. Kumbuka, tuliangalia ukweli huu wenye kusikitisha mapema katika uchunguzi huu.

Biblia kwa uwazi inatufundisha kwamba pasipo mfano, Kristo hakuongea (Marko 4:34). Mfano ni hadithi ya kidunia yenye maana ya mbinguni au kiroho. Hiyo ni kusema kwamba, Biblia kwa ujumla ni kitabu cha kiroho. Ni Neno la Mungu, na Kristo ndiye maana halisi ya Neno la Mungu (Yohana 1:14). Kwa sababu imeandikwa na Mungu, habari zote za kihistoria, mazungumzo yaliyoandikwa, na hadithi fupi zinazofahamika juu ya mtu au watu au tukio la kweli, kwa hakika ni za kweli na zenye kuaminika. Lakini kufahamu kwamba hili tukio la kihistoria kwa hakika lilitokea, ni sehemu tu ya hazina kubwa ya ukweli kwamba kwa hakika Biblia ni ya kweli. Kila mazungumzo, kila hadithi fupi, kila neno la Biblia kwa makini lilikuwa limepangwa na kukusudiwa na Mungu ili kufundisha kweli muhimu sana za kiroho.

Kutafuta ukweli wa kiroho kunahitaji kiasi kikubwa cha uchunguzi wa Biblia, kulinganisha Maandiko kwa Maandiko (1 Wakorintho 2:13). Pia kunahitaji Mungu Roho Mtakatifu kufungua macho ya kiroho ya wanaotafuta ukweli. Kama ambavyo imekwishaonekana, halikuwa kusudi la Mungu kufunua kweli nyingi za Biblia, yaani, kufungua kuyafunua masikio ya kiroho ya wanaotafuta ukweli, mpaka ilipokuwa karibu sana na mwisho wa wakati. Katika kupunguza shida ya huu upofu katika kipindi chote cha nyakati za kanisa,

Mungu hakuonekana kuwa tayari kufungua macho ya kiroho ya waalimu wa Biblia wa makanisa yanayopatikana kila mahali ulimwenguni. Kwa hiyo, kwa mfano, wao hawatambui kwamba wanachunguza Biblia kwa kutumia njia ya tafsiri ya Biblia ambayo kwa jumla ni ya uongo.

Mfano mwingine unaweza kutolewa kuhusu Mungu alivyoyaacha makanisa yasielewe habari nyingi sana za Biblia katika kipindi chote cha nyakati za kanisa. Wale ambao Mungu alikuwa amefungua macho yao ya kiroho kwa hakika wanafamu kwamba kila neno katika lugha asilia za Biblia linatoka katika kinywa cha Mungu, na kwa hiyo, kwa hakika ni la kweli na lenye kuaminiwa. Watafsiri wanaweza kufanya makosa katika kutafsiri, lakini neno la Kiebrania au Kigiriki ambalo limetafsiriwa kamwe halitakiwi kusailiwa.

Tatizo la kusaili Kiebrania au Kigiriki asilia hasa limekuwa likisumbua katika kuwianisha namba za Biblia. Kwa mfano, wanateolojia wameshindwa kupatanisha kipindi cha utawala wa wafalme fulani kama kilivyoandikwa katika mstari mmoja ndani ya Biblia na habari iliyotolewa sehemu nyingine ndani ya Biblia. Kwa hiyo, kila mara wamehitimisha kwamba lazima kuna makosa ya uandishi, yaani, wakati fulani, walipokuwa wakinakili maandiko asili ya Biblia, mwandishi kwa bahati mbaya alibadili kidogo herufi kutoka katika herufi za namba asili, na hivyo ikaifanya kuwa namba ambayo haipo katika maandishi ya asili, na hayo makosa yaliendelea wakati nakala zaidi zilipotengenezwa. Kwa hiyo, wanasema kwamba kwa hakika hatuwezi kuamini kila namba iliyoandikwa katika Biblia.

Tabia ya namna hiyo juu ya Biblia inamaanisha kwamba kwa hakika hatuwezi kuamini mambo ya Biblia. Kama kosa la aina hiyo linawezekana kwa namba ambayo imeandikwa katika Biblia, basi pia lingeweza kuonekana kuhusiana na neno lo lote katika Biblia, na tungetakiwa kuhitimisha kwamba hakuna sehemu ya Biblia ambayo kwa hakika ni ya kuaminiwa.

Lakini, ili kutoa mamlaka katika mistari wanayoitumia katika kufundisha kile wanachotaka kufundisha, waalimu wa Biblia wanatangaza kwamba Biblia haiwezi kukosea na haina makosa. Kama waliamini Biblia nzima ilikuwa haina makosa, kamwe wasingeongea juu ya mambo kama vile makosa ya uandishi. Hawafahamu kwamba Mungu amelinda Neno lake kiasi kwamba kosa la uandishi lisingetokea. Kwa sababu kwa makusudi Kristo aliongea kwa mifano ili kuficha ukweli, na kwa sababu Mungu amewaruhusu wanateolojia wa makanisa kusaili usahihi wa baadhi ya maneno ndani ya Biblia, kweli nyingi zilizoandikwa ndani ya Biblia zimebaki zimefichika.

Hii ni mifano miwili tu, miongoni mwa njia nyingine kadhaa, juu ya jinsi ambavyo Mungu ameendeleza kuzuia kweli fulani za Biblia mpaka pale anapochagua kufunua kweli hizi. Lazima tufahamu kwamba hakuna mtu anayeweza kudai kwamba ulikuwa uwezo wa ufahamu wake au utakatifu wake au unyofu wake uliomsaidia kuifahamu Biblia vizuri. Lazima tufahamu kwamba Mungu peke yake ndiye anayeweza kufungua macho yetu katika kweli ambazo Mungu amezificha katika Biblia. Na pasipo swali, Mungu ana ratiba yake kufanya hivi.

Lazima tuzingatie kwamba Mungu alimaliza kuandika Biblia yapata miaka 2,000 iliyopita. Lakini ulikuwa mpango wa Mungu kwamba kweli nyingi za Biblia hazikutakiwa kufahamika kwa mtu ye yote mpaka karibu sana na mwisho wa wakati. Na bado, kwa karibu miaka 2,000, wanafunzi waaminifu wa Biblia, wenye bidii na waliojitoa, ambao kwa hakika walikuwa wameokolewa, walikuwa na njia ya kuifikia Biblia, na wamejaribu kwa nguvu sana kuifahamau sana Biblia kwa kadri ilivyowezekana.

Kwa hiyo, tunaweza kuanza kuona kwa nini Mungu aliiandika Biblia katika njia ngumu aliyoifanya. Kwa mfano, tunafahamu kwa nini Mungu aliruhusu makanisa yote kuikubali njia ya tafsiri ya Biblia yenye makosa sana. Ni kwa sababu tu tupo karibu na mwisho wa wakati, na sasa hivi ni kusudi la Mungu lililonenwa ili kutupatia hizi kweli za ziada, kwamba tunaweza kufahamu ukweli zaidi wa Biblia kuliko wanafunzi wa Biblia wa zamani.

Sasa Tupo katika Wakati wa Kufahamu

Sasa, tumefika katika wakati huo. Kwa hiyo, mistari ndani ya Biblia ambayo awali imekuwa siri sasa hivi inaeleweka. Karibu kila siku ukweli mpya unamiminika kutoka kwenye Biblia. Matokeo yake ni ufahamu mkubwa zaidi wa mpango wa Mungu kwa ajili ya mwisho wa ulimwengu. Kwa kufuata kanuni ya Biblia ya kulinganisha Maandiko kwa Maandiko, na kutambua kwamba lazima tutafute ukweli wa kiroho uliofichika ndani ya kila mfano na kila hadhithi fupi na kila tukio la kihistoria lililoandikwa katika Biblia, Mungu anafungua macho yetu ili tufahamu aina zote za ukweli ambao awali umekuwa umekataliwa na wengi wanaotafuta ukweli wa Biblia kwa bidii. Sasa hivi tunaweza kutambua mpangilio wa Biblia kwa ajili ya matukio ya mwisho wa ulimwengu. Huu uwezo wa kufahamu ukweli zaidi wa Ki-Biblia umekuja tu kwa sababu ni katika wakati huu wa historia ambapo Mungu anafungua macho ya waamini wa kweli ambao kwa makini wanachunguza Biblia yote kwa ajili ya ukweli.

Lazima tukumbushwe na Biblia kwamba lilikuwa kusudi la Mungu kwamba habari ya namna hii siku moja ingefahamika kwa waamini wa kweli. Kumbuka tamko la Mungu la Mhubiri 8:5-7:

> **Ashikaye amri hatajua neno baya; na moyo wa mwenye hekima hujua wakati na hukumu. Kwa maana kwa kila shauri kuna wakati na hukumu; kwa sababu mashaka ya mwanadamu yaliyo juu yake ni makubwa; kwa kuwa hajui yatakayokuwako; kwa maana ni nani awezaye kumweleza jinsi yatakavyokuwa?**

Katika mistari hii, Mungu anatufundisha kwamba, mwanadamu kwa asili hafahamu ratiba ya siku ya kufa kwake au habari za utaratibu wa hukumu ya Mungu kwa ajili ya mwisho wa ulimwengu. Lakini, katika maisha ya mwamini wa kweli, mtu mwenye roho ya hekima, ni kusudi la Mungu kwamba atafahamu wakati na hukumu.

Ukweli ni kwamba waamini wa kweli watafahamu kiasi kikubwa cha habari za wakati kutoka kwenye Biblia, lakini waamini wa kweli wamepata tu kufahamu ukweli huu siku hizi. Vivyo hivyo, kwa mfano, ni katika wakati wetu kwamba waamini wa kweli wametambua kalenda yote ya historia kutoka kwenye Biblia, kwa kuanza na uumbaji katika mwaka 11,013 K.K.

Kanuni iliyoelezewa katika Mhubiri 8 imetangazwa zaidi katika 1 Wathesalonike 5:2-6, ambapo tunasoma:

> **Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula, kama vile utungu umjiavyo mwenye mimba, wala hakika hawataokolewa. Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza. Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe, na kuwa na kiasi**

Hii mistari inafundisha kwamba wale ambao wameridhika na ufahamu wao wa Biblia wa wakati huu, au falsafa zao za maisha ya wakati huu, ambazo zinajumuisha wazo kwamba hawahitaji kuogopa siku ya hukumu, kwao, Kristo atakuja kama mwivi wakati wa usiku. Hawana ufahamu au imani na habari za wakati zinazotolewa na Biblia.

Kwa upande mwingine, wale ambao wanakesha na kuwa makini, yaani, ambao wana mawazo mazuri kwa sababu Mungu amewapa roho mpya iliyofufuliwa, watafahamu mambo mengi kuhusu tabia na wakati wa kurudi kwa Kristo.

Hii kanuni imeelezewa zaidi katika lugha ya Amosi 3:7, ambapo Mungu anasema:

> **Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake.**

Tukiwa na kanuni hizi akilini, tunafahamu kwamba tunaruhusiwa kutazamia matukio ya mwisho wa historia ya ulimwengu. Kwa hakika, hizi kweli, ambazo tunaamini zinahusiana na mwisho wa ulimwengu, hazitakiwi tu kutoka kwenye Biblia, bali pia lazima zisimamie uchunguzi makini sana wa Biblia.

Biblia kwa uwazi inatwambia kwamba Kristo atakuja kama mwivi wakati wa usiku (2 Petro 3:10; 1 Wathesalonike 5:2). Katika kipindi chote cha nyakati za kanisa, kanisa limefundisha hivi. Kwa kusimamia juhudi zao nzuri katika kuielewa Biblia, waalimu wa Biblia, wacha Mungu, pamoja na wanateolojia kwa usahihi wamesisitiza kwamba lazima tujali sana wokovu wetu binafsi kwa sababu hatuna uhakika kwamba kesho tutakuwa hai. Kadhalika, makanisa mengi yalifundisha kwamba lazima pia tutambue kuwa mwisho wa ulimwengu na kurudi kwa Kristo katika hukumu ni mambo ambayo yanaweza kutokea wakati wo wote.

Lakini, kama ambavyo tayari tumeishaonyesha, katika kipindi chote cha nyakati za kanisa, hapakuwapo na ufahamu wazi wa ratiba ya matukio ya historia ya Biblia. Hakuna mtu aliyeweza kuthibitisha mwaka halisi wa uumbaji, mwaka wa mafuriko ya siku za Nuhu, mwaka ambao Ibrahimu alitahiriwa, siku na mwaka wa ubatizo wa Kristo, n.k.

Huu ukosefu wa ufahamu sahihi wa mpangilio wa matukio yaliyopita, pamoja na ufahamu wa mpangilio wa kurudi kwa Kristo, ulikuwa umepangwa kwa makini na Mungu. Hii inaonyeshwa katika Danieli 12, ambapo tunasoma kwamba Danieli, ambaye alikuwa amepewa ufahamu wa habari nyingi za wakati wa mwisho, aliambiwa "**yafunge maneno haya, ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho"** (Danieli 12:4).

Lakini sasa tupo katika wakati wa mwisho, na Mungu amefungua macho yetu ya kiroho katika umuhimu wa habari kama zile zilizoandikwa katika Mhubiri 8:5-6 na katika Amosi 3:7.

Kwa hiyo, kama ambavyo tumeona awali, Biblia inatufundisha katika 1 Wathesalonike 5:2-6 kwamba watu wengi siku hizi wataendelea kusisitiza kwamba Kristo atakuja kama mwivi wakati wa usiku, kwa kutambua tu kwamba wao ndio wanaolengwa na ghadhabu ya Mungu.

Kwa sababu sasa hivi tupo karibu na mwisho wa wakati, hii mistari ni ya muhimu sana. Kwa neema ya Mungu, siku hizi tunaweza kufunua ratiba ya matukio ya historia kupitia uchunguzi makini wa Biblia. Siyo tu kwamba Biblia imetufunulia habari nyingi kuhusu ratiba halisi ya matukio ya kihistoria yaliyopita yaliyoandikwa katika Biblia, bali pia imetupatia habari nyingi za nyakati kuhusiana na matukio ambayo lazima yatokee mwishoni kabisa mwa ulimwengu.

Hatutakiwi kushangazwa kwamba hii iko hivi. Wakati Mungu alipoangamiza dunia yote (katika) wakati wa Nuhu, Alihakikisha kwamba ulimwengu wa wakati ule umefahamu kwamba hili tukio lenye kutisha, maangamizi ya ulimwengu wote kupitia gharika kubwa, lilikuwa linakuja, na pia, kufahamu siku halisi ambayo lingetokea. Nuhu hakuwa tu mjenzi wa safina kubwa, ujenzi ambao ungefahamika sana katika ulimwengu wa wakati ule, bali Nuhu mwenyewe alikuwa "**mhubiri wa haki"** (2 Petro 2:5). Siku saba kabla ya gharika kuanza, Mungu alimpatia Nuhu tarehe halisi ambapo gharika ingeanza (Mwanzo 7:4,10,16).

Kadhalika, wakati Mungu alipokuwa karibu kuangamiza mji mwovu wa Ninawi, Mungu alimtuma nabii Yona kuuonya mji kwamba katika siku 40, baada ya Yona kuanza kuuonya mji, mji ungeangamizwa (Yona 3:4).

Kadhalika, lazima tutambue kwamba leo, Mungu anatoa habari kuhusu ratiba halisi ya mwisho wa ulimwengu. Habari hizi ni lazima zitoke katika Biblia peke yake. Leo Biblia haina tofauti yo yote ile na Biblia iliyokamilika zaidi ya miaka 1,900 iliyopita. Lakini kwa sababu haukuwa mpango wa Mungu kufunua habari hizi mpaka mwisho wa wakati, habari zote kuhusu wakati wa mwisho wa ulimwengu zilikuwa zimefichika sana ndani ya maandiko ya Biblia. Kwa hiyo, haikuwa rahisi hata kwa wanafunzi waaminifu wa Biblia kuelewa habari hizi.

Lakini, siku zote umekuwa ni mpango wa Mungu kwamba karibu na mwisho wa wakati, hii habari mpya kuhusu wakati lazima ipatikane katika ulimwengu. Kwa kuwa ushahidi wote wa Biblia sasa hivi unaonyesha kwamba tupo karibu na mwisho wa wakati, tunaweza kuwa na uhakika kwamba hii habari muhimu ya wakati lazima sasa hivi iwe inapatikana, na kwa hakika, lazima itolewe kwa ulimwengu wote.

Kwa kuchunguza kwa makini habari yote inayotolewa na Biblia kuhusu matukio ya historia yaliyoandikwa ndani ya Biblia, tunawezeshwa kufahamu vizuri sana juu ya mpangilio na asili ya matukio yanayokuja, moja kwa moja mpaka siku ya mwisho ya kuwepo kwa dunia.

Tunaweza kueleza kwa muhtasari misingi kadhaa ya ukweli ambao Biblia inatufundisha, nayo ni kama ifuatavyo:

1. Biblia ni kitabu changanuzi sana. Haijaandikwa katika hali ya kuthibitisha mawazo changanifu au fikira za falsafa (2 Petro 1:20). Biblia imeandikwa kama kitabu cha uhandisi, ambapo ndani yake ukweli unatolewa kama jambo ambalo limetendeka au limefanywa kwa uhalisi.
2. Kila namba iliyoandikwa katika Biblia iko sahihi. Licha ya kuwa namba inaweza kuwa ngumu kueleweka, kamwe haiwezi kuangaliwa kama ina makosa.
3. Kuna usahihi mkubwa katika kutokea kwa matukio ya historia. Kwa mfano, Israeli walikuwa Misri kwa kipindi halisi cha miaka 430. Israeli walikuwa jangwani wakisafiri kutoka Misri kwenda Kanaani kwa kipindi halisi cha miaka 40.
4. Mara kwa mara, lakini siyo siku zote, Mungu hutumia namba fulani za Biblia katika kuonyesha ukweli wa kiroho. Yesu Kristo anadokeza maana ya kiroho ya namba katika Mathayo 18:21-22. Wakati Petro alipomwuliza Yesu ni mara ngapi amsamehe ndugu yake, Yesu alitumia namba kutoa maelezo ya jibu lake. Anasema katika mstari wa 22:

…Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini.

Kwa sababu siku zote tunatakiwa kusameheana sisi kwa sisi, tunaweza kuona kwamba Yesu anatumia namba kuonyesha ukweli wa kiroho. Hizi namba zingeweza kusimama peke yake au kuwa sehemu ya namba kubwa. Hii kwa nguvu inasaidia katika kupatanisha na kuunganisha pamoja matukio yanayofanana ambayo yametokea miaka mingi tofauti. Ifuatayo (hasa) ni orodha ya namba hizi.

2 – Wale ambao wameagizwa kuleta Injili

3 – Kusudi la Mungu

4 – Mfiko wa mbele kabisa katika wakati au umbali ambao Mungu anao kiroho katika picha

5 – Upatanisho, ambao unasisitiza hukumu na wokovu

7 – Utimilifu kamili wa kusudi la Mungu

10 – Ukamilifu wa cho chote kilicho katika picha

11 – Ujio wa kwanza wa Kristo, 11,000 baada ya uumbaji

12 – Utimilifu wa cho chote kilicho katika picha

13 – Mwisho wa ulimwengu, habari ambazo zilianza miaka 13,000 kamili baada ya uumbaji

17 – Mbinguni

23 – Ghadhabu au hukumu ya Mungu

40 – Majaribu

43 – Ghadhabu au hukumu ya Mungu

Mfano wa jinsi tunavyoweza kugundua ukweli wa kiroho kwa njia ya namba kubwa ambayo inaweza kugawanywa katika namba ndogo umetolewa katika Yohana 21. Hapo Biblia inaandika kuhusu kuvuliwa kwa samaki 153. Jarife halikuvunjika. Samaki wote waliletwa salama katika nchi kavu, ambayo inawakilisha mbinguni, pasipo kutumia chombo au mashua, ambayo inawakilisha kanisa la mahali pamoja. Kiroho, hawa samaki wanawakilisha waamini wa kweli wote, watu walioteuliwa, ambao wataokolewa kutoka jehanum, ambayo inawakilishwa na bahari, baada ya nyakati za kanisa kumalizika. Namba 153 inagawanyika, ambapo tunaona kwa namba 3 x 3 x 17 = 153. Kiroho, namba zinamaanisha kwamba namba 153 inaelezea kusudi la Mungu (3) kuwapeleka mbinguni (17) wale wote ambao Mungu amewaokoa kutoka katika ghadhabu ya Mungu. Kwa hiyo, namba 153 inatusaidia kuona ukweli wa kiroho ambao umefichika katika hili tukio la kihistoria.

5. Wakati fulani Biblia inaita usikivu katika namba ambayo inatabiri tukio linalokuja. Kwa mfano, katika Danieli 12:12, Mungu anaongea juu ya mtu mwenye heri ambaye anangojea na kufikilia siku 1,335. Tunagundua kuwa hii inatabiri ujio wa Yesu, ambaye kazi yake ya upatanisho wa kiroho kwa ajili ya dunia hii ilianza Septemba 26, mwaka 29 B.K., wakati ambapo alitangazwa rasmi kama Mwana-kondoo wa Mungu. Iliendelea mpaka Mei 22, mwaka 33 B.K., siku ya Pentekoste wakati Roho Mtakatifu alipomwagwa na nyakati za kanisa kuanza rasmi. Wakati kati ya haya matukio mawili ulikuwa siku 1,335 kamili, kama Danieli 12:12 ilivyokuwa imetabiri.

6. Lazima ieleweke wazi kwamba ufahamu halisi wa ukweli wo wote wa Biblia unaweza tu kuja wakati Roho Mtakatifu anapoamua kwamba ni wakati wetu kufahamu ukweli huo. Lazima Mungu afungue mioyo na macho yetu ya kiroho kabla ukweli wo wote haujaweza kufahamika. Kwa hiyo, maombi kwa ajili ya huku kuona kiroho lazima yawe maombi ya kudumu kwa mtu ye yote anayetafuta ukweli wo wote wa Biblia. Hii pia inahusika moja kwa moja katika ufahamu wa mpangilio wa muda na hali ya matukio ya mwisho wa historia ya ulimwengu huu.

7. Katika Wakolosai 2:16 na 17, Mungu anatuarifu kwamba utaratibu rasmi wa siku za sikukuu ni vivuli vya mambo yanayokuja. Hii mistari inatangaza:

> **Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo.**

Kwa hiyo, tunaweza kutegemea na kutambua kwamba kila tukio muhimu katika kufunuliwa kwa mpango wa Injili ya Mungu kunatokea katika tarehe ya utaratibu rasmi wa siku ya sikukuu. Kwa mfano, Kristo alisulubiwa katika siku ambayo Pasaka ilikuwa iadhimishwe. Siku ya Pentekoste ilikuwa siku ambayo Roho Mtakatifu alimwagwa mwanzoni mwa nyakati za

kanisa. Tutatambua kwamba hii kanuni inaendelea moja kwa moja mpaka katika siku ya mwisho wa kuwepo kwa dunia, ambayo inakuja katika siku inayofungamanisha siku ya mwisho ya sikukuu ya mahema.

Katika uchunguzi wetu wa Biblia, kama tutatunza hizi kanuni saba akilini mwetu, tutakuwa tumesaidika sana katika juhudi zetu za kujifunza ukweli kutoka kwenye Biblia.

Kwa sababu ya umuhimu wa wazo la 7, ambalo linaongelea uhusiano wa tarehe za sherehe za Ki-Biblia na umuhimu wa matukio katika kufunuliwa kwa ratiba ya Mungu ya matukio ya historia, ingekuwa vyema kuendelea kusisitiza jambo hili. Katika kufanya hivyo, pia tutaona usahihi mkubwa ambao mara kwa mara umekuwapo katikati ya haya matukio ya kihistoria. Baadaye tutatambua kwamba usahihi huu unaendelea mpaka mwisho kabisa wa kuwepo kwa ulimwengu.

Umuhimu wa Mahusiano ya Wakati Umeungamanishwa katika Sikukuu za Utaratibu wa Ibada

Kama tulivyoona mapema, matukio mengi muhimu katika kufunuliwa kwa wakati yalikuwa yameshikamana kwa usahihi kabisa katika utaratibu rasmi wa siku za sikukuu ambazo zilipaswa kuadhimishwa na Israeli ya Agano la Kale. Kalenda ya sherehe za Biblia ilikuwa inaongozwa na kujiri kwa wakati kutoka katika mwezi mchanga mmoja kwenda mwingine, ambako kulifanya mwezi wa Ki-Biblia ama huwe siku 29 au 30. Kwa kuchunguza kwa makini habari ya wakati katika Biblia, tunajifunza kwamba mwezi wa kwanza wa kila mwaka ulianza karibu sana na majira ya kuchipua, lakini siyo mapema zaidi ya siku 14 kabla ya majira ya kuchipua, ambayo ni tarehe 21 Machi au tarehe 22 Machi.

Kama tulivyoona, Mungu alianzisha sherehe kadhaa za sikukuu muhimu sana ambazo zilihusisha vipengele muhimu vya mpango wa wokovu wa Mungu. Zilikuwa **“vivuli vya mambo yanayokuja.”** Hizi sherehe muhimu za sikukuu ni kama zifuatavyo.

1. Pasaka, siku ya 14 ya mwezi wa kwanza.
2. Pentekoste, pia iliitwa sikukuu ya mavuno, siku 50 baada ya Sabato ya siku ya saba ambayo ilikuwa sawia na siku ya Pasaka au ilikuwa siku ya kwanza ya Sabato baada ya Pasaka.
3. Siku ya kwanza ya mwezi wa saba ilikuwa siku ya sikukuu maalumu ambayo wanateolojia wanaiita sikukuu ya tarumbeta. Kwa usahihi zaidi, ingeitwa sikukuu ya yubile. Tarumbeta ambazo zilipigwa katika siku ile hazikuwa tarumbeta za fedha za Ki-Biblia. Kwa wakati ule, iliyopigwa ilikuwa *“shophar,”* baragumu (pembe ya kondoo dume). Wakati Biblia

inapotafsiriwa kwa usahihi, inaizungumzia kama siku ya tarumbeta (Hesabu 29:1) au ukumbusho wa kupiga baragumu (Mambo ya Walawi 23:24).

4. Kila mwaka wa hamsini ulikuwa mwaka wa yubile, ambapo ilisisitiza kwamba Injili (uhuru) ilipaswa kutangazwa katika ulimwengu wote. Miaka ya yubile ilianza katika mwaka 1407 K.K., wakati Israeli walipoingia nchi ya Kanaani na ilitakiwa kuadhimishwa kwa vipindi vya miaka 50 baada ya hapo (Mambo ya Walawi 25:8-13). Kwa hiyo, mwaka wa 7 K.K., mwaka ambao Kristo alizaliwa, ulikuwa mwaka wa yubile. Na mwaka 1994 B.K., ambao ulikuja miaka 2,000 baada ya mwaka wa 7 K.K., pia ulikuwa mwaka wa yubile.

5. Siku ya kumi ya mwezi wa saba iliitwa siku ya upatanisho. Hiyo pia iliitwa siku ya yubile (Mambo ya Walawi 25:9), na ilikuwa ikiashiria tukio kubwa la Yesu kutoa upatanisho kwa ajili ya dhambi za wale wote aliokuwa amekuja kuwaokoa.

6. Siku ya 15 mpaka siku ya 22 ya mwezi wa saba ilikuwa sikukuuu ya mahema, ambayo ilikuwa wakati mmoja na sikukuu ya kukusanya.

Zaidi sana, mpangilio wa kila siku za sikukuu hizi unahusiana na matukio muhimu sana katika kufunuliwa kwa mpango wa wokovu wa Mungu. Wakati tunapolinganisha habari yote ya Biblia ambayo inatusaidia kukuza ratiba ya matukio ya historia moja kwa moja mpaka mwisho wa wakati, tunatambua yafuatayo:

1. Ushahidi mkubwa katika Biblia unaashiria ukweli kwamba, katika uwezekano wote, Yesu, ambaye ndiye asili kabisa ya yubile, alizaliwa mnano Oktoba 2, katika mwaka wa 7 K.K. Mwaka wa 7 K.K., ni mwaka wa yubile. Oktoba 2, katika mwaka wa 7 K.K., ilikuwa siku ya upatanisho ambapo kwayo *"shofar"* (pembe ya kondoo dume au 'baragumu') ya yubile ilitakiwa kupigwa. Kwa hiyo, kwa pamoja, siku ya upatanisho na mwaka wa 7 K.K., vilihusiana na yubile. Kumbuka, yubile ililenga katika ukweli kwamba Injili ilitakiwa kutangazwa katika ulimwengu wote. Na Yesu alikuja katika dunia hii kufanya maandalizi yote ili kwamba Injili iweze kutangazwa katika ulimwengu wote. Kwa hiyo, tunaona uhusiano wa ajabu wa mpangilio wa kuzaliwa kwa Yesu, ambaye ndiye asili kabisa ya yubile, katika siku na mwaka ambao ulikuwa umelenga katika yubile.

2. Hatua muhimu inayofuata katika mpango wa wokovu wa Mungu ilikuwa siku Yesu alipoanza rasmi kazi yake kama Masiha. Ilikuwa siku alipotangazwa ulimwenguni kama Mwana-kondoo wa Mungu ambaye alikuwa amekuja kuchukua dhambi za ulimwengu. Kulingana na kalenda yetu ya siku hizi, ilikuwa Septemba 26, mwaka 29 B.K. Kwa mujibu wa kalenda ya Ki-Biblia, ilikuwa siku ya kwanza ya mwezi wa saba, ambayo ni tarehe ya sikukuu ya yubile (kwa makosa wanateolojia waliita sikukuu ya tarumbeta). Kwa hakika tunaweza kuona kufanana kwa tangazo la kuanza rasmi kwa huduma ya Yesu, yubile yetu, wakati mmoja na sikukuu ya yubile.

3. Yesu, kama Mwana-kondoo wa sadaka wa Mungu, kwa maana iliyo wazi alibeba adhabu, kama ilivyodaiwa na sheria ya Mungu, katika njia ambayo ilikuwa sawasawa na adhabu ambayo ingetolewa kwa wale aliokuwa amekuja kuwaokoa, wakati alipotoa malipo kwa ajili ya dhambi zao. Hii adhabu kubwa ilianza Alhamisi jioni katika Bustani ya Gethsemane na kuendelea mpaka Ijumaa jioni kabla tu ya machweo. Hili tukio la kustaajabisha lilitokea kwa usahihi katika wakati ule ule ambao Biblia iliagiza kwamba sikukuu ya Pasaka ilikuwa iadhimishwe. Hiyo Ijumaa, kwa mujibu wa kalenda ya Ki-Biblia, ilikuwa siku ya kumi na nne ya mwezi wa kwanza. Kwa mujibu wa kalenda yetu ya siku hizi, ilikuwa Aprili 1, mwaka 33 B.K.

4. Katika mwaka 33 B.K., kalenda ya Ki-Biblia ilidai maadhimisho ya sikukuu ya Pentekoste katika siku ya Jumapili, Mei 22, kwa mujibu wa kalenda yetu ya siku hizi. Hii ilikuwa siku ambayo mavuno ya mwanzo yalitakiwa kuletwa. Katika siku hiyo hiyo, Mei 22,

mwaka 33 B.K., Roho Mtakatifu alimwagwa na mavuno ya mwanzo ya waamini wa kweli katika nyakati za kanisa yaliletwa katika ufalme wa Mungu. Kumbuka, katika Matendo 2:41, tunasoma kwamba karibu watu 3,000 waliokolewa katika siku ile.

5. Kila siku ya Pentekoste katika kipindi chote cha nyakati za kanisa, ambayo iliendelea kutoka mwaka 33 B.K., mpaka mwaka 1988, ilisisitiza kwamba mavuno yalitakiwa kuendelea kuletwa. Kwa hiyo, kipindi cha nyakati za kanisa kingeisha siku kabla ya Pentekoste katika mwaka 1988. Hii ilikuwa Mei 21, 1988. Kwa hiyo, kipindi cha nyakati za kanisa kiliendelea kwa miaka kamili 1,955.

6. Wakati tunapoendeleza uchunguzi huu, tutajifunza kwamba nyakati za kanisa zilifika mwisho mnamo Mei 21, 1988 (B.K.). Hii tarehe ilitokea pamoja na wakati ambapo Mungu alianza kuandaa makanisa na ulimwengu kwa ajili ya kile Biblia inachokiita "dhiki kuu." Pia tutajifunza kwamba katika siku 2,300 za kwanza za hii dhiki ya siku 8,400, karibu hakuna mtu aliyeweza kupata kuokolewa.

7. Lakini baadaye, kama tutakavyoona katika uchunguzi huu, siku 2,300 baada ya mwanzo wa dhiki kuu, mpango mkubwa wa mwisho wa wokovu wa Mungu ulianza. Hiyo siku ya historia ilikuwa Septemba 7, mwaka 1994 (B.K.). Ilikuwa katika siku hiyo, ambapo Mungu kwa mara nyingine alimmwaga Roho Wake Mtakatifu, kwa hiyo, kwa miaka 17 iliyofuata, mkutano mkubwa sana wa watu ungeokolewa kila mahali ulimwenguni.[5] Kwa hakika, hakuna mtu aliyetambua tendo la Mungu lenye kustaajabisha wakati lilipotokea. Lakini Biblia inatuhakikishia kwamba lilitokea. Hiyo Septemba 7, kwa mujibu wa kalenda ya Ki-Biblia, ilikuwa siku ya kwanza ya mwezi wa saba, wakati ambapo sikukuu ya yubile (kumbuka, kimakosa, imekuwa ikiitwa sikukuu ya matarumbeta), ilitakiwa kuadhimishwa. Huo mwaka 1994, wakati hili tukio kubwa lilipotokea, ulikuwa mwaka wa yubile, kama tu mwaka wa 7 K.K., wakati Yesu alipozaliwa, ulikuwa mwaka wa yubile. Kwa mara nyingine tunaona uhusiano wa kustaajabisha wa mpangilio wa kufunuliwa kwa mpango wa wovoku wa Mungu pamoja na mpangilio wa utaratibu wa siku za sikukuu.

Usahihi wa Matukio Muhimu ya Wokovu

Kwa kuchunguza Biblia kwa makini tunajifunza kwamba kufunuliwa kwa matukio muhimu katika mpango wa wokovu wa Mungu kwa ajili ya ulimwengu siyo kwa kubahatisha au kuzungukazunguka hata kidogo. Kila tukio lilifuata utaratibu wa wakati uliopangwa kwa makini

---

[5] Katika Ezekieli 39:29, tunasoma, "**Wala sitawaficha uso wangu tena; kwa maana nimemwaga roho yangu juu ya nyumba ya Israeli, asema Bwana MUNGU.**" Kifungu cha maneno, "**Wala sitawaficha uso wangu tena"** kinahusiana na mpango wa mwisho wa wokovu wa Mungu, ambao unakuja katika kipindi cha sehemu ya mwisho wa dhiki kuu. Tunajua hii kuwa ni kweli kwa sababu mpango wa wokovu wa Mungu, katika kipindi cha miaka 1,480 ambayo Israeli iliwakilisha ufalme wa Mungu, na katika kipindi cha miaka 1,955 ya nyakati za kanisa, wakati ambapo makanisa yote yaliwakilisha ufalme wa Mungu, vipindi vyote viliisha kwa Mungu kugeuka kutoka kwao. Ni katika tu kipindi cha makusanyo ya mwisho, katika kipindi cha sehemu ya mwisho ya dhiki kuu, ambapo Mungu hatoficha uso wake tena kutoka kwao. Pia angalia Yoeli 2:28.32, ambapo Mungu anaongea juu ya kummwaga Roho Mtakatifu. Hii mistari imenukuliwa katika Matendo 2:17-21. Katika Yoeli 2, msisitizo upo katika kumwagwa kwa Roho Mtakatifu katika kipindi cha dhiki kuu. Katika Matendo 2, msisitizo wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu upo katika siku ya Pentekoste katika mwaka 33 B.K., na katika kipindi cha dhiki kuu.

sana ambao umefunuliwa katika kitabu cha sheria ya Mungu, Biblia. Ifuatayo ni mifano kadhaa ya utaratibu huu.

1. Israeli walikuwa katika nchi ya Misri kwa miaka 430 katika siku ile ile (Kutoka 12:40-41. Miaka ilikuwa 1877 K.K. mpaka 1447 K.K.
2. Wakati Israeli walipoondoka Misri katika mwaka 1447 K.K., ilikuwa tu, katika siku ile ile, miaka 40 baadaye ambapo walifika katika Mto Yordani, ambao mwishowe walivuka kwenda katika nchi ya Kanaani.
3. Kama ilivyotabiriwa katika Danieli 12:12, ilikuwa siku halisi 1,335, kwa pamoja, ambapo kazi ya Kristo kama Masiha ilijiri. Alianza rasmi kazi yake mnamo Septemba 26, mwaka 29 B.K., wakati alipotangazwa kama Mwana-kondoo wa Mungu (Yohana 1:29). Siku kamili 1,335 baadaye, kwa pamoja, katika Mei 22, mwaka 33 B.K., Roho Mtakatifu alimwagwa na nyakati za kanisa zikaanza rasmi.
4. Kipindi cha kanisa kilifuata katika siku ile ile, miaka 1955 kamili, kwa sababu kilianza katika siku ya Pentekoste, Mei 22, mwaka 33 B.K., na kufika mwisho siku kabla ya Pentekoste, Mei 21, mwaka 1988 (B.K.).
5. Katika mwaka ule ule, kulikuwa na miaka 13,000 kamili kutoka uumbaji, katika mwaka 11,013 K.K., mpaka kufika mwisho wa nyakati za kanisa, ambao pia ulikuwa mwanzo wa kazi ya Mungu ya mwisho ya wokovu na hukumu. Tutajifunza kwamba hii ilianza katika mwaka 1988 B.K.
6. Kuna miaka 7,000 kamili kutoka gharika ya siku za Nuhu, ambayo iliharibu kila kitu juu ya dunia katika mwaka 4990 K.K., mpaka mwaka 2011 B.K., ambapo tutajifunza kuwa ni mwaka ambao Mungu ataangamiza huu ulimwengu wa sasa hivi, na kuumba tena kama mbingu mpya na dunia mpya.
7. Hata kama ilivyotabiriwa katika Danieli 8:14, tutajifunza kwamba kulikuwapo na siku 2,300 kamili kutoka mwanzo wa dhiki kuu, ambazo zilitokea pamoja na mwisho wa nyakati za kanisa mnamo Mei 21, 1988, mpaka kumwagwa kwa Roho Mtakatifu. Huku kumwagwa kwa Roho Mtakatifu, ambako kulitokea Septemba 7, 1994, ni tarehe ya kuanza kwa miaka 17 ya mwisho wa mavuno makubwa ya mkutano mkubwa sana wa watu ambao wamekuwa waamini wa kweli.

Hivi ni baadhi ya vipindi halisi vya wakati ambavyo vinatuonyesha kwamba kufunuliwa kwa Injili ulimwenguni, Mungu alikuwa ameishakupanga kabla.

Mungu Alitumia Hekalu Kueleza Ukweli wa Kiroho kwa Mifano

Lazima tukumbuke kwamba wakati mwingine Biblia hutoa tukio la kihistoria ili kuonyesha ghadhabu ya Mungu pamoja na huruma na upendo wa Mungu. Kwa mfano, Biblia inaeleza hukumu ya Mungu yenye kutisha juu ya ulimwengu wa siku za Nuhu. Alitumia maji ya gharika kuwaangamiza wanadamu. Lakini, katika 1 Petro 3:20, wakati akiongea juu ya gharika hii, Mungu anaonyesha kwamba **“watu wanane, waliokoka kwa maji.”** Kadhalika, Israeli walivuka Bahari ya Shamu wakiwa salama ili kuonyesha wokovu. Walakini, jeshi la Wamisri liliangamizwa katika Bahari ya Shamu ili kuonyesha hukumu ya Mungu juu ya watu waovu. Kwa hiyo, katika mifano hii, Mungu anaonyesha ghadhabu na huruma zake kupitia tukio moja.

Katika njia hiyo hiyo, Mungu alitumia ujenzi mzuri wa hekalu kupitia Sulemani ili kuonyesha hukumu ya Mungu na pia kuonyesha wokovu wa Mungu. Hili hekalu, kama hema la kukutania huko Shilo, lilielezea kwa picha ujenzi wa ufalme wa Mungu katika kipindi cha nyakati za kanisa. Lakini, mwishowe, Mungu kwa pamoja aliharibu hekalu uko Shilo na pia hekalu la Sulemani katika mji wa Yerusalemu kwa sababu ya uovu wa Israeli na Yuda. Kadhalika, katika wakati wetu, Mungu ameleta hukumu yake juu ya makanisa ya kizazi chetu. Hakuna hata kanisa moja kati ya makansia ya leo ambalo lipo ndani ya mpango wa wokovu wa Mungu. Hekalu, ambalo liliwakilisha kipindi chote cha nyakati za kanisa, halipo tena. Hakuna jiwe ambalo limesalia juu ya jiwe lingine. (Mathayo 24:1-3).

Lakini pia Mungu anatumia hekalu la Sulemani kuwakilisha na kuonyesha mpango wa ajabu wa wokovu wa Mungu ambao unajiri siku hizi. Anafanya hivi ndani ya Biblia wakati anapoelezea kuwekwa wakfu wa hekalu. Matukio yote yaliyotokea kuhusiana na huku kuwekwa wakfi yalijiri katika mwezi wa saba wa kalenda ya Biblia (1 Wafalme 8:2). Biblia huzungumzia mwezi wa saba kama mwisho wa mwaka (Kutoka 23:16, 34:22). Ni siku hizi ambapo tupo mwishoni mwa mwaka,[6] kwa kiasi ambacho historia ya ulimwengu inahusika. Kwa hiyo lazima tufahamu kwamba matukio yote yaliyohusishwa katika kuwekwa wakfu kwa hekalu la Sulemani, yalikuwa yanaashiria au kuwakilisha matukio ya Injili ambayo yanatokea siku hizi, wakati wa mavuno ya mwisho.

Habari ya Kuwekwa Wakfu kwa Hekalu Inatoa Habari Muhimu ya Wakati

Katika habari ya kuwekwa wakfu kwa hekalu la Sulemani, Mungu alitumia njia ya kuvutia sana kuonyesha kwamba mwisho wa ulimwengu ni siku moja baadaye zaidi ya vile ambavyo tungeitarajia. Kwa kufanya hivyo, Mungu pia anatuonyesha usahihi wa mpangilio wa muda wa mwisho wa ulimwengu. Ili kupata habari hii, lazima kwanza tuangalie jinsi Mungu anavyotumia maneno “siku ya mwisho.”

Wakati tunapochunguza maneno, “siku ya mwisho” tunaona kwamba yameandikwa katika sehemu nane tu ndani ya Biblia. Sehemu nne kati ya hizi yameandikwa katika Yohana 6, ambapo Mungu anaongea juu ya kuwapa waamini wa kweli wote miili yao iliyofufuliwa katika siku ya mwisho (Yohana 6:39,40,44,54). Maneno, “siku ya mwisho” pia yanapatikana katika Yohana 11:24. Hapo tunasoma kwamba Martha, akisimama pembeni mwa kaburi la ndugu yake Lazaro aliyekuwa amekufa, ananena, chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu:

…Najua ya kuwa atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho.

---

[6] Ni muhimu kwamba Biblia inamwongelea Enoko kuwa alichukuliwa mbinguni, pasipo kufa, akiwa na umri wa miaka 365 (Mwanzo 5:23-24). Kwa hakika siyo bahati mbaya kwamba huu mfano wa kwanza wa unyakuo ulitokea kwa mwamini wa kweli katika umri ambao unalingana na mwaka mmoja (siku 365), wa historia ya dunia.

Maneno haya, pia yameandikwa katika Yohana 12:48, ambapo Kristo anatangaza:

Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hili nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho.

Mifano miwili iliyobaki ya Mungu kutumia maneno “siku ya mwisho” ina umuhimu sana kuhusiana na siku ya mwisho wa sikukuu ya mahema. Yameandikwa katika Yohana 7:37 na Nehemia 8:18.

Sikukuu ya mahema ilikuwa sawia na sikukuu ya kukusanya. Hizi sikukuu kwa hakika zinahusika na mwisho wa ulimwengu. Kwa hiyo, hatushangai kwamba Mungu anatumia maneno “siku ya mwisho” kuhusiana na sikukuu ya mahema. Hiyo ni kusema kwamba, siku ya mwisho ya sikukuu ya mahema inaweza kutuonyesha mpangilio wa muda wa siku ya mwisho wa mwisho wa ulimwengu.

Katika utaratibu wa kalenda ya Ki-Biblia, hizi sikukuu sawia, sikukuu ya mahema na sikukuuu ya kukusanya, zilitakiwa kuwa na urefu wa siku saba, kuanzia katika siku ya 15 ya mwezi wa saba. Siku iliyofuatia hizi siku saba, ambayo Biblia inaiita siku ya nane, pia nayo kwa pamoja iliitwa “kusanyiko takatifu” (Mambo ya Walawi 23:36) na “Sabato au siku ya kustarehe kabisa” (Mambo ya Walawi 23:39). Kwa hiyo, sikukuu ya mahema kwa hakika ilijumuisha siku nane ambazo zilianza katika siku ya 15 ya mwezi wa saba na kumalizika katika siku ya 22, na hii siku ya mwisho ilitakiwa kuadhimishwa kama Sabato.

Hata hivyo, lilikuwa kusudi la Mungu kutuonyesha kwamba wakati tunapofanya mbandiko wa hizi siku katika mwisho wa ulimwengu, siku ya nane inapaswa kuangaliwa kuwa siku mbili katika urefu, kwa hiyo siku ya nane pia ilijumuisha siku ya 23 ya mwezi wa saba wa Ki-Biblia.

Huu ukweli unaelezewa na Mungu katika taarifa ya Biblia kuhusiana na kuwekwa wakfu kwa hekalu la Sulemani, ambao unaweza kuonyeshwa kwa kuvutia ukihusiana na matukio yanayojiri mwishoni wa ulimwengu. Katika 2 Mambo ya Nyakati, Mungu anaelezea kuwekwa wakfu kwa hekalu la Sulemani. Tutaangalia kauli chache ambazo Mungu amezinena kuhusiana na kuweka wakfu. Hizo kauli ni kama ifuatavyo.

1. Wakati ulikuwa katika mwezi wa saba (2 Mambo ya Nyakati 7:10).
2. Kuweka wakfu madhabahu kulikuwa siku saba (2 Mambo ya Nyakati 7:9).
3. Kisha waliadhimisha sikukuu ya mahema (sikukuu ya Biblia) siku saba (2 Mambo ya Nyakati 7:8-9). Kwa hiyo siku 14 zilikuwa zimepita (1 Wafalme 8:65).
4. Sherehe ya siku ya saba ya sikukuu ya mahema ilifuatiwa na siku ya nane wakati walipoadhimisha kusanyiko makini (2 Mambo ya Nyakati 7:8-9).

Hii siku ya nane ingeadhimishwa kama siku ya Sabato (Mambo ya Walawi 23:39), ambapo hakuna kazi iliyopaswa kufanyika, na kusafiri kungekuwa na mipaka. Kulingana na Matendo 1:12, umbali kati ya Mlima wa Mizeituni na Yerusalemu, ambao ulikuwa chini ya nusu maili, ulikuwa urefu au umbali pekee walioruhusiwa kusafiri katika siku ya Sabato. Kwa mshangao, katika 1 Wafalme 8:66, tunasoma:

> **Hata siku ya nane akaagana na watu, nao wakamkaribia mfalme, wakaenda hemani kwao, wakifurahi na kuchangamka moyoni kwa wema wote BWANA aliomfanyia Daudi mtumishi wake, na Israeli watu wake.**

Siku ya Nane, Oktoba 21, 2011

Kama ambavyo tumeona, hii siku ya nane kwa kawaida ilikuwa siku ya 22 ya mwezi wa saba na ilitakiwa kuadhimishwa kama Sabato. Watu walikuja kutoka katika nchi yote ya Israeli (1 Wafalme 8:65). Wangewezaje kutegemewa kufanya kazi yote ya kuhama na kusafiri katika siku ambayo ilitakiwa kuadhimishwa kama Sabato? Mungu alitatua tatizo hili kwa kuonyesha kwamba siku ya nane ilikuwa iendelee kwa siku moja zaidi. Hiyo siku moja ya ziada ilikuwa siku ya 23 ya mwezi wa saba. Tunasoma hivi katika 2 Mambo ya Nyakati 7:10:

> **Akawaruhusu watu waende hemani kwao siku ya ishirini na tatu, ya mwezi wa saba, wakifurahi na kuchangamka mioyoni kwa wema wote BWANA aliomfanyia Daudi, na Sulemani, na Israeli watu wake.**

Tafadhali angalia lugha ya mstari huu inavyokaribia kufanana na ile ya 1 Wafalme 8:66 (iliyonukuliwa juu). Kumbuka, 1 Wafalme 8:66, mstari ulirejea kuzungumzia siku ya nane, ambayo ilikuwa siku ya 22 ya mwezi, lakini 2 Mambo ya Nyakati 7:10 unazungumzia siku ya 23 ya mwezi.

Huu ufunuo ni muhimu sana wakati tunapotambua kwamba kuwekwa wakfu kwa hekalu na maadhimisho ya sikukuu ya mahema (sikukuu ya Biblia), vinahusiana kwa ndani sana na kukamilika kwa mpango wa hukumu ya Mungu mwishoni mwa ulimwengu. Inamaanisha kwamba katika mwaka 2011 B.K., siku ya nane ya sikukuu ya vibanda (sikukuu ya Biblia) kwa hakika inatakiwa kuangaliwa siku mbili katika urefu. Wakati ambapo siku ya nane (siku ya 22 ya mwezi wa saba) ni Oktoba 20, kwa hakika inatakiwa kuadhimishwa kama walivyofanya katika 2 Mambo ya Nyati 7:10, katika siku ya 23 ya mwezi wa saba, ambayo ni Oktoba 21, 2011. Kwa

hiyo, lazima tutambue kwamba Oktoba 21, 2011 itakuwa siku ya mwisho wa kuwepo kwa dunia hii.

Mtazamo Mwingine katika Sikukuu ya Mahema

Wakati tulipochunguza kuwekwa wakfu kwa hekalu la Sulemani, tuliona kwamba sikukuu ya mahema ilikuwa sehemu muhimu ya shughuli za kuweka wakfu. Pia tulijifunza kwamba inatusaidia kuelewa mpangilio wa muda wa mwisho wa ulimwengu. Lakini kwa nini iliitwa sikukuu ya mahema?

Tutagundua kwamba neno la Kiebrania ambalo limetafsiriwa kama “hema” kuhusiana na hii sikukuu ni neno la Kiebrania ambalo kwa kawaida sana hutafsiriwa kama “kibanda.” Zaidi, tutagundua kwamba neno “kibanda” linahusisha wingu na moto vilivyofunika hema katika miaka yote 40 ambayo Israeli walikuwa jangwani, katika safari yao kutoka Misri kwenda katika nchi ya Kanaani. Pia, tutatambua kwamba wingu na moto viliwakilisha amri za Mungu, kwa hiyo kutengeneza kibanda kunawakilisha amri za Mungu. Kwa hiyo, sikukuu ya mahema kwa kawaida ni sikukuu ya sheria ya Mungu au sikukuu ya Biblia. Sikukuu ya mahema (sikukuu ya Biblia), inasisitiza utukufu wa Mungu pale unavyoendelezwa na utukufu wa kitabu cha Mungu, Biblia.

Neno la Kiebrania kwa neno hema ambalo Mungu aliliweka katika maneno “sikukuu ya mahema” ni neno *“sukkah,”* ambalo pia limetafsiriwa “kibanda.” Kifungu cha Biblia ambacho kinatusaidia kuelewa hili neno ni Isaya 4:5-6. Hapo tunasoma:

> **Tena juu ya makao yote ya mlima Sayuni, na juu ya makusanyiko yake, BWANA ataumba wingu na moshi wakati wa mchana, na mwangaza wa miali ya moto wakati wa usiku; kwa maana juu ya utukufu wote itatandazwa sitara. Kisha kutakuwa na hema kuwa uvuli wakati wa mchana kwa sababu ya hari, na kuwa mahali pa kukimbilia na kujificha wakati wa tufani na mvua.**

Neno la Kiebrania lililotafsiriwa kama “sitara” katika mstari huu lingetafsiriwa vizuri kama “kinga.” Maneno yaliyotafsiriwa kama “**kutakuwa na hema”** yangetafsiriwa vizuri kama “**kutakuwa na kibanda.”** Kwa hiyo, hii mistari ingetafsiriwa vizuri kama hivi:

> **Tena juu ya makao yote ya mlima Sayuni, na juu ya makusanyiko yake, BWANA ataumba wingu na moshi wakati wa mchana, na mwangaza wa miali ya moto wakati wa usiku; kwa maana juu ya utukufu wote itatandazwa kinga. Kisha**

kutakuwa na kibanda kuwa uvuli wakati wa mchana kwa sababu ya hari, na kuwa mahali pa kukimbilia na kujificha wakati wa tufani na mvua.

Hii mistari inafundisha yafuatayo.

1. **“juu ya makao yote ya mlima Sayuni.”** Hii inahusu sura nzima ya ufalme wa Mungu, ufalme ambao tumepata kuwa raia wake wakati tulipookolewa.
2. “**juu ya makusanyiko yake”** Hili ni neno la umoja ambalo linaongelea kusanyiko moja kubwa la milele ambalo linajumuisha wale wote ambao wamepata kuokolewa.
3. **“wingu na moshi wakati wa mchana, na mwangaza wa miali ya moto wakati wa usiku”** Hii inahusu sheria ya Mungu, Biblia, ambayo hutoa mwongozo wa kiroho kwa wanadamu.
4. **“juu ya utukufu wote itatandazwa kinga”** Hii inaongelea ufalme wa Mungu kwamba kuna wingu wakati wa mchana na moto wakati wa usiku kama kinga.
5. **“kisha kutakuwa na hema [kibanda] kuwa uvuli wakati wa mchana kwa sababu ya hari, na kuwa mahali pa [kinga] kukimbilia na kujificha wakati wa tufani na mvua.”** Wingu na moto, hiyo ni kusema kwamba, neno la Mungu ni kibanda ambacho kinakinga na kutoa mahali pa kukimbilia na kujificha kutoka kwenye ghadhabu ya Mungu, tufani na mvua.

Mapema tulijifunza kwamba wingu na nguzo ya moto vinahusiana na Neno la Mungu. Tunaweza kuona hivi kwa sababu tunaona kwamba Biblia ina mambo mengi ya kusema juu ya wingu na nguzo ya moto kutoa mwongozo kwa Israeli katika miaka yao 40 jangwani. Kwa mfano, tunasoma katika Hesabu 9:21-23:

Na pengine lile wingu lilikaa tangu jioni hata asubuhi; na lile wingu lilipoinuliwa asubuhi walisafiri, au kama likikaa usiku na mchana pia, lilipoinuliwa lile wingu, ndipo waliposafiri. Ikiwa lile wingu lilikawia, likikaa juu ya maskani siku mbili, au mwezi, au mwaka, wana wa Israeli walikaa katika kambi yao, wasisafiri; bali lilipoinuliwa walisafiri. Kwa amri ya BWANA walipiga kambi yao, na kwa amri ya BWANA walisafiri; wakayalinda malinzi ya BWANA, kwa mkono wa Musa.

Katika Hesabu 9:15-23, wingu wakati wa mchana na moto wakati wa usiku, kwa uwazi sana Mungu anavihusisha na amri za Mungu. Na kwa hakika, amri za Mungu ni Biblia.

Kwa hakika lazima tuelewe kwamba, kama kamwe sisi hatutaokolewa, sheria ya Mungu itaifanya laana ya ghadhabu yake kushuka juu yetu. Lakini, kama sisi ni miongoni mwa wateule wa Mungu (na tunaweza kujua sisi ni wateule wake, kama tumepokea roho zetu mpya zilizofufuliwa), basi hatupo chini ya adhabu ya laana ya milele kwa ajili ya dhambi zetu. Hiyo ni kusema kwamba, sheria haiwezi tena kutuhukumu. Badala yake, sheria ni uhakikisho tunaopewa na Mungu kwamba milele tupo salama katika Kristo. Tumefichwa na sheria ya Mungu kutoka

katika ghadhabu ya Mungu. Na sheria ya Mungu, Biblia, inatupa mwongozo kamili jinsi kwa ujumla tunavyotakiwa kuishi katika utukufu wa Mungu.

Kwa hiyo, tumejifunza kwamba sikukuu ya vibanda kwa ujumla imelenga katika Biblia ambapo kwayo Mungu anafunua utukufu wake mkubwa sana. Hivyo, ingekuwa sahihi zaidi kuzungumzia “sikukuu ya vibanda” kama “sikukuu ya Biblia.” Sikukuu ya Biblia iliadhimishwa katika siku zile zile ambazo sikukuu ya kukusanya ilikuwa iadhimishwe. Sikukuu ya kukusanya ilikuja katika wakati ule ule ambapo yalitokea mavuno ya mwisho wa mwaka. Kiroho, hii inaashiria ukweli kwamba Biblia imetukuzwa na sikukuu za Biblia. Huu msisitizo juu ya asili ya utukufu wa Biblia umedhihirishwa zaidi kwa sababu Mungu analeta mavuno makubwa ya watu ambao wanapata kuokolewa kabla tu ya mwisho wa ulimwengu.

Haya mavuno ya mwisho yametabiriwa katika Warumi 9:28. Hapo tunasoma:

> **Kwa maana Bwana atalitekeleza neno [*Kigiriki, logos]* lake juu ya nchi, akilimaliza na kulikata.**

Neno la Kigiriki *“logos”* kwa kawaida hutafsiriwa kama “neno.” Kwa hiyo, huu mstari unazungumzia kipindi kifupi cha wakati huu wa sasa hivi, ambapo tutajifunza kutoka kwenye Biblia kwamba ni miaka 17 ya mwisho wa historia ya ulimwengu. Kiini katika umuhimu wa hii miaka 17 ni Neno (*logos)* tukufu la Mungu ambapo kwayo sasa hivi Mungu anaokoa mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu (Ufunuo 7:9). Huu mwisho wa uenezaji wa Injili kwa ulimwengu ambao unatokea hivi sasa hautayumba wala kusita. Utaendelea vikwazo au dosari mpaka kufikia ukamilifu wake wa milele, ambapo kwa muda mfupi sana Kristo anarudi na kunyakua waamini wa kweli wote, watelue wote katika ulimwengu wote ili wawe pamoja naye milele katika mbingu mpya na dunia mpya.

Sura ya 4.

Tunaanza Uchunguzi Wetu kwa Ajili ya Ratiba ya Mwisho

Sasa tutaelezea misingi ya kweli ambazo tunajifunza kutoka kwenye Biblia ambazo zinatupeleka katika ufahamu halisi wa ratiba ya matukio ya mwisho wa historia. Katika miaka 2,000 ya mwisho, kipindi ambacho Biblia nzima imekuwapo, waamini wa kweli wanaomcha Mungu wamechunguza Biblia kwa bidii katika kujaribu kutambua ufunuo unaokuja wa historia ya dunia hii. Wote walifahamu ukweli mmoja, ambao ni kusema kwamba, kungekuja wakati ambapo historia ya ulimwengu huu ingekuja kufika mwisho. Ingetokea pamoja na kurudi kwa Kristo kama hakimu wa dunia mwenye haki, na kunyakuliwa kwa waamini wa kweli wote kwenda katika mbingu mpya na dunia mpya, ambapo milele watatawala pamoja na Kristo.

Lakini, kabla ya wakati huu kutokea, kungekuwapo na kipindi cha dhiki kubwa ya aina fulani. Kwa kawaida, hii ilieleweka vibaya kuwa wakati wa mateso makubwa ya kimwili kwa wanaomwamini Kristo. Kwa hakika, ni wakati tu ambao unaweza kueleweka kiroho.

Sura ya Biblia kama vile Mathayo 24 na Marko 13 kimsingi zilichunguzwa kwa uangalifu mkubwa kwa sababu zilionekana kusisitiza dhiki inayokuja kabla tu ya kurudi kwa Kristo. Ni kweli kwamba ndani ya hizi sura mbili, Mungu anatupa dokezo zuri ili kutusaidia kuanza kujenga msingi wa Ki-Biblia ambao unaunganisha mambo ya zamani hadi kufikia mwisho wa historia. Hilo dokezo lipo katika Marko 13:28, ambapo Mungu anatangaza:

> **Kwa mtini jifunzeni mfano; tawi lake liishapo kuwa laini, na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno ni karibu.**

Mstari huu haukuweza kuanza kueleweka mpaka karibu miaka 60 iliyopita, mnamo Mei 14, 1948. Ulikuwa wakati ambao mtini Ki-Biblia, taifa la Israeli, kwa mara nyingine lilipata kuwa taifa lenye uwezo wa kujitegemea miongoni mwa mataifa ya ulimwengu. Huu karibu ulikuwa muujiza, kwa sababu kwa kipindi chote kutoka mwaka 70 B.K., wakati Israeli pamoja na mji wa Yerusalemu na hekalu vilipoangamizwa kabisa na Warumi, Israeli ilikuwa haijawa taifa la ulimwengu likiwa na nchi yake ya asili. Walakini, kwa muujiza, mnamo Mei 14, 1948, kwa mara nyingine lilikuwa taifa lenye nchi yake ya asili.

Kwa haraka sana Wakristo wengi kwa usahihi walihusisha hili tukio lenye kuvutia na unabii wa mtini wa Marko 13:28. Kwa usahihi waliona kwamba Mungu aliliwakilisha taifa la Israeli kama mtini, na kwamba mtini kuwa na majani kulihusisha Israeli kwa mara nyingine (kupata) kuwa taifa.*

---

*Israeli, kwa mfano, inafananishwa na mtini ambao Kristo aliulaani, hivyo kamwe haukuweza tena kuzaa matunda (Marko 11:12-21).

Kwa sababu mstari huu unasisitiza kwamba wakati mtini unapochanua majani, matukio yote yaliyoandikwa katika Marko 13 na Mathayo 24 yatatokea, lazima tutambue kwamba Mungu ametoa dokezo linaloonyesha dhahiri kwamba wakati wa mwisho wa ulimwengu umekaribia sana. Hii ni kwa sababu usomaji makini wa Mathayo 24 na Marko 13 unaonyesha haya matukio yakihusiana na wakati wa dhiki kuu (Mathayo 24:21), ambayo itafuatiwa na kurudi kwa Kristo (Mathayo 24:29-31).

Dokezo lingine ambalo Mungu anatupatia linapatikana katika Ufunuo 7:9-14. Hapo Mungu anazungumzia mkutano mkubwa sana ya watu, ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wanaotoka katika dhiki kuu. Zaidi, katika Luka 21:22, mstari ambao pia unazungumzia wakati wa dhiki kuu, Mungu anazungumzia hii dhiki kama wakati wa mapatilizo. Hukumu ya Mungu kwa watu waovu ni wakati wa mapatilizo. Katika kipindi cha dhiki kuu, Mungu ameanza kuwaandaa watu wa ulimwengu pamoja na makanisa kwa ajili ya ukamilisho wa hatua ya hukumu ya Mungu.

Mstari unaofuata ambao unatusaidia ni Mathayo 24:22, ambapo tunasoma:

> **Na kama siku hizi zisingalifupizwa, asingeokoka mtu ye yote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo.**

Inaonekana kwamba huu mstari unasema kuwa huu ni wakati wa dhiki kuu ambapo mapatilizo ya Mungu juu ya mwanadamu yataanza. Lakini, kwa sababu wengi wa wateule wa Mungu, wale waliokuwa wameteuliwa na Mungu ili wapate kuokolewa (Waefeso 1:3-6), bado hawajaokolewa, kipindi cha dhiki kuu kimefupizwa. Kwa maneno mengine, hiki kipindi cha dhiki kuu kinahusisha sana mpango wa hukumu ya Mungu, lakini kwa wakati huo huo kinahusiana na aina fulani ya wimbi kubwa katika shughuli za wokovu. Tunawezaje kuweka pamoja mawazo haya?

Tumejifunza kutoka katika uchunguzi wa kufunuliwa kwa matukio ya historia ya Biblia, na kutoka katika mafundisho ya Wakolosai 2:16-17, kwamba yanahusika katika utaratibu wa siku za sikukuu. Mwaka wa yubile, kwa mfano, unasisitiza kwamba uhuru (wokovu) unatakiwa kutangazwa ulimwenguni. Ukweli ni kwamba, ushahidi wote wa Ki-Biblia unaashiria uwezekano wa hali ya juu sana kwamba Yesu, ambaye ndiye asili kabisa ya yubile, alizaliwa katika mwaka wa yubile, mwaka 7 K.K., katika siku ya upatanisho, wakati ambao *shophar* (pembe ya kondoo dume) baragumu (Kiebrania *"teruah"*) ilipigwa (Mambo ya Walawi 25:9).[7]

Zaidi, tunajifunza kwamba Yesu alitangazwa rasmi kama Mwana-kondoo wa Mungu mnano Septemba 26, mwaka 29 B.K., ambapo Kibiblia ilikuwa Tishri 1 (Tishri ni mwezi wa saba), ambao pia unaitwa siku ya yubile (Hesabu 29:1). Kwa sababu Kristo, yubile, alikuwa amekuja na akatangazwa rasmi, hatua ilikuwa imewekwa ili kupeleka Injili katika ulimwengu

---

[7] Tafsiri ya Kiingereza katika baadhi ya vifungu ilitafsiri neno la Kiebrania "teruah" kama "tarumbeta." Lakini katika Mambo ya Walawi 25:9, kuhusiana na siku ya upatanisho, tunasoma kwamba neno hili hili "teruah" limetafsiriwa kiusahihi kama "baragumu." Kwa hiyo, maneno "siku ya kupiga tarumbeta," yangetafsiriwa vizuri kama "siku ya baragumu."

wote. Majuma saba baada ya Jumapili wakati Yesu alipofufuka, Roho Mtakatifu alimwagwa na kazi ya kuhubiri Injili kwa ulimwengu wote ilianza.

Ingeweza kuonekana kana kwamba kuna wimbi kubwa katika shughuli za wokovu, basi kwa njia fulani lingehusiana na mwaka wa yubile. Kwa hiyo, katika miaka iliyofuatia mwaka 1948, ni lini ambapo kungekuwapo na mwaka mwingine wa yubile? Kuna miaka 50 kamili kutoka mwaka mmoja wa yubile kwenda mwaka mwingine wa yubile. Kwa hakika, mwaka 1994 ni mwaka wa kwanza wa yubile baada ya mwaka 1948. Ni miaka 2,000 kamili baada ya yubile ya mwaka 7 K.K., wakati Kristo alipozaliwa, ambaye ndiye asili kabisa ya yubile.

Yubile kwa hakika inahusiana na mpango wa wokovu wa Mungu. Lakini Biblia inatuhakikishia kwamba huu mwaka wa yubile upo katikati ya kipindi cha dhiki kuu, ambacho ni kipindi cha maandalizi kwa ajili ya matukio ya mwisho ya hukumu ya Mungu. Inawezekanaje haya matukio sawia yasiyopatana yawe kwa wakati mmoja na yahusiane na mwaka 1994?

Unabii wa Danieli 8 unakuwa msaada sana. Katika Mathayo 24, ambapo tunajifunza juu ya hii dhiki kubwa, Mungu anatuongoza kutafuta habari zaidi katika Kitabu cha Danieli. Mathayo 24:15-16 inasema:

> **Basi hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu; lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika patakatifu (asomaye na afahamu), ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani;”**

Katika Danieli Sura ya 8, Mungu anazungumzia kipindi cha siku 2,300, ambapo katika kipindi hicho mfalme mwenye nguvu sana angetawala. Angeifanya sadaka ya kuteketezwa ya daima kuondolewa na kosa lifanyalo ukiwa kuchukua nafasi kiasi kwamba patakatifu na jeshi pangekanyagwa (Danieli 8:12-14). Kiroho, hii inamaanisha kwamba Injili ya kweli ingeondolewa na injili ya kishetani. Zaidi, kuhusiana na maono ya siku 2,300, Mungu anatangaza katika Danieli 8:17, “**maono haya ni ya wakati wa mwisho.”**

Tumeona kwamba mwaka 1994 ni mwaka wa yubile ambao unasisitiza kutangazwa kwa Injili ulimwenguni kote. Kwa hiyo, huo mwaka, ni mwisho wa kipindi cha siku 2,300 zilizozungumziwa katika Danieli 8, siku ambazo ndani yake dhiki kuu inatokea?

Kama hiyo iko hivyo, na siku 2,300 mapema kabla ya mwaka 1994 ilikuwa mwaka 1988, je huo unaweza kuwa mwaka ambapo dhiki kuu ilianza? Hiyo ingemaanisha kwamba katika kipindi hicho, kwa sehemu ya kwanza ya dhiki kuu, karibia hakuna mtu aliyeokolewa. Lakini pia ingemaanisha kwamba katika kipindi cha sehemu ya mwisho wa dhiki kuu, mkutano mkubwa sana wa watu ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu wangepata kuokolewa (Ufunuo 7:9-14).

Wakati tunapotafakari juu ya hili, lazima tufahamu kwamba katika Matendo 7:11 maneno “dhiki nyingi” yametumiwa katika kuhusisha mapito ya Yakobo na Israeli wote wakati walipoiacha nchi ya ahadi, nchi ya Kanaani, kwenda Misri ili kujiokoa na miaka saba ya njaa.

Tunajua kwamba hili lilikuwa pito la kutisha kwa Yakobo. Maneno “dhiki nyingi” ni maneno yale yale ya Kigiriki ambayo yametafsiriwa “dhiki kubwa” katika Mathayo 24:21.[8]

Zaidi sana, tunatambua kwamba Yakobo alikwenda Misri katika kipindi chake cha dhiki kubwa katika mwaka 1877 K.K. Mwaka ambao tunauchunguza kuhusiana na dhiki kubwa ya Mathayo 24:21 ni mwaka wa yubile 1994. Hii miaka, 1877 na 1994, inapishana miaka 3,870. 1,877+1,994-1 = 3,870. (Kwa kuwa hakuna mwaka sufuri, tunapoenda kutoka kalenda ya Agano la Kale kwenda Agano Jipya, mwaka mmoja lazima utolewe). Kwa kuvutia sana, 3,870 = 3 x 1,290.

Namba 1,290 inaonekana kuwa muhimu sana kwa sababu kuna wakati mwingine ambapo Israeli walishurutishwa kutoka kwenye nchi ya ahadi. Yerusalemu na hekalu viliharibiwa kabisa na Wababeli. Hii ilitokea katika mwaka 587 K.K., ambapo ilikuwa katika kipindi cha miaka 70 ya ghadhabu kuu ya Mungu juu ya taifa la Yuda. Hiki kipindi cha miaka 70 kilianza katika mwaka 609 K.K., na kuisha mwaka 539 K.K., wakati mji wa Babeli ulipoharibiwa na Wamedi na Waajemi. Tukio la kutisha, kuharibiwa kwa Yerusalemu na hekalu, lilitokea katika mwaka 587 K.K. Kwa ajabu na kwa uhakika zaidi, miaka mitatu tunayoichunguza (1877 K.K., 587 K.K., na 1994 B.K.,) inashikamanishwa pamoja na namba 1,290.

1877 K.K. - 587 K.K. = 1,290

587 K.K. mpaka 1994 B.K. -1 = miaka 2,580 = 2 x 1,290

1877 K.K. mpaka 1994 B.K. -1 = 3,870 = 3 x 1,290

Namba 1,290 imesisitiziwa ndani ya Biblia kuhusiana na shughuli za kiroho ambazo zinatukia katika moja ya kila mwaka mara tatu. Biblia inasisitiza hii nafasi ya namba 1,290 katika Danieli 12:11, ambapo tunasoma:

Na tangu wakati ule ambapo sadaka ya kuteketezwa ya daima itaondolewa, na hilo chukizo la uharibifu litakaposimamishwa, itapata siku elfu na mia mbili na tisini.

Lazima tukumbuke kwamba wakati mwingine, Mungu hutumia siku katika kuwakilisha mwaka. Kwa mfano, katika Hesabu 14:34, Mungu alionyesha kwamba Israeli wangebakia jangwani kwa miaka 40, kwa kufuatana na siku ambazo wapelelezi waliichunguza nchi ya Kanaani. Kwa hiyo, tunajua kwamba siku 1,290 za Danieli 12:11 zinaweza kufahamika kama

---

[8] Maneno “dhiki kubwa” yanapatikana mara nne tu katika Biblia. Yapo katika Mathayo 24:21 na Ufunuo 7:14, ambayo tayari tumeisha yachunguza, na pia, Matendo 7:11 na Ufunuo 2:22. Katika Luka 21:23, Mungu alichagua maneno ya Kigiri ambayo yametafsiriwa kama “shida nyingi” katika kuzungumzia kipindi hicho hicho.

miaka 1,290. Mungu kwa hakika anashikamanisha pamoja wakati wa kutisha ambapo Yakobo alitakiwa kuiacha nchi ya ahadi kwenda katika nchi ya Misri, na kufukuzwa kwa taifa la Yuda kutoka Yerusalemu, na katika jambo la kutisha ambalo lilitokea katika mwaka wa yubile 1994. Hilo jambo la kutisha lilikuwa ni nini?

Tunafahamu kwamba nchi ya Kanaani imetumiwa katika Biblia katika kuwakilisha ufalme wa Mungu. Yerusalemu na hekalu, pia kwa nje viliwakilisha ufalme wa Mungu. Kwa hiyo, kwa Yakobo na familia yake kuiacha nchi ya Kanaani, ilikuwa ni kama kuuacha ufalme wa Mungu. Pia, kuondolewa kutoka Yerusalemu, na kujua kwamba hekalu lilikuwa limeharibiwa, hiyo ilikuwa kama kufukuzwa kwenye ufalme wa Mungu. Lakini ni nini kilichowakilisha ufalme wa Mungu katika mwaka 1994? Tunafahamu kwamba katika kipindi chote cha nyakati za kanisa, makanisa yote ya mahali pamoja yaliwakilisha ufalme wa Mungu kwa sababu yalikuwa taasisi takatifu zilizokusudiwa na Mungu ili kuwakilisha huo ufalme kwa nje. Wao walikuwa watunzaji wa Biblia, na walikuwa na jukumu la kupeleka Injili ulimwenguni kote.

Dhiki kubwa ya mapito ya Yakobo (Matendo 7:11-12) ilijumuisha miaka saba ya njaa, lakini katika kipindi hicho, kipindi kibaya sana kilitokea mwishoni mwa miaka miwili, wakati Yakobo alipotakiwa kuiacha nchi ya Kanaani (1877 K.K.). Wakati Yakobo na familia yake walipoamriwa kuiacha nchi ya Kanaani, ilikuwa ni kama kuamrishwa kuuacha ufalme wa Mungu. Hakuna jambo ambalo lingeweza kudhikisha zaidi ya hilo. Ilimaanisha kwamba nchi ya ahadi, nchi ya Kanaani, ilikuwa imeachwa kwa wapagani waliokuwa katika ufalme wa Shetani. Kwa hiyo, kiishara, ilikuwa kana kwamba Shetani alikuwa amepewa utawala wa ufalme wa Mungu. Kwa hiyo, mwaka 1877 K.K., ulikuwa mwaka wa huzuni na wenye kuogofya sana.

Kadhalika, mwaka wa kutisha sana kati ya mapito ya Israeli ya miaka 70 ulikuwa mwaka 587 K.K., wakati Yerusalemu na hekalu, ambavyo pia viliwakilisha ufalme wa Mungu, vilipoharibiwa. Katika mwaka huo, kwa amri ya Mungu, hekalu na mji wa Yerusalemu viliangamizwa na mfalme wa Babeli, ambaye alimwakilisha Shetani (Isaya 14). Kwa mara nyingine, ilikuwa kana kwamba ufalme wa Mungu duniani ulikuwa umefikia mwisho.

Haya matukio mawili ya kihistoria yaliwakilisha kile kilichotokea katika mwaka wa yubile, 1994 B.K. Kwa miaka 1955, makanisa kila mahali ulimwenguni yalikuwa kiwakilishi cha ufalme wa Mungu, kama vile tu ilivyokuwa nchi ya Kanaani katika siku za Yakobo, na kama Yuda, na nchi ya Israeli, mji wa Yerusalemu, na hekalu vilivyokuwa katika siku za Israeli.

Tutatambua kwamba wakati fulani mapema kabla ya mwaka 1994, Mungu alikuwa amemaliza kuyatumia makanisa katika kuwakilisha ufalme wa Mungu. Kwa hiyo, mwaka wa ajabu wa yubile 1994 ulikuwa mwaka wa kuogofya kwa makanisa yote. Kila mahali ulimwenguni, Mungu kwa mara nyingine alikuwa anaokoa idadi ya watu wasioweza kuhesabika, lakini makanisa yalibakia chini ya utawala wa kiroho wa Shetani. Kwa hakika, Mungu alikuwa amemaliza kabisa kutumia makanisa katika kuwakilisha ufalme wa Mungu. Hali ilikuwa kama vile tu ilivyokuwa katika mwaka 1877 K.K., wakati nchi ya Kanaani ilipokuja kabisa chini ya utawala wa kipagani, na katika mwaka 587 K.K., wakati nchi ya Yuda ilipokuja chini ya utawala wa mfalme wa Babeli.

Mwaka 1877 K.K., uligawa dhiki ambayo Yakobo aliipitia katika sehemu mbili, kama vile mwaka 587 K.K., ulivyogawa kipindi cha miaka 70 ya dhiki iliyopitiwa na Israeli katika sehemu mbili. Kwa hiyo, pia dhiki kubwa ya siku hizi iligawanyika katika sehemu mbili katika

mwaka 1994, wakati ilipokuwa dhahiri kwamba Mungu alikuwa amemaliza kabisa kuyatumia makanisa katika kuwakilisha ufalme wa Mungu.

Kwa kuwa hivi vipindi viwili vya dhiki ya miaka saba na miaka sabini ni mifano ya dhiki kuu ya siku hizi, tungeweza kutegemea kwamba hiki kipindi cha dhiki ya sasa hivi pia kinahusisha namba saba. Tayari tumeishatambua kwamba sehemu ya kwanza ya dhiki kuu inaonekana kuhusiana na siku 2,300 za Danieli 8. Kwa sababu mapito ya dhiki ya Yakobo yalijumuisha miaka saba, na mapito ya dhiki ya Yuda yalijumuisha miaka 70, tunaweza kutegemea kwamba muda kamili wa kipindi cha dhiki kuu ya sasa hivi pia utakuwa na sehemu muhimu ya namba saba. Inaweza kuwa siku 7,000 au labda 7 x 12 x 100, ambayo ni sawa sawa na siku 8,400. Kiroho, namba 100 humaanisha “ukamilifu” na namba 12 humaanisha “utimilifu.” Baadaye tutatambua kwamba kipindi cha dhiki kuu ni siku 8,400 (miaka 23), na hii imethibitishwa kwa nguvu na taarifa ya ziada ya Ki-Biblia.

Zaidi, tutatambua usambamba uliopo katika kugawanyikwa ndani ya sehemu mbili kwa miaka saba, miaka 70, na siku 8,400. Kama ambavyo tumejifunza, kipindi cha miaka saba cha dhiki ya Yakobo kiligawanyika katika sehemu mbili. Tukio la kutisha la kuiacha nchi ya Kanaani lilikuwa mwishoni mwa miaka miwili ya mwanzo wa miaka saba (Mwanzo 45:6-8). Kwa hiyo, sehemu ya kwanza ilikuwa mbili-ya-saba, au 28.6% ya kipindi chote. Kadhalika, dhiki ya Yuda ilianza katika mwaka 609 K.K., wakati Mfalme Yosia alipofariki, na iliendelea mpaka mwaka 539 K.K., wakati Babeli iliposhindwa na Wamedi na Maajemi. Hiki kipindi cha miaka 70 kilikuwa kimegawanyika katika sehemu mbili, sehemu ya kwanza ilikuwa miaka 22. Ishirini na mbili ni 31.4% ya miaka 70.

Kumbuka, dhiki ya Yakobo na dhiki ya Yuda ni mifano ya dhiki kuu ya sasa hivi. Kwa hiyo, tungetemea sehemu ya kwanza ya dhiki kuu ya siku hizi nayo pia kuwa karibu na 28.6% au 31.4% ya kipindi chote cha dhiki kuu. Kwa hakika, tunaona kwamba siku 2,300 ni 27.4% ya siku 8,400. Tunaweza kuona mfanano uliopo kupitia ukaribu wa 27.4% kwa 28.6% na 31.4%. Baadaye tutatambua kwamba ushahidi mwingi sana ndani ya Biblia ambao unatuonyesha kwamba mgawanyo wa kujaribia wa siku 2,100 kama sehemu ya kwanza ya jumla ya siku 8,400 za kipindi cha dhiki kuu upo sahihi kabisa.

Kwa hiyo, tunajifunza kwamba siku 8,400 zinaonyesha namba 7 (7 x 12 x 100). Pia inaonekana kugawanyika katika sehemu mbili, sehemu ya kwanza kuwa karibu 30% ya wakati wote. Na kwa sababu miaka 23, ambayo ndani ya Biblia kila mara huwakilisha ghadhabu ya Mungu, ina urefu wa siku 8,400 kamili, kwa nguvu tunasaidiwa kuamini kwamba kipindi cha dhiki kuu kina urefu wa siku 8,400 kamili.

Tunasoma katika 1 Petro 4:17:

Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasiotii injili ya Mungu utakuwaje?

Katika mstari huu, Mungu anazungumza juu ya wakati wa maandalizi kwa ajili ya hukumu ya Mungu inayokuja, na inatakiwa kuanzia katika makanisa. Kwa hiyo, kipindi cha siku 8,400 (miaka 23) kinaweza kuwa kipindi hicho cha wakati.

Siku 2,300 ambazo zinafunganisha sehemu ya kwanza ya hii dhiki kuu pia zinaweza kufunganisha Ufunuo 8:1, ambapo tunasoma:

> **Hata alipoifungua muhuri ya saba, kukawa kimya mbinguni kama muda wa nusu saa.**

Muda wa karibu na “nusu saa” ulikuwa wakati ambapo kila mahali ulimwenguni, na ndani ya makanisa yote, karibu hakuna mtu aliyekuwa akiokolewa. Tunaweza kufahamu hivi kwa sababu tunasoma katika Luka 15:10:

> **Nawaambia, Vivyo hivyo kuna furaha mbele ya malaika wa Mungu kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye.**

Wakati watu wanapokuwa hawapati kuokolewa, kunakuwa kimya mbinguni kwa sababu hakuna furaha.

Kwa hiyo, tunatambua kwamba mwishoni mwa nyakati za kanisa, kuna kipindi cha siku 8,400 (miaka 23) ambacho kinaanza na kipindi cha siku 2,300, wakati ambapo ulimwengu wote, na hasa makanisa, yanaandaliwa kwa ajili ya siku ya hukumu.

Kwa mfano, hiyo ndiyo maana tunasoma katika Ufunuo 13:7-8 juu ya mnyama (Shetani) anayekuja kutoka baharini (katika ghadhabu ya Mungu), na ambaye anawashinda watakatifu (kuwaondoa makanisani), na pia kutawala juu ya ulimwengu.

Lakini, kama ambavyo tumeishaona, mwaka 1994 ulikuwa mwaka wa yubile, katika kipindi ambacho Roho Mtakatifu alimwagwa (Ezekieli 39:25-29; Yoeli 2:28-32), na kipindi kikubwa cha mwisho cha kuuhubiria Injili ulimwengu wote kilitokea. Tungependa kuamini kwamba hii ilimanisha kuwa makanisa yangetumiwa tena na Mungu. Walakini, kama tunavyojifunza, makanisa yaliyokuwa kila mahali ulimwenguni yalifananishwa na hekalu, na Mungu anatuhakikishia kwamba wakati ungekuja ambapo hekalu lingeharibiwa na kusingebakia jiwe juu ya jiwe (Mathayo 24:1-3). Hakuna mahali po pote tunaposoma kwamba hekalu lililozungumziwa katika Mathayo 24 lilijengwa tena baada ya kubomolewa. Hiyo ni kusema kwamba, kamwe Mungu asingeweza tena kulitumia kanisa lo lote katika kuleta Injili ulimwenguni.

Dhiki kuu inaendelea hadi siku 8,400, ambazo ni miaka 23 kamili. Hii inamaanisha kwamba kuanzia katika mwaka wa yubilie 1994, Mungu alitumia njia nyingine katika kupeleka Injili ulimwenguni. Hakutumia tena mikusanyiko (ya mahali pamoja) makanisa. Hiyo ni kusema kwamba, kwa namna fulani mwaka 1994 ulikuwa mwaka wa ajabu wa kuanza tena kwenda mbali sana na Injili katika ulimwengu wote. Kwa makanisa, huo ulikuwa mwaka wenye kuogofya sana. Hii ilikuwa hivyo kwa sababu makanisa yanatakiwa kuendelea mpaka mwisho wa siku 8,400 za kipindi cha dhiki kuu chini ya ghadhabu ya Mungu.

Tarehe ya Mwisho wa Nyakati za Kanisa

Habari ambayo tumeichunguza mpaka sasa hivi inatuhakikishia kwamba mwaka wa yubile 1994 ulikuwa mwisho wa kipindi cha siku 2,300, kipindi ambacho karibu hakuna mtu aliyekuwa akiokolewa mahali po pote ulimwenguni. Huo ukweli unatusaidia kutambua tarehe ya mwisho wa nyakati za kanisa, ambayo lazima inaafikiana na mwanzo wa miaka 23 (siku 8,400) ya dhiki kuu.

Kipindi cha siku 2,300 ni miezi michache zaidi kuliko miaka sita. Kwa hiyo, mwisho wa nyakati za kanisa lazima utakuwa ulitokea miaka sita mapema zaidi ya mwaka 1994. Kwa hiyo, lazima ulitokea katika mwaka 1988.

Ili kutambua siku halisi katika mwaka 1988 ambapo nyakati za kanisa zilikuja kufika mwisho, lazima tukumbuke kwamba nyakati za kanisa zilikuwa zimehusishwa na siku ya kusherekea sikukuu ya majuma, ambapo pia inaitwa siku ya Pentekoste. Iliadhimishwa katika Jumapili ambayo ilikuwa majuma saba baada ya Jumamosi ya kwanza (siku ya saba ya Sabato), ambayo ilikuja baada ya sikukuu ya Pasaka. Ilikuwa katika siku hiyo ambapo malimbuko au mavuno yalitakiwa kuletwa katika hekalu. Hii ilibashiri kuletwa kwa mavuno kutoka kila mahali ulimwenguni, mavuno ya kwanza ya waamini wa kweli ambao waliletwa katika ufalme wa Mungu. Mwanzo rasmi wa nyakati za kanisa ulikuwa katika siku ya Pentekoste katika mwaka wa 33 B.K. Hiyo siku, wakati ilipooanishwa na kalenda yetu, ilikuwa Mei 22, mwaka 33 B.K.

Wakati siku ya Pentekoste ilipowadia kila mwaka, kiroho, iliashiria mwanzo wa mavuno kwa ajili ya mwaka mwingine. Walakini, katika mwaka 1988 B.K., kuletwa kwa mavuno yaliyokuwa yakihusiana na Pentekoste kulifika mwisho. Kwa sababu katika mwaka 1988 B.K., Pentekoste ilitokea Mei 22, siku ya mwisho wa nyakati za kanisa ingekuwa siku kabla ya Mei 22, ambayo ilikuwa Mei 21. Kwa ajabu, hii inamaanisha kipindi cha kanisa, ambacho kilianza rasmi mnamo Mei 22, mwaka 33 B.K., kiliendelea kutokea mwaka 33 B.K. mpaka mwaka 1988, ambapo ni sawa na miaka kamili 1955, mpaka siku ile. Hii ni ishara nyingine ya usahihi wa ratiba ya Mungu ya matukio ya historia.

Kwa hiyo, Mei 21, 1988, ulikuwa mwisho rasmi wa nyakati za kanisa na mwanzo rasmi wa dhiki kuu. Siku 2,300 za sehemu ya kwanza ya dhiki kuu zilifika mwisho mnamo Septemba 7, 1994. Zaidi, Septemba 7, 1994, kwa mujibu wa siku ya sikukuu ya kalenda ya Biblia, ilikuwa Tishri 1, ambayo pia katika Biblia iliitwa sikukuu ya yubile. Kumbuka, neno “yubile” lina kila kitu kinachohusiana na kutuma Injili ulimwenguni.

Kufuatia kipindi cha siku 2,300, kuna siku 6,100 (8,400-2,300 = 6,100) zilizobakia kwenye kipindi cha miaka 23 (siku 8,400) ya dhiki kuu. Kwa hiyo, hizi siku 6,100 zitaisha mnamo Mei 21, 2011.

Mapema tulijifunza kwamba siku ya mwisho wa kuwepo kwa dunia hii, kama ilivyoonyeshwa kupitia maadhimisho ya sikukuu ya vibanda (sikukuu ya Biblia) ni Oktoba 21, 2011. Kwa hiyo, baada ya dhiki kuu lazima kutakuwapo na kipindi cha mwisho chenye siku 153, ambapo tutaona ni siku ya hukumu, wakati Mungu anapokamilisha utaratibu wa adhabu yake juu ya watu wasiookolewa.

Kwa neema za Mungu, kwa uangalifu tumeweza kutambua ratiba ya matukio ya historia Ki-Biblia moja kwa moja mpaka mwisho wa ulimwengu. Sasa tutaonyesha jinsi Biblia inavyotoa ushahidi mwingi wa usahihi wa hii ratiba ya matukio.

Kanuni ya msingi ambayo imetusaidia sana katika jitihada hii ni ile ambayo imeelezewa katika Wakolosai 2:16-17, ambapo Mungu anatangaza:

> **Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo.**

Katika mistari hii inayoerevusha sana, Mungu anatangaza kanuni kwamba mpangilio wa muda wa maadhimisho ya taratibu mbalimbali za sheria za ibada yanaelekeza na yanahusiana na mpangilio wa muda wa mambo yanayokuja. Kwa hiyo, kwa haraka tunafahamu kwa nini Yesu, Mwana-kondoo wa Mungu, alisulubiwa katika siku ya 14 ya mwezi wa kwanza (Nisan 14) wa kalenda ya Biblia, ambayo ilikuwa Pasaka. Pia tunaweza kufahamu kwa nini Roho Mtakatifu alimwagwa na nyakati za kanisa kuanza karibu majuma saba baadaye, katika siku ile ile Israeli waliposherekea sikukuu ya Pentekoste.

Unabii mwingine wa Biblia wenye msaada sana ambao mapema tulijifunza juu yake katika uchunguzi huu ulikuwa ni ule wa Marko 13:28-29, ambapo ndani yake Mungu anatufundisha:

> **Kwa mtini jifunzeni mfano; tawi lake liishapo kuwa laini, na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno ni karibu; nanyi kadhalika, myaonapo mambo hayo yanaanza, tambueni ya kuwa yu karibu milangoni.**

Taifa la Israeli mara kwa mara ndani ya Biblia linawakilishwa kama mtini. Baada ya kutokuwa na nchi au utambulisho wa taifa kwa karibu miaka 2,000, takriban katika hali ya kustaajabisha Israeli kwa mara nyingine ikawa taifa lenye uwezo wa kujitegemea ulimwenguni. Hili tukio kubwa sana limewakilishwa kiusahihi na waalimu wengi sana wa Biblia kama utimilifu wa huu unabii wa Marko 13. Kwa kuwa hili tukio lilitokea Mei 14, 1948, tunafundishwa na mistari hii kwamba haya matukio yote yaliyoelezewa kwa muhtasari katika Marko 13 yalipaswa kutokea haraka sana katika miaka iliyofuatia mwaka 1948.

Dokezo lingine la msaada linalotusaidia kutambua ratiba ya matukio yanayotuongoza kuelekea mwisho wa ulimwengu ni ukweli kwamba mwaka 1994 ulikuwa mwaka wa yubile. Mapema tulijifunza kwamba Yesu, ambaye ndiye hasa asili ya yubile, alizaliwa katika mwaka 7 K.K., ambao ulikuwa mwaka wa yubile. Kumbuka, yubile ilimaanisha kwamba uhuru (wokovu) ulitakiwa kutangazwa ulimwenguni.

Uchunguzi makini wa Marko 13, na sura zinazofanana kama Mathayo 24, na Luka 17, na Luka 21, unaonyesha kwamba matukio yafuatayo yangejitokeza wakati Mungu alipofunga historia ya ulimwengu.

1. Wakati ungekuja ambapo makanisa yote kila mahali ulimwenguni, yaliyokuwa yamewakilishwa kama hekalu la Mungu, yangefika mwisho. "**Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe"** (Mathayo 24:2). Wangetawaliwa na Shetani ambaye anaitwa "**chukizo la uharibifu"** (Mathayo 24:15).[9]

2. Huu ungekuwa wakati wa dhiki kuu wakati ambapo waamini wa kweli walifukuzwa na kuamriwa kuyaacha makanisa yao. Ungekuwa wakati wa ukanaji mkubwa wa imani makanisani, kwa sababu Shetani alikuja katika mengi ya makanisa hayo akiwa na ishara na miujiza (Mathayo 24:24).

3. Huu wakati wa dhiki kuu uliwakilishwa na miaka saba ya dhiki ambayo Yakobo aliipitia katika mwaka 1877 K.K., wakati alipoamriwa na Mungu kuiacha nchi ya ahadi, Kanaani, na kwenda katika nchi ya Misri.

4. Pia iliwakilishwa na kipindi cha miaka 70, mwaka 609 K.K. mpaka 539 K.K., kipindi ambacho Yuda ilikuwa chini ya ghadhabu ya Mungu. Hiki kilikuwa kipindi cha miaka 70 kutoka mwaka 609 K.K., wakati Yosia, mfalme mzuri wa mwisho, alipouawa, mpaka mwaka 539 K.K., wakati Babeli iliposhindwa na Wamedi na Waajemi, na hivyo, kuruhusu mateka wa Kiyahudi kurudi Yerusalemu. Katikati ya huu wakati wa kutisha uliopitiwa na Israeli katika mwaka 587 K.K., Yerusalemu na hekalu zuri la Sulemani viliharibiwa kabisa na Wababeli.

5. Kwa kiwango kidogo, tunaweza kutambua kwamba pia kilifananishwa na kipindi cha miezi saba wakati hema lilipokuwa Shilo na sanduku la agano lilipotekwa na Wafilisti na kuchukuliwa katika nchi yao. Hii ilitokea katika mwaka 1068-1067 K.K.

Kwa hiyo, namba 7 ilionekana kuhusika kwa ukaribu na kipindi cha dhiki kuu tunayoisoma katika Mathayo 24.

Tulijifunza kwamba katika uwezekano wo wote, namba 23 ilihusiana na kipindi cha dhiki kuu. Kwa kurudia rudia imetumika katika Biblia kuonyesha ghadhabu ya Mungu, na kipindi cha dhiki kuu kwa hakika ni kipindi ambacho Mungu anayaandaa makanisa na ulimwengu kwa ajili ya ghadhabu ya Mungu, ambayo mara itafuatia kipindi hiki. Namba 7 na 23 zote zilitokea kuwa muhumi sana wakati tulipotambua kuwa kwa usahihi siku 8,400 ni sawasawa na miaka 23 kamili. Namba 8,400 ni sawasawa na 7 x 12 x 100, hivyo kuruhusu namba 7 na namba 23 kuwa sehemu muhimu ya siku 8,400, yaani, kipindi cha miaka 23 ya dhiki kuu.

Tulitambua kwamba hiki kipindi cha dhiki ya siku 8,400 kilikuwa kimegawanyika katika sehemu mbili. Kwa mujibu wa kile tulichojifunza kutoka Ufunuo 8:1, katika kipindi cha sehemu ya kwanza, karibu hakuna mtu aliyekuwa akiokolewa mahali po pote ulimwenguni. Tuliihusisha sehemu ya kwanza na nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu za Danieli 8:13-14.

Tulitambua kwamba katika sehemu ya pili ya dhiki kuu, mkutano mkubwa sana wa watu, ambao hapa mtu awezaye kuuhesabu, ulikuwa ukiokolewa kila mahali ulimwenguni kote (Ufunuo 7:9-14). Hii kwa ujumla ilitakiwa kutokea nje ya makanisa, ambayo yanabaki chini ya ghadhabu ya Mungu.

Pia tulitambua kwamba utaratibu wa sikukuu ya vibanda (sikukuu ya Biblia), ambayo inatakiwa kuwa kivuli cha mambo yanayokuja, ilihusishwa na siku ya mwisho. Kwa sababu siku ya mwisho inahusiana na mwisho wa ulimwengu, mpangilio wa muda wa Biblia wa sikukuu ya vibanda lazima nao uhusiane na mwisho wa ulimwengu.

Sehemu moja ya taarifa ambayo ni ngumu zaidi lazima iwekwe akilini, na hiyo ni tangazo la Marko 13:24-26, ambapo tunasoma:

---

[9] Unakaribishwa kutumiwa vitabu vya bure *Mwisho wa Nyakati za Kanisa na Baada* na *Ngano na Magugu,* ambavyo vinatoa habari zaidi ya Ki-Biblia kuhusu mwisho wa nyakati za kanisa.

Lakini siku zile, baada ya dhiki hiyo, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake. Na nyota za mbinguni zitakuwa zikianguka, na nguvu zilizo mbinguni zitatikisika. Hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija mawinguni kwa nguvu nyingi na utukufu.

Hatuna budi kuendelea kujifunza zaidi juu ya kipindi hiki.

Kwa kutoa muhtasari wa yale yote ambayo tumeyatambua mpaka sasa, tunaweza kuhitimisha kwamba kukua kwa matukio yanayoandaa mwisho wa ulimwengu kunaonekana kuwa kama ifuatavyo.

1. Kipindi cha kanisa, ambacho kilianza katika mwaka 33 B.K., kingeisha wakati fulani baada ya mwaka 1948, wakati ambapo Israeli kwa mara nyingine ilipata kuwa taifa huru lenye uwezo wa kujitegemea miongoni mwa mataifa ya ulimwengu.
2. Kwa sababu kipindi cha kanisa kilianza wakati wa Pentekoste, na kwa ukaribu sana kimekuwa kikihusishwa na Pentekoste, kuletwa kwa mavuno ya mwanzo, basi mwisho rasmi wa kipindi cha kanisa, lazima uwe siku kabla ya tarehe ya Pentekoste katika mwaka wo wote ambao kipindi cha kanisa kilikuwa kifikie mwisho.
3. Kwa sababu sehemu ya mwisho wa dhiki kuu ilikuwa inahusisha mkutano mkubwa wa watu ukiwa unaokolewa, hiyo sehemu ya mwisho lazima ilianza katika mwaka 1994, ambao ulikuwa mwaka wa yubile.
4. Kwa sababu sehemu ya kwanza ya dhiki kuu inahusiana na siku 2,300 za Danieli 8, wakati ambapo karibu hakuna mtu aliyekuwa akipata kuokolewa, mwanzo wa dhiki kuu, ambao lazima utokee wakati mmoja na mwisho wa kipindi cha kanisa, lazima ulitokea wakati fulani katika mwaka 1988 (siku 2,300 kidogo zaidi ya miaka sita).
5. Kwa sababu mwisho rasmi wa kipindi cha kanisa lazima ulikuwa siku kabla ya Pentekoste katika mwaka 1988, tunatambua kwamba hiyo siku ya Pentekoste ilikuwa Mei 22. Kwa hiyo, mwisho wa kipindi cha kanisa na mwanzo wa dhiki kuu lazima viwe vimetokea Mei 21, 1988.
6. Kwa kuwa sehemu ya kwanza ya dhiki kuu, katika kipindi ambacho karibu hakuna mtu aliyepata kuokolewa, ilikuwa iwe siku 2,300, basi siku 2,300 baada ya Mei 21, 1988, zinatufikisha Septemba 7, 1994. Basi tarehe hii lazima iwe tarehe ya mwanzo wa mavuno makubwa ya watu ambao wanatakiwa kuokolewa katika siku 6,100 zilizobaki kati ya siku 8,400 (miaka 23 kamili) za dhiki kuu.
7. Mwisho wa siku 6,100 baada ya Septemba 7, 1994, ni Mei 21, 2011, siku ambayo lazima itakuwa mwisho wa dhiki kuu.
8. Katika mwaka 2011, siku ya mwisho ni ipi kwa sikukuu ya vibanda (sikukuu ya Biblia)?. Tumejifunza kwamba inatokea katika Oktoba 21, 2011. Kwa hiyo, kuna miezi mitano, zikijumuisha siku 153 za kalenda yetu, kipindi ambacho ndani yake matukio ya Marko 13:24-27 lazima yatokee. Kwa hakika, sasa hivi, tunatiwa moyo kwamba labda tumefika katika ufahamu sahihi wa kufunuliwa kwa matukio yanayotuongoza katika mwisho wa ulimwengu. Katika Ufunuo 9, Mungu anazungumzia kipindi cha miezi mitano ambayo inahusiana na wakati ambapo jua linatiwa giza na hukumu kuanza. Na siku 153, Mei 21 mpaka Oktoba 21, ni miezi mitano kamili.

Sura ya 5.

Je Ufahamu Wetu Juu ya Ratiba ya Matukio ya Historia Uko Sahihi?

Lakini sasa linakuja swali kubwa. Ni vipi tunavyoweza kuwa na uhakika wa hii ratiba ya matukio? Hii ni habari ya ajabu sana, kwa hakika tunategemea kwamba Mungu angetupa uhakika zaidi, kama kwa hakika huu ni ufahamu thabiti wa ratiba ya matukio ya mwisho.

Biblia inaandika tukio lingine la kustaajabisha lililotokea ambalo ni kiini cha mpango wa wokovu wa Mungu. Tukio hilo lilikuwa kufa na kufufuka kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Kama hatuwezi kuthibitisha kabisa kwamba Kristo alifufuka kama ushahidi kwamba alikuwa ametoa malipo kabisa kwa ajili ya dhambi za wateule, basi tungebaki na wasiwasi juu ya mpango wote wa wokovu.

Ili kutupa huo uhakika, tunasoma katika Matendo 1:1-3:

> **Kitabu kile cha kwanza nalikiandika, Theofilo, katika habari ya mambo yote aliyoanza Yesu kufanya na kufundisha, hata siku ile alipochukuliwa juu, alipokuwa amekwisha kuwaagiza kwa Roho Mtakatifu wale mitume aliowachagua; wale aliowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyohusu ufalme wa Mungu.**

Na Mungu anasema katika 1 Wakorintho 15:3-8:

> **Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu; kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alimtokea Kefa; tena na wale Thenashara; baadaye aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja; katika hao wengi wanaishi hata sasa, ila baadhi yao wamelala; baadaye akamtokea Yakobo; tena na mitume wote; na mwisho wa watu wote, alinitokea mimi, kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake.**

Biblia kwa uwazi inafundisha ya kuwa lilikuwa kusudi la Mungu kwamba ukweli wa kufufuka kwa Kristo ulikuwa unapita mabishano. Mtu ye yote anayeendelea kukana ukweli huu wa kustaajabisha, ana hekima tu machoni pake mwenyewe, na anafikiri anajua zaidi kuliko Mungu.

Kwa mshangao, wakati Mungu anapofungua macho yetu katika mpangilio wa muda wa matukio ya mwisho wa historia ya ulimwengu, Mungu pia anatoa mathibitisho mengi ambayo

yanatuhakikishia kwamba tumefahamu kwa usahihi mpango halisi wa muda wa matukio ya mwisho wa historia ya dunia.

Mpaka hapa tumeelezea kidogo dokezo la kujaribia mpangilio wa muda wa matukio ya mwisho wa ulimwengu. Kwa sababu ni matukio muhimu sana hatuna budi kuyatolea muhtasari kwa mara nyingine. Tumefika katika tarehe zifuatazo.

1. Kusulubiwa kwa Yesu kulikuwa katika siku ya 14 ya mwezi wa kwanza wa mwaka 33 B.K. Hii ilikuwa Nisan 14, mwaka 33 B.K., kwa kalenda ya Biblia, na ilikuwa Aprili 1, mwaka 33 B.K., kwa kalenda yetu ya siku hizi.

2. Kipindi cha kanisa kilianza rasmi katika Pentekoste iliyofuata, ambayo ilikuwa Mei 22, mwaka 33 B.K.

3. Kipindi cha kanisa kilifika mwisho na siku 8,400 za dhiki kuu zilianza siku kabla ya Pentekoste mwaka 1988, ambayo ilikuwa Mei 21, 1988.

4. Siku 2,300 za kwanza za dhiki kuu zilianza Mei 21, 1988, na kumalizika Septemba 7, 1994.

5. Sehemu ya pili ya dhiki kuu, ambayo inajumuisha siku 6,100 (8,400-2,300 = 6,100), ilianza Septemba 7, 1994, na inaishia Mei 21, 2011.

6. Miezi mitano ya mwisho wa historia ya ulimwengu inaanza Mei 21, 2011, na itaisha Oktoba 21, 2011.

Mpaka hapa tumeelezea dokezo la msingi wa miunganisho muhimu ya wakati inayoelekea kwenye mwisho wa ulimwengu. Pia tumeona taarifa ya Biblia ambayo inatufanya tufike katika hii habari ya wakati.

Lakini sasa tunahitaji kuchunguza tarehe zilizoelezewa katika hili dokezo la wakati katika mwangaza wa habari nyingine yo yote tunayoweza kupewa na Biblia. Tutatambua kwamba Mungu ametoa taarifa nyingi za ziada ambapo pasipo shaka yo yote tunaweza kujua kwamba kwa hakika hii ni ratiba sahihi. Sasa tutaeleza hatua kwa hatua ili kuonyesha jinsi hii mifano ya wakati inavyoshikamana kwa nguvu.

Tutaanza na muda wa kipindi cha kanisa, ambacho kilianza Mei 22, 33 B.K., na kuishia Mei 21, 1988. Wakati wa kipindi cha kanisa ulijumuhisha siku ya Mei 22, 33 B.K., na siku ya Mei 21 ya mwaka 1988. Hii inamaanisha kanisa liliendelea kwa kipindi cha miaka 1955 (1988-33 = 1,955) katika siku ile ile. Maneno “katika siku ile ile” yanakubaliana kabisa na usahihi wa matendo ya Mungu yaliyopita. Kwa mfano, Israeli walikuwa Misri kwa miaka 430 katika “**siku**

ile ile” (Kutoka 12:40-41). Inaweza kuonyeshwa kutoka katika takwimu za Biblia kwamba kutokea siku Israeli walipotoka Misri, mpaka Israeli walipowasili katika Mto Yordani kujiandaa kuvuka, ilikuwa miaka 40 katika siku ile ile.

Zaidi ya hayo, kwa sababu Kristo aliongea katika mifano tutaona sifa ya pekee ya hii miaka 1,955. Kumbuka, mfano ni hadithi ya kidunia yenye maana ya mbinguni. Kwa hiyo, maneno au namba (ambazo pia ni maneno), zinaweza kuwa na maana ya kawaida ya kidunia, na pia zinaweza kuwa na maana ya kiroho. Kwa hiyo, namba 3 kila mara kiroho husisitiza kusudi la Mungu. Hapa pangekuwa mahali pazuri kuelezea tena maana ya kiroho anayoisisitizia Mungu kila mara kupitia matumizi ya namba.

2 – Wale ambao wameagizwa kuleta Injili

3 – Kusudi la Mungu

4 – Mfiko wa mbele kabisa katika wakati au umbali ambao Mungu anao kiroho katika picha

5 – Upatanisho, ambao unasisitiza hukumu na wokovu

7 – Utimilifu kamili wa kusudi la Mungu

10 – Ukamilifu wa cho chote kilicho katika picha

11 – Ujio wa kwanza wa Kristo, 11,000 baada ya uumbaji

12 – Utimilifu wa cho chote kilicho katika picha

13 – Mwisho wa ulimwengu, habari ambazo zilianza miaka 13,000 kamili baada ya uumbaji

17 – Mbinguni

23 – Ghadhabu au hukumu ya Mungu

40 – Majaribu

43 – Ghadhabu au hukumu ya Mungu

Zaidi ya hayo, tumejifunza kutoka kwenye Biblia ya kwamba kama namba kubwa inaweza kugawanywa katika namba ndogo, ambayo kila moja ina maana ya kiroho, hiyo inaweza kutusaidia kufahamu maana ya ujumbe wa kiroho katika namba kubwa. Tunaweza kuhakikishiwa kwamba namba kubwa inatoa habari muhimu ya kiroho ambayo inatusaidia kufahamu mazingira ambayo imepatikana ndani yake.

Hii kanuni imetolewa katika miaka 1,955 ya kipindi cha kanisa. Namba 1,955 inaweza kugawanywa katika 5 x 17 x 23. Na hizi namba zote tatu kiroho zina uhusiano mkubwa na tabia ya kiroho ya kipindi cha kanisa. Tunasoma katika 2 Wakorintho 2:14-16:

> **Ila Mungu ashukuriwe, anayetushangiliza daima katika Kristo, na kuidhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu. Kwa maana sisi tu manukato ya Kristo, mbele za Mungu, katika wao wanaookolewa, na katika wao wanaopotea; katika hao wa pili harufu ya mauti iletayo mauti; katika hao wa kwanza harufu ya uzima iletayo uzima. Naye ni nani atoshaye kwa mambo hayo?**

Hii mistari inatufundisha kwamba Injili huleta wokovu na kifo. Wokovu unahusisha mbinguni (17). Kifo kinahusisha ghadhabu ya Mungu (23). Kumbuka kwamba namba 5 kiroho inahusisha upatanisho. Kwa hiyo, miaka 1,955 ya kipindi cha kanisa, kipindi ambacho Injili ilitakiwa kupelekwa ulimwenguni, kwa hakika kinahusisha asili na tabia ya Injili: 1,955 = 5 x 17 x 23. Kwa hiyo, miaka 1,955 ya kipindi cha kanisa inapatikana katika upatanisho (5), ambao unaleta mbingu (17) na kuleta ghadhabu ya Mungu (23). Je huku ni kubahatisha? Siyo kubahatisha hata kidogo. Inakubaliana kabisa na kanuni ambayo tumeielezea.

Maadhimisho ya Miaka 13,000 ya Ulimwengu

Wazo moja zaidi halina budi kutolewa kuhusiana na mwaka 1988. Je ni kwa bahati kwamba mwaka 1988 ni maadhimisho ya miaka 13,000 ya historia ya ulimwengu? Tumejifunza kutoka kwenye Biblia kwamba ulimwengu uliumbwa katika mwaka 11,013 K.K. Kama tunaongeza 11,013 katika 1988 na kutoa moja (kwa sababu hakuna mwaka sufuri tunapoenda kutoka Agano la Kale kwenda Agano Jipya), jumla inakuwa miaka 13,000. Kwa hakika mwaka

wa mwisho wa kipindi cha kanisa, ambao kwa usahihi unahusiana na maadhimisho ya miaka 13,000 ya ulimwengu, lazima unaonyesha kwamba Mungu anafuata mpango sahihi ulioandaliwa kabla.

Habari hii hasa inapata kuvutia pale tunapotambua kwamba kutoka mwaka wa uumbaji (11,013 K.K.), mpaka mwaka wa gharika la siku za Nuhu (4990 K.K.), wakati hukumu ya Mungu ilipokuja juu ya ulimwengu, ni miaka 6000 kamili kujumlisha miaka 23. Kumbuka, namba 23 kila mara humaanisha ghadhabu ya Mungu. Vivyo hivyo, kutoka mwaka 4990 K.K., mpaka mwaka 33 B.K., wakati Kristo alipobeba hukumu ya Mungu, ilikuwa miaka 5000 kamili kujumlisha miaka 23, yote pamoja. Sasa tunajifunza kwamba mwaka 2011 ni mwaka wa mwisho, na mwaka 11,013 K.K., mpaka 2011 B.K., ni sawasawa na miaka 13,000 kujumlisha miaka 23. Je haya yote ni kubahatisha? Kumbuka, kwa uangalifu tulihitimisha kwamba mwaka 2011 ulikuwa mwaka wa mwisho kwa sababu tulifahamu uwezekano mkubwa kwamba dhiki kuu ingekuwa muda wa siku 8,400 kamili. Na siku 8,400 ni miaka 23 kamili. Na 23 ikijumlishwa katika 1988 inatuleta katika mwaka 2011 kama mwisho wa ulimwengu.

Miaka 23 ya mwisho ambayo ilianza Mei 21, 1988, ni kipindi cha dhiki kuu, ambacho ni mwanzo wa wakati wa mwisho wa utaratibu wa hukumu ya ulimwengu wote. Inamaanisha kwamba Mei 21, 1988, ilimaliza kipindi cha kanisa, wakati ambapo hukumu ya dhiki kuu ilianza, kwa usahihi kulingana na unabii wa Biblia wa 1 Petro 4:17, "**hukumu lazima ianzie katika nyumba ya Mungu."** Hivyo tumejifunza kwamba kwa pamoja, mwaka 1988 na siku ya Mei 21, 1988, vinaafikiana sana na ufunuo wa ratiba ya matukio ya historia.

Tukio muhimu linalofuata katika kufunuliwa kwa ratiba ya matukio ya Mungu lilikuwa mwaka 1994. Tulijifunza kwamba Septemba 7, 1994, ilikuwa siku kamili 2,300 baada ya Mei 21, 1988. Kumbuka, tayari tumeishatambua kwamba mwaka 1994 ulikuwa mwaka wa yubile. Hiyo ni kusema kwamba, ni mwaka ambao ulisisitiza kusudi la kiroho la Mungu katika kutangaza Injili ulimwenguni. Sasa tunajifunza kwamba Septemba 7, 1994, ilikuwa siku ya kwanza ya mwezi wa saba (Tishri 1), wa utaratibu wa kalenda ya Ki-Biblia.

Tishri 1 ilikuwa utaratibu wa siku ya sikukuu ambayo iliitwa **"ukumbusho wa kuzipiga baragumu"** (Mambo ya Walawi 23:24) na "**siku ya kupiga tarumbeta"** (Hesabu 29:1).[10] Ilikuwa siku ile ile ya sikukuu ya Ki-Biblia ambayo ilitokea katika mwaka 29 B.K., wakati Yesu alipoanza rasmi kazi yake kama yubile au Masiha. Ilikuwa katika siku hiyo ambapo alitangazwa kama "**Mwana-kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu"** (Yohana 1:29). Katika mwaka 29 B.K., kwa mujibu wa kalenda yetu ya siku hizi, hiyo siku ilikuwa Septemba 26. Kwa mujibu wa kalenda ya Ki-Biblia, hiyo siku ilikuwa Tishri 1, ambayo ilikuwa sikukuu ya siku ya yubile au baragumu, kama ambavyo Septemba 7, 1994 ilivyo siku ya sikukuu ya yubile au baragumu.

Neno "yubile" lina kila kitu kinachohusiana na kutangazwa kwa uhuru ulimwenguni (Mambo ya Walawi 25:10). Hiyo ndiyo maana "*teruah*" limetafsiriwa kiusahihi "yubile" katika

---

[10] Kwa pamoja katika Mambo ya Walawi 23:24 na katika Hesabu 29:1, Mungu anazungumzia sikukuu ya siku ya kwanza ya mwezi wa saba. Katika mistari yote, neno la Kiebrania "*teruah"* limetafsiriwa kama "kupiga matarumbeta." Mara nyingi katika Biblia, neno "*teruah"* limetafsiriwa kama "toa sauti kuu" au "onyo la hatari" au "paza sauti." Lakini kamwe halijatafsiriwa "kupiga tarumbeta" isipokuwa katika hii mistari miwili. Lakini, katika Mambo ya Walawi 25:9, ambao unazungumzia siku ya upatanisho, limetafsiriwa "baragumu."

kuhusiana na siku ya upatanisho. Kristo ndiye asili ya upatanisho, na pia ndiye asili ya yubile. Kwa hiyo, wakati alipotangazwa Septemba 26, 29 B.K., kupitia Yohana Mbatizaji, kama tunavyosoma katika Yohana 1:29, "**Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu,"** lilikuwa tangazo takatifu kwa ulimwengu kwamba Kristo alikuwa "yubile" aliyekuja na Injili ya wokovu.

Vivyo hivyo, katika mwaka wa yubile 1994, Septemba 7, Injili kwa mara nyingine ilitakiwa kutangazwa katika ulimwengu wote. Na katika tarehe zote mbili, Septemba 26, mwaka 29 B.K., na Septemba 7, 1994, tarehe ya sherehe ya Biblia ilikuwa siku ya kwanza ya mwezi wa saba. Kwa hakika, kama ambavyo neno "*teruah"* limetafsiriwa kwa usahihi kama "baragumu" katika Mambo ya Walawi 25:9 kuhusiana na siku ya upatanisho, tunaweza kuona hivyo katika Mambo ya Walawi 23:24 na Hesabu 29:1, mistari ambayo inaongea juu ya "ukumbusho wa *teruah"* na "siku ya *teruah,"* na tunaweza kuelewa lilitakiwa kutafsiriwa kama "ukumbusho wa yubile" na "siku ya yubile." Kwa hiyo, hii sikukuu, ambayo wanateolojia wanaiita "sikukuu ya matarumbeta," ingeitwa "sikukuu ya yubile."

Kumbuka, tulijifunza kwamba Septemba 7, 1994, ilimaliza siku 2,300 za kwanza kati ya siku 8,400 za kipindi cha dhiki. Septemba 7, 1994, mkutano mkubwa wa watu, ambao hapana mtu anayeweza kuuhesabu, kila mahali ulimwenguni, ulianza kuja katika ufalme wa Mungu. Ilikuwa siku ambayo kwa mara ya pili katika historia ya ulimwengu, Roho Mtakatifu alimwagwa. Kama ingekuwa siku yo yote mbali na Septemba 7 katika mwaka 1994, isingehusiana na siku ya sikukuu ya mwezi mchanga wa Tishri 1, ambayo ilikuwa "**kivuli cha mambo yanayokuja"** (Wakolosai 2:16-17). Hili tukio la kustaajabisha, siku ya sikukuu ya utaratibu wa ibada ya Septemba 7, 1994 (Tishri 1, 1994), kwa hakila lilionyesha ishara na kuanza kwa kipindi cha mwisho cha siku 6,100 za wokovu.

Lakini mwaka 1994, mwaka ambao ndani yake Mungu alianza siku 6,100 za mwisho wa wokovu mkuu kila mahali ulimwenguni, pia ulikuwa mwaka wa hofu kuu kwa makanisa kila mahali ulimwenguni. Roho Mtakatifu alimwagwa, kwa hiyo nje ya makanisa, yaani, nje kabisa ya kanisa mahali po pote ulimwenguni, mkutano mkubwa sana wa watu ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, ungepata kuokolewa. Wakati huo huo, ndani ya makanisa, utaratibu wa hukumu ungeendelea. Shetani, ambaye alikuwa amewekwa ndani ya makanisa yote mwanzoni mwa dhiki kuu, angeendelea kutawala. Mungu angeendelea kuwaletea **"nguvu ya upotevu, wauamini uongo"** (2 Wathesalonike 2:11). Mungu angeendelea kuwaandaa wale walioko makanisani kwa ajili ya adhabu.

Ni masimulizi ya kutisha mno kupita kiasi kwa makanisa. Wao wenyewe hawatambui hili. Waamini wanamtumikia Kristo kwa uaminifu. Lakini Biblia inatupa ukweli. Kamwe hakutakuwapo na uwezekano tena wa wokovu kutokea chini ya mamlaka ya kanisa. (la mtaa).

Kumbuka, mapema katika uchunguzi huu, hali yao ya kuhuzunisha sana ililisitizwa wakati tulipochunguza mifano ya wakati wa vipindi vya historia ya dhiki kuu vilivyoelezewa ndani ya Biblia. Katika mwaka 1879 K.K., Yakobo alianza kupitia dhiki nyingi (Matendo 7:11) kwa sababu ya njaa kuu katika nchi. Miaka miwili baadaye, katika mwaka 1877, Yakobo aliamriwa kwenda na familia yake yote kuishi katika nchi ya Misri. Walitakiwa kuiacha nchi ya ahadi ambayo ilikuwa imetolewa kwa mkuu wa ukoo, Ibrahimu, babu yake, miaka 215 mwanzoni. Kwa sababu nchi ya Kanaani iliwakilisha ufalme wa Mungu, ilikuwa kana kwamba kuamriwa kuuacha ufalme wa Mungu. Kama vile katika mwaka 1988 B.K, Mungu alipoyatoa makanisa kwa utawala wa Shetani, ndivyo pia katika mwaka 1877 K.K., nchi ya ahadi, nchi ya

Kanaani ilivyotolewa kwa watu waovu wa ulimwengu kutawala huko. Huo kwa hakika ulikuwa wakati wa dhiki kubwa.

Mungu anashikamanisha hiyo dhiki na dhiki ya makanisa, wakati ambapo katika mwaka 1994, ni wazi kwamba Mungu alikuwa amemalizana nayo kabisa, na kuanza kuyaandaa kwa ajili ya hukumu. Kwa mara nyingine, wakati tunapochunguza namba ambazo zinahusianisha dhiki ya siku za Yakobo na wakati wa sasa hivi wa dhiki kuu, tunapata msisitizo zaidi juu ya tabia ya kiroho ya haya matukio yaliyopishana sana. Wakati tunapojumlisha 1877 katika 1994, na kutoa mwaka 1, tunapata jumla ya 3,870 kama idadi ya miaka katikati ya haya matukio ya kuhuzunisha. Namba 3,870 inagawanyika kwa 3 x 1,290, au 10 x 3 x 3 x 43. Namba 43 kwa kawaida humaanisha hukumu. Kwa hiyo, matukio mawili yameunganishwa pamoja na hii idadi ya miaka, ambayo inamaanisha kusudi (3 x 3) kamili (10) la Mungu katika kuleta hukumu (43). Namba 3 kurudiwa mara mbili siyo tu kwamba inamaanisha kusudi la Mungu peke yake, bali pia inamaanisha kwamba Mungu atalitimiza (Mwanzo 41:32).

Mapema katika uchunguzi huu tulijifunza kwamba pia Mungu anaunganisha huu wakati wa hukumu unaotisha juu ya makanisa, ambapo leo Shetani anatawala ndani yake, na dhiki kubwa ambayo Israeli iliipitia kwa miaka 70. Ilianza na kufa kwa Mfalme Yosia katika mwaka 609 K.K., na kuendelea kwa miaka 70, mpaka mfalme wa Babeli alipouawa katika mwaka 539 K.K. Mwaka 587 K.K., ulikuwa mwaka wa hiyo hofu kuu. Tayari katika mwaka 609 K.K., wakati Yosia mfalme mwema wa mwisho wa Israeli alipouawa, Israeli ilianza kuzidi kutawaliwa na wafalme wapagani ambao waliwakilisha utawala wa Shetani juu ya makanisa. Walakini, katika mwaka 587 K.K., Yerusalemu ilikuwa imeangamizwa kabisa, pamoja na hekalu. Nebukadreza, mfalme mwovu wa Babeli, ambaye anamwakilisha Shetani katika Biblia, alitokea kuwa mtawala kamili wa nchi ya Israeli. Inatisha sana!

Hili tukio la kuhuzunisha na lenye kutisha pia ni mfano ambao unatolewa na Mungu juu ya dhiki kuu ya siku hizi. Nalo pia linahusishwa na mwaka 1994 wa dhiki kuu ya sasa hivi kwa jumla ya miaka iliyopo katikati yake. Yerusalemu iliharibiwa katika mwaka 587 K.K. Kama tunaongeza 587 katika 1994, na kutoa 1, jumla inakuwa 2,580, ambayo inagawanyika kwa 2 x 1,290 au 10 x 3 x 2 x 43. Kwa sababu namba 2 kiroho huwakilisha wale wanaotakiwa kuleta Injili, ujumbe wa kiroho wa hiki kipindi cha miaka 2,580 ni kwamba lilikuwa kusudi (3) kamili (10) la Mungu juu ya makanisa, ambayo yalikuwa yameamriwa na Mungu kuleta Injili katika ulimwengu (2), kwamba yangekuja katika hukumu (43).

Katika hali ya kuvutia na yenye msaada sana, Mungu anahusisha haya mateso matatu ya Yakobo, Israeli, na ya siku hizi kupitia mstari katika Danieli 12:11, ambapo Mungu anatangaza:

Na tangu wakati ule ambapo sadaka ya kuteketezwa ya daima itaondolewa, na hilo chukizo la uharibifu litakaposimamishwa, itapata siku elfu na mia mbili na tisini.

Kwa kuwa wakati mwingine Biblia hutumia siku kuelezea mwaka (Ezekieli 4:6), tunajua tunaweza kuelewa hii kama miaka 1,290. Kulikuwa na miaka 1,290 katikati ya dhiki ya Yakobo ya mwaka 1877 K.K., na dhiki ya Israeli ya mwaka 587 K.K. Kadhalika, kuna 3 x miaka 1,290 katikati ya dhiki ya Yakobo ya mwaka 1877 K.K., na dhiki ya makanisa ya mwaka 1994.

Vivyo hivyo, kuna 2 x miaka 1,290 katikati ya dhiki ya Israeli ya mwaka 587 K.K., na dhiki ya siku hizi ya mwaka 1994.

Tafadhali angalia jinsi matukio haya yanavyoshikamana pamoja kwa ukaribu, ikionyesha kwamba, kwa hakika, uelewa wetu wa mwanzo juu ya kufunuliwa kwa ratiba ya matukio ya historia unazidi kuimarishwa zaidi na lugha ya Biblia.

Tukio la wakati linalofuata tunalotakiwa kulichunguza kwa makini ni Mei 21, 2011, ambayo ni siku ya mwisho wa siku 8,400, au miaka 23 kamili ya dhiki kuu. Kumbuka, tulijifunza kwamba hiyo inatakiwa kufuatiwa na kipindi cha siku 153 (miezi 5) za mwisho ambazo zinaisha Oktoba 21, 2011. Kwa kuwa Mei 21 na Oktoba 21 zote zinatokea katika mwaka 2011, ambao tunajifunza ni mwaka wa mwisho wa kuwepo kwa ulimwengu, tunatakiwa kuchunguza mwaka huo kwa makini sana.

Siku Moja ni Miaka Elfu

Mungu anavuta usikuvu wetu katika mwaka huo katika njia ya kuvutia sana. Katika 2 Petro 3:6, Mungu anazungumzia gharika ambalo liliangamiza ulimwengu wote katika siku za Nuhu, na hapo tunasoma:

> **Kwa hiyo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji, ikaangamia.**

Kisha katika mstari unaofuata, Mungu anaongea juu ya hukumu yenye kutisha ambayo itatokea mwishoni mwa ulimwengu. Tunasoma katika mstari wa 7:

> **Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu.**

Mara tu baada ya hii mistari hii miwili, Mungu anafanya kauli ya kipekee sana katika 2 Petro 3:8, ambapo tunasoma:

> **Lakini, wapenzi, msilisahau neno hili, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja.**

Ni “neno” gani lililopo katika picha wakati Mungu anaposema kwamba anataka wateule wote, ambao ni “wapenzi” wa Mungu, wasilisahau? Lazima liwe neno muhimu sana, na Mungu anasisitiza kwamba wanatakiwa kulijua. Hili neno kwa ujumla linahusiana na wakati.

Mungu anasema, “**kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja.”** Mara moja tunaona kwamba Mungu anazungumza juu ya neno hili mara mbili. Hiyo ni kusema kwamba, kwanza, Anatangaza, “**siku moja ni kama miaka elfu.”** Kisha anarudia habari hii kwa kusema “**miaka elfu ni kama siku moja.”** Hii kwa nguvu inaongeza umuhimu wa ukweli kwamba waamini wa kweli wote kwa hakika wanatakiwa kufahamu kwamba siku moja ni miaka elfu.

Kumbuka, Farao aliota kwanza kuhusu ng’ombe saba wanono ambao waligeuka kuwa ng’ombe dhaifu, na baadaye akaota juu ya masuke saba yaliyokuwa yamejaa ambayo yaligeuka kuwa membamba. Kuhusiana na tukio hili, Mungu alitoa kanuni ya Biblia katika Mwanzo 41:32, ambapo tunasoma:

> **Na ndoto ya Farao kwa vile ilivyokuja mara mbili, ni kwa sababu neno hilo Mungu amelithibitisha, na Mungu atalitimiza upesi.**

Sheria ambayo Mungu anaielezea katika mstari huu ni kwamba wakati Mungu anapofanya kauli mara mbili, inasisitiza ukweli kamili wa kauli hiyo. Cho chote kitakacho tokea kimehakikishwa kutokea, na kitatokea upesi. Kwa hiyo, kwa kurudia kauli kwamba siku moja ni miaka elfu, Mungu anatwambia kwamba ni muhimu sana, na kwa hakika itatokea upesi.

Lakini ni vipi habari hiyo inavyohusiana na mazingira ya 2 Petro 3, ambapo Mungu anaongea juu ya hukumu mbili za ulimwengu wote, hukumu ya siku za Nuhu na hukumu ya siku hizi? Wakati tunapoangalia kwa makini habari ya gharika iliyotolewa katika Mwanzo Sura ya 7, tunapata jibu letu. Lazima tuangalie safina, merikebu kubwa ambayo Mungu alimwamuru Nuhu kuijenga. Tunasoma katika Mwanzo 7:1-4:

> **BWANA akamwambia Nuhu, Ingia wewe na jamaa yako yote katika safina; kwa maana nimekuona wewe u mwenye haki mbele zangu katika kizazi hiki. Katika wanyama wote walio safi ujitwalie saba saba, mume na mke; na katika wanyama wasio safi wawili wawili, mume na mke. Tena katika ndege wa angani saba saba, mume na mke; ili kuhifadhi hai mbegu juu ya uso wa nchi yote. Kwa maana baada ya siku saba nitainyeshea dunia mvua, siku arobaini mchana na usiku; na kila kilicho hai nilichokifanya juu ya uso wa nchi nitakifutilia mbali.**

Kiroho, maji ya gharika yanawakilisha hukumu ya Mungu juu ya watu waovu wa ulimwengu wote wa siku za Nuhu. Safina iliwakilisha usalama kutoka katika hukumu ile, kwa hiyo, ilimwakilisha Mwokozi wetu, Bwana Yesu Kristo, ambaye yeye peke yake ndiye anaweza

kutulinda kutoka hukumuni. Wanyama waliwakilisha uumbaji wote, ambao unamwitaji Kristo kwa ajili ya ukombozi kutoka katika utumwa wa uharibifu (Warumi 8:19-23). Hii itatokea wakati Mungu anapoiumba mbingu mpya na dunia mpya.

Kwa hiyo, katika Mwanzo 7, Mungu kwa hakika anasema kwamba wanadamu wote katika ulimwengu wote wana siku saba kuingia katika usalama wa Kristo, ambaye yeye peke yake ndiye anayeweza kutuokoa na ghadhabu ya Mungu. Lakini subiri kidogo. Je Mungu hakusisitiza katika 2 Petro 3 kwamba kwa hakika tunatakiwa kufahamu kwamba siku moja ni kama miaka elfu? Hebu tubadili miaka 7,000 kwa siku saba. Kwa hiyo, kwa hakika Mungu alikuwa akimwambia Nuhu kwamba wanadamu wote ambao wangewahi kuishi katika ulimwengu wote wana miaka 7,000 kuingia katika usalama wa Kristo, kama wanataka kuepuka ghadhabu ya Mungu.

Ni mwaka gani ambao ungekuwa miaka 7,000 kamili baada ya gharika ya siku za Nuhu? Je unaweza kuamini! Zamani sana tulijifunza kwamba gharika ilitokea katika mwaka 4990 K.K., na miaka 7,000 baadaye inatuleta katika mwaka 2011. Kumbuka, tunajumlisha miaka ya Agano la Kale katika miaka ya Agano Jipya na kutoa mwaka 1, kwa sababu hakuna mwaka sufuri.

4990 + 2011 – 1 = miaka 7,000

Hivyo, lazima tufahamu kwamba Mungu kwa hakika anatangaza ya kuwa anategemea kwamba wateule wa Mungu wote wangejua kabisa kwamba mwaka 2011 unatakiwa kuwa mwaka wa mwisho wa ulimwengu.

Miezi Mitano ya Mwisho

Lakini kuna mengi zaidi yanayotakiwa kusemwa. Tumejifunza kwamba kuna kipindi cha miezi mitano ambacho mara tu kinafuata kipindi cha dhiki kuu ya siku 8,400. Je ni nini kinachoendelea katika wakati huo? Hii miezi mitano ya mwisho ambayo inaanza Mei 21, 2011, kwa nguvu imelenga katika mpango wa wokovu wa Mungu na katika mpango wa hukumu yake. Tutatambua kwamba katika siku ya kwanza ya hiyo miezi mitano, ambayo ni Mei 21, 2011, waamini wa kweli wote wanatakiwa kunyakuliwa ili kuwa na Kristo milele. Pia tutatambua kwamba ni siku ambayo hukumu ya jehanum kwa watu wote wasiookolewa.

Katika Ufunuo 9, Biblia inazungumzia wakati ambapo jehanum itaanza juu ya dunia hii. Inajumuisha kipindi cha miezi mitano (mstari wa 5 na 10). Sura inaanza na maneno kwamba “**shimo la kuzimu”** (neno lenye maana sawa na jehanum), limefunguliwa na moshi unapanda kutoka mle shimoni kama moshi wa tanuru kubwa. Kwa wakati huo, wale ambao walikuwa wamejithibitishia kwamba walikuwa wameokolewa kwa sababu walikuwa waalimu na wahubiri wa Biblia, lakini walikuwa hawajaokolewa, na walikuwa hawajanyakuliwa, bado wanaendelea

kujaribu kufundisha ufahamu wao wa Biblia uliopotoka. Wanawakilishwa na nzige (mstari wa 3), na wanatawaliwa na Abadoni (uharibifu) na Apolioni (mwangamizaji) (mstari wa 11), na wanawadhuru wale watu wanaoshi duniani kwa wakati huo. Walakini, hawatakiwi kuwadhuru wale ambao wana muhuri ya Mungu juu ya vipaji vya nyuso zao.

Roho ya kuzimu inatakiwa kupokea malipo ya uharibifu wa milele, kuangamizwa milele. Hii ndiyo maana hawa watu wasiookolewa wanatawaliwa na Abadoni na Apolioni (Ufunuo 9:11), ambayo ni majina yanayoelezea roho za kuzimu. Kwa sababu wapo kuzimu katika hii miezi mitano ya jehanum duniani,imehakikishwa kwamba watu wote wasiookolewa wataangamizwa milele. Kamwe, kamwe hawatokuwa hai tena. Wao, pamoja na ulimwengu wote, wataangamizwa. Hawawezi kuwadhuru waamini wa kweli ambao wana muhuri ya Mungu juu ya vipaji vya nyuso zao kwa sababu waamini wa kweli kamwe hawatakiwi kupitia jehanum. Waamini wa kweli watanyakuliwa (watainuliwa hewani), mara tu hii miezi mitano ya mwisho ya jehanum duniani inapoanza.

Katika Ufunuo 9:4, Mungu anasema:

> **Wakaambiwa wasiyadhuru majani ya nchi, wala kitu cho chote kilicho kibichi, wala mti wo wote, ila wale watu wasio na muhuri ya Mungu katika vipaji vya nyuso zao.**

Katika mazingira haya, majani, kitu kilicho kibichi, na miti vinawakilisha waamini wa kweli. Katika Ufunuo 15, Mungu anasisitiza mapigo ya mwisho, wakati wa mwisho wa jehanum duniani, na katika mstari wa 1 Mungu anasema, "**maana katika hayo ghadhabu ya Mungu imetimia."**

Kisha mstari unaofuata unatuhakikishia kwamba wakati huo huo, waamini wa kweli wote wako salama na Mungu juu ya "**bahari ya kioo."** Tunasoma katika Ufunuo 15:2:

> **Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto, na wale wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake, walikuwa wamesimama kando-kando ya hiyo bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu.**

"**Bahari ya kioo"** ipo mbinguni, kama inavyoonyeshwa na Ufunuo 4:2, "**...na tazama, kiti cha enzi kimewekwa mbinguni na mmoja ameketi juu ya kile kiti."** Mstari wa 6 unasema, "**Mbele ya kile kiti cha enzi kulikuwa na mfano wa bahari ya kioo."**

Waamini wa kweli watakuwa wameishanyakuliwa katika siku ya kwanza ya hiki kipindi cha miezi mitano ya mwisho, kwa hiyo watakuwa wamenusurika kabisa na maafa ya hicho kipindi cha wakati wa mwisho. Wakati ambapo hiki kipindi cha miezi mitano kitakuwa habari kubwa yenye kuogofya kwa wale ambao hawajanyakuliwa, utakuwa wakati wa furaha kuu na muujiza kwa wale ambao wamenyakuliwa.

Hiki kipindi cha miezi mitano kinajumuisha siku 153 kamili, Mei 21 mpaka Oktoba 21. Namba 153 kiroho inagawanyika kwa 3 x 3 x 17, kama ambavyo inafanya wakati tunapochunguza samaki 153. Kwa hiyo, kiroho, inawakilisha wale ambao kwao lilikuwa (kusudi) lengo (3) la Mungu kuwapeleka mbinguni (17). Namba 3 kujirudia inamaanisha kwamba Mungu kwa hakika atalitimiza.

Habari ya Kushangaza Zaidi

Kama ushahidi zaidi kwamba hii tarehe, Mei 21, 2011, ni tarehe ya unyakuo, tulitambua ukweli muhimu sana. Kwa mujibu wa utaratibu wa kalenda ya Biblia, Mei 21, 2011, ni siku ya 17 ya mwezi wa pili. Kwa usahihi, miaka 7000 iliyotangulia, katika siku ya 17 ya mwezi wa pili, kulingana na kalenda iliyotumiwa na Nuhu, Mungu alifunga mlango wa safina. Tunasoma katika Mwanzo 7:1 na 4:

> **BWANA akamwambia Nuhu, Ingia wewe na jamaa yako yote katika safina; kwa maana nimekuona wewe u mwenye haki mbele zangu katika kizazi hiki….Kwa maana baada ya siku saba nitainyeshea dunia mvua, siku arobaini mchana na usiku; na kila kilicho hai nilichokifanya juu ya uso wa nchi nitakifutilia mbali.**

Na tunasoma katika Mwanzo 7:10-11:

> **Ikawa baada ya siku hizo saba, maji ya gharika yakawa juu ya nchi. Katika mwaka wa mia sita wa maisha ya Nuhu, mwezi wa pili, siku ya kumi na saba ya mwezi, siku ile chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu, madirisha ya mbinguni yakafunguka.**

Na tunasoma katika mstari wa 13 na 16:

> **Siku ile ile Nuhu akaingia katika safina, yeye, na Shemu na Hamu na Yafethi; wana wa Nuhu, na mkewe Nuhu, na wake watatu wa wanawe pamoja naye; …Na walioingia, waliingia mume na mke, wa kila kitu chenye mwili, kama vile alivyomwamuru Mungu; BWANA akamfungia.**

Kalenda ya siku za Nuhu ilikuwa tofauti kidogo na kalenda ya baadaye ya Biblia kwa sababu ilikuwa na siku 30 kwa mwezi, wakati ambapo kalenda ya baadaye ya Biblia ilikuwa na siku 29 ½ kwa mwezi, kwa sababu ilifuata mabadiliko ya mwezi. Lakini Mungu, katika njia ya kustaajabisha, aliunganisha wakati wa kufunga mlango wa safina, katika siku ya 17 ya mwezi wa pili, na kufungwa kwa mlango Mei 21,2011, ambayo kwa mujibu wa utaratibu wa kalenda ya Biblia ni siku ya tarehe 17 ya mwezi wa pili. Hii milele iliwatengenisha waamini wa kweli walioko ndani ya safina kutoka kwa watu wote wa ulimwengu wasiookolewa ambao waliangamia nje ya safina. Hii ilitabiri ukweli kwamba katika tarehe ambayo ndani yake waamini wa kweli wanatakiwa kunyakuliwa, kamwe kusingekuwapo na uwezekano wo wote wa wokovu kwa wale walioachwa. Kwa hiyo, tunaweza kujua kwamba ni kana kwamba kuna miaka 7,000 kamili, kufika siku ile ile, kutoka kufungwa kwa mlango katika uwezekano wo wote zaidi wa wokovu, kwa pamoja katika kipindi cha kuangamizwa kwa ulimwengu wa siku za Nuhu na kuangamizwa kwa ulimwengu wote wa siku hizi. Je huku kunaweza kuwa ni kubahatisha?

Upatanisho Mpaka Unyakuo: Siku 722,500

Mungu anatupa habari nyingine muhimu na yenye kuvutia ambayo zaidi inaelezea usahihi wa Mei 21, 2011, kama tarehe ya unyakuo. Aprili 1, 33 B.K., Bwana Yesu alisulubiwa kwa ajili ya dhambi za wale aliokuwa amekuja kuwaokoa. Siku kamili 722,500 (zote pamoja) baadaye, unyakuo (Mei 21, 2011) utatokea. Hii namba inagawanyika katika namba muhimu sana:

(5 x 10 x 17) x (5 x 10 x 17) = 722,500

Tumejifunza maana ya kiroho ya hizi namba. Kazi ya upatanisho (5) imekamilika (10), wakati ambapo wateule wote wapo salama mbinguni (17). Huu ukweli wa kustaajabisha umerudiwa mara mbili kupitia kujirudia kwa namba tatu, 10 x 5 x 17. Huu msisitizo ni kwa mujibu wa Mwanzo 41:32, “**kwa sababu neno hilo Mungu amelithibitisha, na Mungu atalitimiza upesi.”**

Je tunaweza kuona jinsi ambavyo Mungu ameshikamanisha unyakuo wa Mei 21, 2011, na wakati mbingu ilipoleta (upatanisho), kwa sababu wakati Kristo aliposulubiwa, alifanya malipo yote kwa ajili ya dhambi za wale wanaotakiwa kuinuliwa juu mbinguni ili kuwa pamoja na Yesu milele?

Sasa hivi katika uchunguzi wetu, hatuna budi kupumzika kidogo na kutafakari kile ambacho tumejifunza katika aya zilizopita.

Tuna uhakika kabisa kwamba kusulubiwa kwa Kristo kulitokea katika siku ya sikukuu ya Pasaka, ambayo ilikuwa Ijumaa, katika mwaka 33 B.K., ambayo ilikuwa siku ya 14 ya mwezi wa

kwanza wa utaratibu wa kalenda ya Biblia. Pia tuna uhakika kabisa kwamba hii siku ilikuwa Aprili 1, 33 B.K., kulingana na kalenda yetu ya siku hizi. Ilikuwa katika siku hiyo ambapo Kristo aliadhibiwa kwa ajili ya dhambi za wale wote aliokuwa amekuja kuwaokoa. Kwa sababu Kristo alitoa malipo kwa ajili ya dhambi zao, walihakikishiwa kwenda mbinguni ili kutawala pamoja naye milele.

Kutoka katika habari nyingi tulizopewa ndani ya Biblia, tumetambua kwamba katika hiyo Mei 21, 2011, wale wote waliookolewa kupitia malipo ya Yesu, ambayo yalifanywa wakati wa kusulubiwa kwake, watatambua ukamilifu wa wokovu wao wakati wanaponyakuliwa (kuinuliwa juu) mbinguni. Kwa hiyo, ni wazi kabisa kwamba tarehe 1 Aprili, 33 B.K., na 21 Mei, 2011, kiroho zimehusianishwa pamoja kwa ukaribu sana.

Lakini pia tulitambua kwamba hizi tarehe mbili, ambazo karibu zinapishana kwa miaka 2,000, pia kwa nguvu zinashikana pamoja na namba halisi ya siku zinazozitenganisha pamoja na maana ya kiroho ya hiyo namba kubwa ya siku.

Angalia tena namba 722,500. Je si inastaajabisha kabisa kwamba inagawanyika kwa usahihi katika makundi mawili muhimu sana ya namba za kiroho, 10, 5 na 17? Mungu peke yake, aliyeumba huu ulimwengu mkubwa ukiwa na sheria zake zote sahihi, ndiye ambaye angeweza kupanga ratiba ya matukio ya historia katika njia sahihi na ya ajabu. Tafadhali! Ni uwezekano gani kwamba mahusiano haya ya wakati yangekuwa ya kubahatisha? Jibu linatakiwa kuwa, kamwe yasingekuwa ya kubahatisha.

Mathibitisho Zaidi

Tunaendelea kujifunza mathibitisho mengine ambayo yanaonyesha kwamba tumefikia ufahamu sahihi wa mpangilio wa muda wa mwisho. Kama tulivyoona, Mungu anaisisitiza hii tarehe, Mei 21, 2011, kwa kuweka siku ya kufunga mlango, wakati utakapotokea unyakuo katika siku ya 17 ya mwezi wa pili wa kalenda ya Biblia. Kwa umuhimu, namba 17 inahusiana bila kasoro katika ukweli wa unyakuo kwa sababu kiroho, namba 17 humaanisha mbinguni. Zaidi ya hayo, namba 2 (mwezi wa pili) kiroho huwakilisha wale ambao wameamriwa kuleta Injili. Je si inashangaza kwamba watanyakuliwa katika siku ya 17 ya mwezi wa pili? Je huko ni kubahatisha?

Pia tumejifunza kwamba siku ya mwisho wa kuwepo kwa dunia, Oktoba 21, 2011, ni siku ya 23 ya mwezi wa saba wa kalenda ya Biblia. Namba 23 kwa kawaida humaanisha kumwagwa kwa ghadhabu ya Mungu. Namba 7 (mwezi wa saba) humaanisha utimilifu kamili wa makusudi ya Mungu. Je huku pia kungekuwa kubahatisha, kwamba ukamilisho wa mwisho wa hukumu ya Mungu juu ya watu wasiookolewa unatokea katika mwezi wa saba, katika siku inayojumuisha namba 23, ambayo ni namba inayohusisha kabisa ghadhabu ya Mungu, hivyo kumaanisha ghadhabu kamili ya Mungu juu ya watu wasiookolewa?

Usahihi wa ratiba ya matukio ya mwisho wa ulimwengu unasisitizwa zaidi wakati tunapochunguza hiki kipindi cha miezi mitano ya mwisho kutoka katika mtazamo wa ghadhabu ya Mungu. Wakati Mungu alipomwadhibu Yesu, wakati alipokuwa anatoa malipo kwa ajili ya dhambi za wateule, inavuta usikivu wetu katika ukweli kwamba adhabu fulani kwa ajili ya

dhambi za watu wasioteuliwa bado lazima itatokea. Hizi adhabu mbili zinashikamanishwa pamoja na miaka 1,978 ambayo inatenganisha muda wa msalaba (33 B.K.) kutoka muda wa mwisho (2011 B.K.).

2011 – 33 = 1,978

1978 = 2 x 23 x 43

Namba 2 humaanisha wale wanaotakiwa kuleta Injili

Namba 23 humaanisha ghadhabu

Namba 43 humaanisha hukumu

Hivyo, kupitia namba 1,978, Mungu anasisitiza kwamba hukumu itashuka juu ya wale waliokuwa wameamriwa kuleta Injili (2) na bado wanaelekea katika ghadhabu ya Mungu (23 na 43).

Utaratibu wa Hukumu ya Mungu Unaendelea Wakati Mkutano Mkubwa Unaokolewa

Wakati tunapochunguza kwa makini tarehe za dhiki kuu, unyakuo, na siku ya mwisho wa kuwepo kwa ulimwengu, tunagundua ukweli mwingine wenye kuvutia. Tumejifunza kwamba katika siku 6,100 za mwisho kati ya siku 8,400 za kipindi cha dhiki kuu, waamini wa kweli, ambao watakuwa nje ya makanisa, wanatumiwa na Mungu ili kuleta ndani ya ufalme wa Mungu, mkutano mkubwa wa watu ambao hapana mtu awezaye kuwahesabu. Wakati huo huo, wanachama wote wa kanisa wanaandaliwa kwa ajili ya kuingia katika kipindi cha miezi mitano ya mwisho wakati hukumu ya Mungu ya mwisho inapotokea kwa ajili yao. Lakini wakati huo huo, katika hizi siku 153 za mwisho, wale wote waliokuwa wameokolewa katika siku 6,100 zilizopita watakuwa salama mbinguni, pamoja na wale wote waliookolewa kwa wakati wote. Hizi siku 6,100, wakati zinapoongezwa katika siku 153 za mwisho, inaleta jumla ya siku 6,253. Namba 6,253 inagawanyika katika namba muhimu 13 x 13 x 37.

Namba 13 ni mwisho wa ulimwengu

Namba 37 ni hukumu ya Mungu.

Kumbuka, Nuhu alikuwa katika safina kwa siku 370 kamili. Pia, kumbuka, jeshi la Waashuru la watu 185,000 chini ya Senakeribu liliangamizwa na Mungu katika usiku mmoja (2 Wafalme 19:35), na 185,000 = 1,000 x 5 x 37. Kwa hiyo, tunaweza kuona jinsi namba 37 inavyohusiana na uharibifu ambao ni matokeo ya hukumu ya Mungu.

Kupitia namba 6,253 Mungu anatuhakikishia kwamba wakati kukiwa na mkutano mkubwa ambao utakuwa unapitia wokovu katika kipindi hicho cha nyakati, utaratibu wa

hukumu ya Mungu (37) utakuwa umekamilika mwishoni mwa ulimwengu (13). Kwa mara nyingine, tafadhali angalia kujirudia kwa namba 13.

Mapema katika uchunguzi huu, tulithibitisha mpangilio wa muda wa mwisho wa historia katika hali ya kupapasa kidogo, kutoka tu katika taarifa ya Biblia. Lakini, baadaye, kwa kuendelea kutumia taarifa ya ziada ya Biblia kwa makini, tumetambua kwamba mpangilio wa muda ulikuwa sahihi sana. Uthibitisho baada ya uthibitisho umesisitizwa. Kama mpangilio wa muda unaoelezewa sasa hivi hauko sahihi katika moja ya tarehe zake, mathibitisho mengi yangekuwa yamebatilishwa Kwa hakika, kama tarehe yo yote tuliyojifunza kutoka kwenye Biblia haiko sahihi, basi mathibitisho mengi yasingefahamika tena. **Pasipo shaka tunaweza kuwa na uhakika kwamba unyakuo utatokea Mei 21, 2011, na siku ya mwisho wa historia ya ulimwengu ni Oktoba 21, 2011.**

Lakini hizi siyo tu habari za kisomi au kitaaluma. Hizi ni kweli ambazo zinahusika kwa njia ya pekee kwa kila mtu (karibu watu billioni saba) ambaye anaishi katika dunia hii. Je inawezekana kupona hiyo siku ya hukumu yenye kutisha.

Sura ya 6.

Je kuna Tumaini kwa ajili Yangu?

Biblia kwa uwazi inasema kwamba Bwana Yesu Kristo atakuja kama mwivi wakati wa usiku (2 Petro 3:10; 1 Wathesalonike 5:2). Tumejifunza kwamba hili lilitakiwa kueleweka wakati wote wa kipindi cha kanisa. Kwa hiyo, wanafunzi wa Biblia na wanateolijia hawakuhitaji kujihusisha na mpangilio wa muda wa kurudi kwa Kristo. Walilazimika kulenga kwenye jukumu la mara moja la kupeleka Injili katika ulimwengu wote (Matendo 1:6-8).

Lakini, tumejifunza kwamba karibu sana na wakati wa mwisho wa ulimwengu, waamini wa kweli wangefahamu mambo mengi juu ya ratiba ya matukio ya historia (Mhubiri 8:5-6; 1 Wathesalonike 5:3-5; Ufunuo 3:3).

Tupo katika wakati mzuri wa historia, na kwa hiyo, kwa hakika, kwa usahihi mkubwa wa Biblia tumeweza kutambua siku, mwezi, na mwaka wa mpangilio wa muda wa mwisho wa mwisho wa ulimwengu.

Kwa kuwa mwisho wa wakati umekaribia sana, kwa hakika tungetakiwa kufanya shauri pamoja: JE KUNA TUMAINI KWA AJILI YANGU? Kwa hakika, kuna tumaini kubwa kwa ajili ya kila mtu anayeishi leo. Hii iko hivi kwa sababu Mungu kwa uhakika anatuhakikishia kuwa wakati huu katika historia, mkutano mkubwa sana wa watu, ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, unaokolewa (Ufunuo 7:9-14). Kwa hiyo, kwa ufupi hatuna budi kujadili mpango wa wokovu wa Mungu. [11]

Katika (Marko 1:14b-15), Marko 14-15, Yesu anatangaza amri ya Mungu kwa wanadamu:

> …**Yesu akaenda Galilaya, akiihubiri Habari Njema ya Mungu, akisema, Wakati umetimia; tubuni, na kuiamini Injili.**

Kuiamini Injili kama mstari huu unavyoamuru inamaanisha kutambua kwamba Injili inatoka katika kinywa cha Mungu. Kwa hiyo, Injili bila shaka ni ya kweli, ni muhimu sana, na kwa hakika ni yenye mamlaka. Ni sheria ya Mungu, Biblia, ambayo kila mtu anatakiwa kuitii. Kwa hiyo, mtu anayeiamini Injili lazima ajaribu kuwa mtii inavyowezekana, kwa kiwango anachoweza kuelewa Biblia.

Kila mtu kwa asili, kwa kiwango fulani ana uwezo wa kufanya kazi fulani ya kiroho, pamoja na ile ya kuamini na kuitii Biblia. Hii ni kwa sababu sheria ya Mungu imeandikwa

---

[11] Kwa uchunguzi wa kina wa mpango wa wokovu wa Mungu, unakaribishwa kupiga simu au kuiandikia Redio ya Familia ili kupata bila malipo, kitabu cha *Natumaini Mungu Ataniokoa.* Anwani ni: Family Radio, Oakland, CA 94621. U.S.A. Au unaweza kupiga simu: 1-800-543-1495. Anwani yetu ya barua pepe ni: familyradio@familyradio.org

moyoni mwake (Warumi 2:14-15), na Mungu amempa dhamiri kiasi kwamba ana uwezo wa kutambua mema na mabaya. Hata kama amekufa kiroho, kwa pamoja katika mwili na roho, kiasi kwamba hakuna uwezekano wa yeye mwenyewe kupokea uzima wa kiroho, bado kwa kiasi fulani ana uwezo wa kutii sheria za Mungu. Kila mtu, kwa kiasi fulani hutubu au hugeuka kutoka katika dhambi zake. Kwa hiyo, ana uwezo wa kuishi maisha ya uadilifu. Kwa asili, amekufa kiroho kwa sababu yeye ni wa uzao wa Adamu, wazazi wetu wa kwanza. Wakati Adamu alipotenda dhambi katika Bustani ya Edeni, kimsingi, wanadamu wote walitenda dhambi kwa sababu wote tulikuwa katika sehemu ya mwili wa Adamu (1 Wakorintho 15:22).

Lakini, kwa hakika hana uwezo wa kupata kuokolewa, yaani, kupokea uzima wa milele katika mwili wake au katika nafsi yake. Hii iko hivi kwa sababu Injili inaonyesha kwamba malipo ya sheria ya Mungu yanayodaiwa kwa ajili ya dhambi ni kwamba mtenda dhambi anapaswa kuadhibiwa kupitia kifo cha aibu. Kwa hiyo, mtu ye yote ambaye amehukumiwa katika hiki kifo cha aibu kwa ajili ya dhambi zake kamwe hatopata kuwa hai tena, na amepoteza urithi wa ajabu wa uzima wa milele. Hii ndiyo maana kila mmoja wetu lazima atafute mtu kuwa mbadala wetu au kusimama katika kubeba hii adhabu kwa niaba yetu.

Hili agizo la Marko 1:15, katika kuamini Injili na kutubu (kuacha kutenda dhambi na kuitii Biblia), lilitolewa karibu miaka 2,000 iliyopita. Linatangaza kwamba "**Wakati umetimia."** Ilikuwa katika wakati huo ambapo Yesu, Masiha alikuja kufanya malipo yaliyodaiwa na sheria ya Mungu kwa niaba ya wale aliokuja kuwaokoa.

Leo, maneno, "wakati umetimia" yanahusika zaidi katika mpango wa wokovu wa Mungu kwa sababu tupo katika wakati mfupi sana kutoka katika kukamilishwa kabisa kwa mpango wa wokovu wa Mungu. Wakati tunapochunguza huu mpango wa wokovu wa ajabu kwa ajili ya ulimwengu, tunapata kufahamu kwamba kimsingi kuna watu wa aina tatu ulimwenguni. Watu hao ni kama wafuatao:

1. Wale ambao katika maisha yao yote hawajawahi kusikia neno lo lote la Biblia.

2. Wale ambao wamesikia mafundisho ya Biblia, lakini wanadharau au wanaidhihaki Biblia, au wanaijia Biblia wakiwa na mawazo yao kabla ya kujua ukweli.

3. Wale wanaoamini kwamba Biblia ni Neno la Mungu na ambao kwa bidii na kwa unyenyekevu wanatamani wokovu, zaidi kulingana na ukweli wa Biblia.

Wale Ambao Kamwe Hawajawahi Kusikia

Wakati wote wa historia ya ulimwengu, kuna wale ambao wameishi na kufa pasipo kuwahi kusikia au kusoma maneno yo yote kutoka kwenye Biblia. Na kwa sababu "**Imani**

chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo” (Warumi 10:17), lazima tuamini kwamba hakuna watu miongoni mwa hawa watu waliokuwa wameteuliwa na Mungu ili wapate kuokolewa. Kwa hiyo, haikuwa muhimu kwa Mungu wakati wo wote katika kipindi cha uhai wao kuwaweka chini ya usikivu wa Neno la Mungu.

Wale Ambao Wamesikia Neno lakini Ni Watu wa Dhihaka

Kutokea wakati Mungu alipotoa agizo la kutubu na kuiamini Injili (Marko 1:15), lilikuwa kusudi la Mungu kwamba katika ulimwengu, watu wengi sana ilivyowezekana wangekuja chini ya usikivu wa Injili. Hiyo ndiyo maana karibu miaka 2,000 iliyopita, Yesu aliamuru kwamba waamini wa kweli wote wanatakiwa kupeleka Injili ulimwenguni kote (Mathayo 28:19-20).

Kwa huzuni, matokeo ya watu wengi sana ambao kwa kiasi fulani walipata kuifahamu Biblia, ama waliidharau au kuidhihaki, au walifuata sheria zao binafsi badala ya sheria za Biblia, wakati wakijaribu kuelewa ukweli wa Biblia. Wale walioidhihaki Biblia waliamini kulikuwapo na makosa na kupingana ndani ya Biblia, na kwa hiyo, hawakuwa na shauku wala kuhitaji kuiamini. Wale walioijia Biblia wakiwa na njia yao ya kutafsiri iliyotengenezwa na mwanadamu, au waliokuwa wameweka tumaini lao katika makanisa yao, au madhehebu yao kama mamlaka ya mwisho, badala ya kuiamini Biblia, pia walipata kutii mafundisho ambayo hayakuwa kweli katika Biblia.

Biblia hufundisha kwamba watu wasiookolewa, kwa kiasi fulani wanaweza kutii sheria za Mungu. Huu ukweli unaelezea tumaini potofu la watu wengi. Kwa mfano, hii ni kweli kwa wale ambao ni wanachama wa makanisa ambayo yanafundisha mawazo matano ya mafundisho ya Calvin, ambayo yametokana na Sheria za Dort, kanuni za imani ya zamani.[12] Wazo la kwanza ni kwamba tunatakiwa kuamini kwamba kabla hatujaokolewa, tunakuwa tumepotoshwa kabisa. Kwa sababu wanachama wa makanisa haya wanaishi maisha mazuri na maadilifu, na ni watiifu katika sheria za kanisa lao, wanajua hawawezi kupotoshwa kabisa. Wamekuwa wakifundishwa na maungamo yao kwamba upotovu kabisa ni hali ya kiroho ya watu wasiookolewa. Kwa hiyo, maisha yao ya kumcha Mungu na uaminifu katika kanisa lao, pamoja na ukweli kwamba wamekwisha batizwa kwa maji na ni wanachama waaminifu wa kanisa lao, kwa hakika huwahakikishia kwamba kwa sababu hawajapotoka kabisa, hivyo, lazima Mungu atakuwa amewaokoa. Wanashindwa kutambua kwamba ushahidi wa wokovu ni shauku kubwa ya kuwa mtiiifu kwa Biblia yote. Hivyo, wamenaswa katika hali ya watu wasiookolewa kwa sababu ya kuamini mahitimisho ya teolojia isiyo ya Biblia.

Mfano mwingine unaweza kuangaliwa. Katika makanisa mengine mengi, msingi wa wokovu unaofundishwa ni mtu binafsi kumkubali Yesu kama Mwokozi pamoja na ubatizo wa

---

[12] Sheria za Dort, au kanuni za imani, ni hitimisho la mafundisho yaliyoshikiliwa na makanisa ya Kipresibiteri na makanisa ya Kiprotestanti yasiyopenda kubadilika ambayo kwa karibu yanafuata mahitimisho ya teolojia ya John Calvin, mwanateolojia maarufu, aliyeishi karibu miaka 400 iliyopita.

maji. Katika makanisa haya, haya matendo, pamoja na kuwa mwaminifu katika sheria za kanisa, na kuishi maisha maadilifu, vinaonekana kuwa ushahidi mwingi sana wa wokovu. Lakini, ni mpango wa wokovu uliobuniwa na wanateolojia badala ya mpango sahihi wa wokovu uliotolewa ndani ya Biblia, ambao ndani yake ushahidi wa wokovu ni shauku kubwa yenye kuendelea kuwa mwaminifu katika kila kitu kilichoko ndani ya Biblia.

Kwa hiyo, makanisa ya siku hizi ambayo yanadai yanafuata kwa makini mafundisho yote ya Neno la Mungu lisilo kosea, Biblia, yamejawa na hawa watu waaminifu, waadilifu, ambao ni wanachama katika ushirika kamili. Hawa watu wapendwa hawafahamu kwamba bado wapo chini ya ghadhabu ya Mungu, wala hawaoni hitaji lo lote la kuchunguza kwa makini mafundisho ya kanisa lao ili kubainisha kama kanisa lao ni aminifu kabisa kwa Biblia.

Onyo la 1 Wathesalonike 5:2-4 linatakiwa kuwashitua. Hii iko hivyo kwa sababu karibu wote walioko makanisani wanaamini wako salama pamoja na Kristo, na kwa hiyo, wanaridhika na kuamini kwamba Kristo atakuja kama mwivi wakati wa usiku. 1 Wathesalonike 5:2-4 inatangaza:

> **Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula, kama vile utungu umjiavyo mwanamke mwenye mimba, wala hakika hawataokolewa. Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi.**

Uharibifu wa ghafla unaweza tu kuwa unarejea katika siku ya hukumu ambayo imekaribia sana. Inatisha sana kwamba hawa wapendwa bado wanaelekea katika ghadhabu kamili ya Mungu ambayo lazima itakuja kwa kila mtu ambaye hajaokolewa.

Katika mifano mingi, hawa watu ni wastahifu, watu waadilifu ambao ni wacha Mungu sana na wanachama waaminifu wa kanisa. Lakini, kwa kuijia Biblia wakiwa na mafundisho yao ya uongo (yasiyogeuka) ya kujitungia, ambayo yanafundishwa na kanisa lao, kwa hakika, wanakuwa hawalisikilizi Neno la Mungu. Wanasikiliza na kutamani kutii mafundisho ya uongo ya kanisa lao, badala ya mafundisho ya Biblia nzima. Pasipo kutambua, mara nyingi wanasoma Biblia, na kisha, katika akili zao, wanageuza ukweli wa Biblia kujaribu kuufanya ukubaliane na mawazo yao yasiyobadilika. Kwa hiyo, hawasikilizi Biblia wakiwa na shauku ya kuitii.

Biblia inafanya marejeo mengi katika tabia ya aina hii. Siku zote inaonya kwamba hiyo tabia itasababisha ghadhabu kamili ya Mungu kushuka juu ya wale wanaodharau Neno lake kwa njia hii. Haiwapi moyo au tumaini kwamba labda Mungu anaweza kuwaokoa. Kwa hakika, wao wenyewe hawaoni hitaji la tumaini la aina hiyo. Wanaamini tayari wameishaokolewa, au kulingana na mpango wao wa wokovu wa jifanyie mwenyewe, wanaamini wanaweza kuokoka wakati wo wote wanapotaka.

Ukweli wa ajabu na wenye kuogofya ni kwamba Mungu anatambua aina hii ya uasi wa kiroho na kwa kawaida huwaacha hawa watu katika uasi wao. Kwa mfano, tunasoma kwamba Yesu alikuja Nazarethi kuhubiri, na Biblia inaripoti katika Marko 6:5-6:

Wala hakuweza kufanya mwujiza wo wote huko, isipokuwa aliweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache, akawaponya. Akastaajabu kwa sababu ya kutokuamini kwao. Akazunguka-zunguka katika vile vijiji, akifundisha.

Wakati ambapo kwa hakika Mungu alikuwa na nguvu ya kuwafanya watu wa Nazarethi wamwamini, kwa hakika anasisitiza kwamba watu ambao hawana shauku ya kuwa watii katika Neno la Mungu lote wapo katika hatari kubwa kiroho. Mwitikio wa Mungu wa kawaida kwa watu wa aina hii umenenwa wazi kabisa, kwa mfano, tunasoma katika Yeremia 26:4-6:

Nawe utawaambia, BWANA asema hivi, Kama hamtaki kunisikia, kwenda katika sheria yangu, niliyoiweka mbele yenu, kuyasikiliza maneno ya watumishi wangu, manabii, niliowatuma kwenu, naam, nikiondoka mapema na; lakini ninyi hamkuwasikiliza; basi, nitafanya nyumba hii kuwa kama Shilo, na mji huu nitaufanya kuwa laana kwa taifa zote za dunia.

Wale Ambao kwa Unyenyekevu Wanaamini Biblia Inatakiwa Kufuatwa

Biblia inaongea juu ya watu wa aina ya tatu, na hao ni wale wanaosikiliza Biblia na kwa bidii wanataka sana kuitii Biblia. Wanaamini kwamba Biblia, ambayo ni Injili, ni sheria ya Mungu ambayo inahubiriwa kwao. Wanatambua kwamba wao ni watenda dhambi wenye aibu na wapo katika taabu kubwa na Mungu. Wanatambua kwamba kila neno ndani ya Biblia linatoka katika kinywa cha Mungu, na kwa hiyo, wanatakiwa kulisikiliza kwa makini. Wanatambua ukweli kwamba Mungu peke yake ndiye anayeweza kuwaokoa, na licha ya kuwa wangetakiwa kuadhibiwa kupitia kifo cha milele kwa sababu ya dhambi zao, wanatumaini kwamba labda Mungu anaweza kuwahurumia (Luka 18:13). Wanajaribu kuwa watii katika kila wanachokifahamu juu ya Biblia, wakifahamu vizuri kabisa kwamba matendo ya utii wao hayachangii kwa njia yo yote katika wokovu au kuhakikisha kwamba Mungu atawaokoa. Wanaweza kujifunza kwamba sasa hivi Mungu anaokoa mkutano mkubwa sana wa watu, na kwa sababu Mungu ni mwenye huruma, na wao pia labda wanaweza kupata kuokolewa.

Na kwa hiyo, wanamlilia Mungu kwa ajili ya huruma zake, wakifahamu kwamba ni kwa neema ya Mungu tu wasiyostahili, iwapo wangepata kuokolewa. Kwa sasa, wakati wakimngojea Mungu kwa unyenyekevu (Maombolezo 3:26), wanajaribu kujifunza kila wanachoweza kutoka kwenye Biblia, ili kwamba waweze kuwa watiifu inavyowezekana katika sheria ya Mungu.

Hatuwezi kufahamu ni kwa nini tabia ya watu wa kundi la tatu ni tofauti sana na ile ya kundi la pili. Inaweza kuwa Mungu anawavuta katika maandalizi ya kuwaokoa. Inaweza kuwa ni matokeo tu ya ukweli kwamba sheria ya Mungu imeandikwa katika mioyo yao, na dhamiri yao inawaonya juu ya madhara ya dhambi. Ukweli muhimu siyo tu <u>kwa nini</u> wana hii tabia ya kuitii Biblia. Ukweli muhimu ni kwamba <u>wana</u> hii tabia ya kuitii Biblia. Lazima tukumbuke kwamba wakati wo wote, mtu ye yote, ambaye anatii sheria za Mungu anafanya kazi ya kiroho. Lakini

hiyo kazi kamwe haiwezi kuwa mchango katika wokovu wa mtu (Waefeso 2:8-9). Wokovu utakuja tu kwa wateule, na kazi ya kuteua ni kazi ya Mungu kabisa. Hiyo ndiyo maana Mungu anaweza kumwokoa mtoto mchanga au mtu ambaye kabisa ana matatizo ya akili ambaye yupo chini ya usikivu wa Biblia.

Katika maongozi ya Mungu yasiyoelezeka, Mungu hutoa masikio ya kiroho kwa wateule, ambao ni miongoni mwa wale wanaosikiliza Neno la Mungu kimwili. Tunasoma katika Mathayo 11:15:

Mwenye masikio, na asikie.

Hivyo, tunaweza kufahamu kwamba, Mungu katika hili swala la wokovu lisiloweza kuelezeka, anazungumzia watu kutoka katika sura mbili tofauti. Kwa upande mmoja, Anaongelea wale ambao kimwili wapo chini ya usikivu wa Injili, na ambao, kama wana uwezo wo wote hata kufahamu kidogo Neno la Mungu, watajaribu kuwa watiifu katika Biblia. Katika kutii kwao, wanaomba rehema za Mungu; kwa unyenyekevu wanamngojea Mungu, wakitumaini kwamba, na wao pia wanaweza kupata kuokolewa. Katika kutaka kwao sana kuwa watii, angalau wapo katika mazingira (Biblia) ambayo ndani yake Mungu atawaokoa iwapo Mungu anapenda kuwaokoa.

Kwa upande mwingine, Mungu anatoa maonyo mengi kwa wale ambao wapo chini ya usikivu wa kimwili wa Neno la Mungu, lakini ambao hawatasikiliza kwa nia ya unyenyekevu katika kutii Neno la Mungu. Lakini matendo yao, kwa hakika yanaonyesha wanalidharau Neno la Mungu. Mungu kwa kurudia rudia anaonya kwamba matendo hayo, iwapo yataendelea, yataishia na hukumu ya fedheha kamili, laana, kupoteza urithi, na hukumu ya kifo ambavyo vyote ni sehemu ya ghadhabu ya Mungu dhidi ya dhambi.

Huu sio wakati wa kujivuna, kujipendelea, kujitukuza wala kujiheshimu nafsi. Siyo wakati wa kiburi cha kiroho au majisifu ya kiroho. Ni wakati ambapo tunatakiwa kutambua kabisa mamlaka yote ya Biblia juu ya maisha yetu, na kwa hiyo, kusikiliza kwa makini sana katika kile ambacho Mungu anamwambia kila mmoja wetu.

Ni wakati ambapo kila mtu anatakiwa kutambua kabisa aibu ya dhambi zake, na uhakika kwamba kwa sababu ya dhambi zake, anastahili sheria kamili ya ghadhabu ya Mungu. Ni wakati wa kumsihi Mungu kwa unyenyekevu kwa ajili ya huruma yake tusiyoistahili. Huruma yake ya ajabu ni kubwa sana, zaidi mtu ye yote miongoni mwetu anavyostahili au anavyoweza kufikiri.

Leo, katika huruma yake kuu na ya ajabu, Mungu anaokoa mkutano mkubwa sana wa watu. Kwa hiyo, inawezekana kwamba, wakati mtu ye yote miongoni mwetu anapoomba rehema kwa unyenyekevu, kama bado hatujaokolewa, tunaweza kuwa miongoni mwa wale waliojumuishwa katika huo mkutano mkubwa ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu.

SWALI MOJA KUBWA NI: Je unamsihi Mungu kwa unyenyekevu kwa ajili ya wokovu, ukifahamu vizuri kabisa kwamba haustahili wokovu hata kidogo, huku ukitafakari aibu

yako ya kutotii na kuasi kwako dhidi ya sheria za Mungu? Wakumbuke watu wa Ninawi (Yona 3:6-10).

MUNGU AMHURUMIE KILA MMOJA WETU!